**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

| | |
|---|---|
| Mhe. Pandu Ameir Kificho | - SPIKA |
| 1. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | - MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3. Mhe. Omar Yussuf Mzee | -MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4. Mhe. Haji Omar Kheri | -MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | -MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | -MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7. Mhe. Abubakar Khamis Bakary | -MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8. Mhe. Hamad Masoud Hamad | -MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole. |
| 9. Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | -MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa |
| 10. Mhe. Juma Duni Haji | -MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |
| 11. Mhe. Zainab Omar Mohammed | -MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |

| | |
|---|---|
| 12. Mhe. Abdillah Jihad Hassan | -MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni |
| 13. Mhe. Ali Juma Shamuhuna | -MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge. |
| 14. Mhe. Mansoor Yussuf Himid | -MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki |
| 15. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | -MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16. Mhe. Said Ali Mbarouk | -MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando |
| 17. Mhe. Haroun Ali Suleiman | -MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi |
| 18. Mhe. Suleiman Othman Nyanga | -MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | -MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20. Mhe. Machano Othman Said | -MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21. Mhe. Othman Masoud Othman | - Mwanasheria Mkuu |
| 22. Mhe. Issa Haji Ussi | -Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Zahra Ali Hamad | - Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24. Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | -Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 25. Mhe. Bihindi Hamad Khamis | -Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26. Mhe. Haji Mwadini Makame | -Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27. Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | -Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28. Mhe. Abdalla Juma Abdalla | - Jimbo la Chonga |
| 29. Mhe. Abdalla Moh'd Ali | - Jimbo la Mkoani |
| 30. Mhe. Abdi Mosi Kombo | - Jimbo la Matemwe |
| 31. Mhe. Ali Mzee Ali | - Kuteuliwa na Rais |
| 32. Mhe. Ali Abdalla Ali | - Jimbo la Mfenesini |
| 33. Mhe. Ali Salum Haji | - Jimbo la Kwahani |
| 34. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - Nafasi za Wanawake |
| 35. Mhe. Asaa Othman Hamad | - Jimbo la Wete |
| 36. Mhe. Asha Abdu Haji | - Nafasi za Wanawake |
| 37. Mhe. Asha Bakari Makame | - Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. Ashura Sharif Ali | - Nafasi za Wanawake |
| 39. Mhe. Bikame Yussuf Hamad | - Nafasi za Wanawake |

40. Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

41. Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

42. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

43. Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

44. Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

45. Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

47. Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

48. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

49. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

50. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

51. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

52. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

53. Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

54. Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

55. Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

57. Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

58. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

61. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

62. Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

63. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

65. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

67. Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

68. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

69. Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

70. Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

72. Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

73. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

74. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

76. Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

77. Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

78. Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

79. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

80. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 20 Julai, 2011**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 153**

**Msongamano wa Majahazi kwenye Chelezo – Malindi**

**Mhe. Hassan Hamad Omar -** Aliuliza**:-**

Ni ukweli usiopingika kuwa Sekta ya Uvuvi ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Ukizingatia sekta hii imeajiri watu wengi kuliko sekta nyengine binafsi. Kwa masikitiko makubwa kuna kero ya msongamano wa majahazi ya mizigo katika uwazi wa Soko Kuu la Samaki Malindi, ukizingatia pia kuna chelezo katika eneo hilo.

Ni lini majahazi haya yatatengewa sehemu yao ya kushusha na kupakia mizigo ili kuvipa nafasi vyombo vya wavuvi kuegesha na kuuza bidhaa zao kwa wasaa na usalama.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 153 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Sekta ya Uvuvi ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu na hasa ukizingatia kuwa sekta hii imeajiri watu wengi kuliko sekta nyengine za binafsi. Mhe. Spika, msongamano mkubwa wa vyombo unaoonekana katika eneo baina ya Soko Kuu la Samaki na Chelezo cha Malindi unatokana na kuwa eneo hilo ni dogo na linatumiwa kwa pamoja na vyombo vya uvuvi na vya mizigo.

Mhe. Spika, vyombo vya mizigo (Majahazi, Mashua na Maboti) vinalazimika kutumia eneo hilo kushusha mizigo kwa sababu ya ukosefu wa nafasi katika Gati ya Majahazi iliyopo bandarini. Vyombo hivyo vimekuwa vikilitumia eneo hilo kwa muda mrefu sasa kutokana na kukua kwa shughuli za bandari.

Hata hivyo, kwa kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Idara yake ya Uvuvi inaendelea na uratibu wa Mradi wa Ujenzi wa sehemu ya kuhudumia vyombo vya uvuvi *(Fish Landing Site)* katika eneo hilo, mradi huo utakapokamilika utatoa nafasi nzuri kwa vyombo vya uvuvi kuegesha, kuhifadhi na kuuza bidhaa zao kwa wasaa.

Mhe. Spika, kwa upande wa wizara yetu tunaamini kwamba baada ya kupata ujenzi wa bandari mpya ya Maruhubi matatizo haya yatakuwa yameondoka.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba katika msongamano huu huwa unasababisha vita wakati watu wanapotoka baharini kuja kuuza samaki kwa kugongeana mashine zao. Je, Mhe. Waziri wizara yako imejipanga vipi kutatua msongamano uliopo ili wananchi wauze samaki wao kwa usalama bila ya mgogoro.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, matatizo anayosema Mhe. Mwakilishi yana njia mbili. Kwa upande wa utatuzi wa suala hili ni utatuzi wa kudumu na kwa vyovyote utahitaji muda mrefu na mipango yake kama nilivyoeleza. Lakini kwa utatuzi wa muda mfupi nadhani ipo haja ya kukaa tukazungumza tukakubaliana namna gani ya kuweza kutumia nafasi hii ndogo ili wote waweze kupata huduma nzuri na kuendeleza shughuli zao kama kawaida.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, huo mradi wa ujenzi wa sehemu ya kuhudumia vyombo unaendelea, umeanza lini na uko wapi.

Mhe. Spika, swali (b) mradi huo umezingatia vipi ufinyu wa udogo wa sehemu hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, katika majibu yangu mama nilieleza kwamba eneo lile ni dogo. Matarajio yetu kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanaanza utaratibu wa kujenga chelezo kwa ajili ya vyombo vya uvuvi. Mategemeo yangu kwamba eneo wanalolijenga litakapokamilika linaweza likapunguza kadhia hii. Eneo hilo lipo baina ya chelezo na kwenye sehemu ya kiwanda cha *Blue Marine* wanapotengeneza *edible oil.*

Mhe. Spika, ni matarajio yangu kwamba wenzetu hawa Wizara ya Mifugo na Uvuvi watakapokamilisha suala hili basi matatizo haya mengi yanaweza yakawa yamepata ufumbuzi na yatapungua.

Mhe. Spika, ningependa kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Shirika la Bandari tuliahidi kwamba siku 30 zinaweza zikatutosha kwa ajili ya kufanyia ukarabati tishali kubwa ambalo lilikuwa likitumiwa kwa huduma za usafiri bandarini.

Mhe. Spika, napenda kulithibitishia Baraza lako tukufu kwamba Shirika la Bandari wamekamilisha marekebisho yale, tishali limerejeshwa na huduma ile imerudi, pia ule usumbufu waliokuwa wakiupata wananchi umeshaondoka.

**Nam. 202**

**Masafa Marefu Kufuata Huduma za Elimu**

**Mhe. Hija Hassan Hija –** Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Zanzibar imekuwa ikitajwa kufikia viwango vya kimataifa vya kupunguza masafa marefu kwa kuwapatia watoto wake huduma ya elimu kwa kuwajengea majengo ya skuli na kuwapatia vitabu na walimu. Pamoja na mafanikio hayo bado baadhi ya maeneo ya Zanzibar wanafunzi wanatoka mbali kupata huduma za elimu mfano wanafunzi wanaotoka vijiji vya Ngomeni ambao husoma Skuli ya Ngwachani.

(a) Kwa kuwa wanafunzi wanaoishi Ngomeni hupata masomo yao Skuli ya Ngwachani zaidi ya kilomita 8. Je, Serikali haioni haja ya kujenga Skuli ya Msingi eneo la Ngomeni.

(b) Kutokana na vipingamizi mbali mbali vinavyowakabili watoto wa Ngomeni kielimu, watoto wengi huacha masomo njiani kwani mbali na masafa marefu lakini pia suala la barabara na afya ni vikwazo vinavyochangia wanafunzi wa Ngomeni kuacha masomo yao. Je, Wizara haioni haja ya kushawishi wahusika wengine ili kuitengeneza barabara hiyo ya Ngomeni – Kiyuni na kuwajengea Kituo cha Afya.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 202 lenye sehemu (a) na (b) lakini kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikishirikiana na wananchi katika sehemu mbali mbali imefanikiwa kufikisha huduma za elimu karibu sana na maeneo wanayoishi wananchi wengi. Ni katika vijiji vichache tu ndio huduma za elimu hazijafikia. Pia ni kweli kuwa watoto wa kijiji cha Ngomeni wanasoma katika Skuli ya Ngwachani Wilaya wa Mkoani Pemba kutokana na ukosefu wa skuli katika kijiji chao. Sera ya Elimu inawaagiza wananchi kuanzisha ujenzi wa skuli mpya ya msingi au madarasa katika maeneo na serikali na wahisani watachangia juhudi za wananchi hao kwa kumalizia ujenzi huo. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika,

a) Wizara iko tayari kushirikiana na wananchi wa Ngomeni katika ujenzi wa skuli ndogo ya msingi. Hivi sasa wananchi wa Ngomeni wameanzisha skuli ya maandalizi yenye madarasa mawili na Wizara imesaidia mifuko 20 ya saruji na pia imewapatia walimu wawili wa jamii mafunzo ya ualimu wa maandalizi. Ni matarajio yangu kuwa skuli hiyo ya maandalizi itakua hatua kwa hatua na baadae itaweza kuchukua madarasa ya awali ya msingi ili watoto wadogo wa Ngomeni waweze kusoma karibu na kijiji chao.

b) Nakiri kuwa huduma ya barabara na kituo cha Afya ni muhimu sana kwa ustawi wa wananchi wote wa Ngomeni wakiwemo watoto wa umri wa kwenda skuli, ingawa hizo zinatolewa na sekta zilizoko nje ya mamlaka yangu. Kwa vile Mhe. Waziri wa Afya na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano wanakisikia kilio cha wananchi wa Ngomeni ni matarajio yangu watashirikiana na wananchi ili huduma hizo ziweze kupatikana kijijini hapo.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba wanafunzi wa Ngomeni wanasoma masafa marefu Skuli ya Ngwachani. Kwa kuwa wanafunzi wale ni kuanzia darasa la kwanza hadi la saba. Kwa kuwa Ngomeni ni sehemu moja ambayo mvua ikinyesha huwa hakupitiki. Kwa kuwa Ngomeni Mhe. Spika, ni eneo moja ambalo karafuu huzaliwa kwa wingi.

(a) Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuishawishi serikali kuwajengea kituo cha afya na kuendelezwa angalau kwa kifusi barabara yao ili watoto wetu waweze kupita.

(b) Kwa kuwa sehemu kubwa ya wananchi wa Ngomeni ni sehemu ya wananchi wa Jimbo la Kiwani. Je, Mhe. Waziri atakuwa tayari kuambatana na mimi kwenda kufanya harambee kuanzia ujenzi huo wa skuli ya msingi.

**Mhe. Spika:** Hebu Mheshimiwa jibu haya maswali yanayohusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, haya mengine kama kuna wenyewe hapa wanaweza wakajibu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, wizara iko tayari kushirikiana na mwakilishi kwenda kufanya harambee ili tuweze kupata skuli katika eneo hilo la Ngomeni.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu iko tayari kuzungumza nae ili kuona namna gani tunaweza tukawasaidia wananchi hao kuondosha usumbufu huo wa barabara.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kila wilaya kuna Kamati ya Afya ambao wanajua ni maeneo gani yanatakiwa kujengwa. Naomba Mhe. Mwakilishi awasiliane na Kamati ya Afya inayohusika ili wajue kama kuna haja ya kujenga kituo kijijini hapo.

**Nam. 179**

**Kifaa cha *Ultra Sound***

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza**:-**

Wakati tunafanya kazi za Kamati tulipokea kilio cha watu wa Makunduchi kuwa wamepata misaada ya machine ya *ultra sound* kutoka Kampuni ya *Hips Healthing Improvement* ya Uingereza. Ni chombo ghali na cha kisasa ambacho kinahitaji hifadhi na utaalam maalum.

Je, Mhe. Waziri, Serikali itawasidia vipi wananchi wa Makunduchi kuwapatia utaalam wa kuitunza na kuifanyia kazi mashine hiyo na pia kupata mazingira yanayokubalika kwa ajili ya matunzo na huduma nzuri za mashine hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 179 kama ifuatavyo:

Ni kweli mashine ya *Ultra Sound* ipo katika hospitali ya Makunduchi kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa wanaofika kituoni hapo.

Katika hospitali hiyo kuna wataalam wawili wa *x-ray* ambao wameshajifunza kutumia mashine hiyo chini ya uangalizi wa daktari wa kigeni. Mwishoni mwa wiki wataalam hao wanakuja hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya mazoezi zaidi.

Tatizo la chumba cha *Ultra Sound* ni joto wakati mashine inapotumika, kuna mpango wa kuweka *AC* kupitia *district support fund* na itakuwa inafanyiwa *service* kila baada ya muda wa kufanya utakapofika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kuna uhakika gani kuwa *AC* itapatikana kwa mpango huu alioutaja.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, uhakika ninao kwa sababu pale kuna watu ambao wanalishughulikia suala hilo. Kuna wafadhili na Kituo cha Makunduchi kiko chini ya mpango wa *Pilot*. Kwa hiyo, nina uhakika kwa sababu nimezungumza nao baada ya kuliona hili suala na wamenambia kwamba *AC* inatiwa kwa sababu maabara wameshatia na huku watatia. Chumba kile mwanzo hakikuwa cha *ultra sound* isipokuwa mashine ilikuwa imeshafika na ilikuwa lazima iwekwe. Kwa hiyo, imewekwa mashine baadae watakiandaa chumba.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba tena kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe kwamba baadhi ya majibu ya maswali haya tuliyaeleza kwa urefu kwenye bajeti. Hivi sasa naomba Mhe. Mwakilishi arudie kitabu chetu kuna Mradi wa Huduma za Afya Wilayani Unguja na Pemba wa kuimarisha *Cottage Hospitals.* Sidhani kwamba milioni 45 tutashindwa kununua *AC.*

**Nam. 190**

**Wafanyabiashara wa Mafuta Kunyanyasa Wananchi**

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla -** Aliuliza**:-**

Wafanyabiashara ya mafuta hasa wanaoendesha vituo vidogo vidogo vinavyouza mafuta wamekuwa wakiwatesa wateja kwa kusimamisha mauzo ya bidhaa hizo kwa siku mbili au tatu bila ya kutoa taarifa yeyote kwa wananchi. Aidha wafanyabiashara hao hupandisha bei kiholela bila ya taarifa.

(a) Kwa nini wafanyabiashara hao wamepewa uhuru mpana wa kuwanyanyasa wananchi.

(b) Hadi mwezi Mei 2011, bei ya mafuta ya taa ni 1700/= kwa lita moja, Je, Mhe. Waziri huoni kuwa inawaumiza wananchi wa kipato cha chini ambao ndio wanatumia zaidi bidhaa hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 190 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wafanyabiashara wa vituo vidogo vidogo vya mafuta hawapewi uhuru mpana wa kuwanyanyasa wananchi isipokuwa makampuni yanayowauzia mafuta yanapunguza uuzaji wa mafuta, baadhi ya vituo vinakuwa na mafuta na vyengine hukosa kabisa.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyojibu swali Nam. 131 katika Baraza lako tukufu kuwa upandaji wa bei za mafuta vituoni unategemea sana upandaji wa bei za mafuta duniani. Serikali ingependa sana bei za mafuta kuwa chini lakini upandaji wa mafuta duniani uko nje ya uwezo wa Serikali.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando):** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kumekuwa na uuzaji holela wa mafuta yaani vituo vidogo vidogo vya mikononi ambavyo vinasababisha wakati mwengine kuweza kutokezea hata madhara ya moto.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wauzaji wa aina hii wanatoweka kabisa katika nchi yetu ili kuweza kuweka usalama.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwanza nakubaliana nae kwamba wapo wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanafanya biashara kinyume na taratibu. Lakini serikali kwa kuliona hili tutawaita wafanyabiashara hao na kuwapa taratibu zinazofaa ili tuondoshe janga hili la moto ambalo linajitokeza mara kwa mara.

**Nam. 191**

**Ukarabati na Umiliki wa Nyumba za Maendeleo**

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla** - Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilijenga nyumba kubwa za maendeleo mijini na vijijini Unguja na Pemba. Nyumba hizo hapo awali zilimilikiwa na SMZ, lakini hivi sasa baadhi ya nyumba hizo zinamilikiwa na watu binafsi na pia ziko katika hali mbaya na ya hatari kwa wakaazi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati.

(b) Kwa kuwa baadhi ya nyumba hizo wenyewe ni watu binafsi Serikali itawashirikisha vipi ili kile kitakachofanyika kiwe cha aina moja.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati** - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 191 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

*(a)* Mhe. Spika, kwa kawaida Serikali huwa inazifanyia matengenezo nyumba hizo lakini pia tunakiri kuwa ni kwa kiwango kidogo, kwani fedha zinazotengwa huwa zinawezesha kufanya matengenezo madogo madogo kama vile kutengeneza makaro yanapoharibika na pia kubadilisha mabomba ya maji machafu. Serikali kwa kulitambua tatizo la matengenezo ya nyumba za maendeleo ndio maana mwaka jana Serikali ilileta Mswada wa Sheria *(Condominium)* mswada ambao ulipata ridhaa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi.

*(b)* Mhe. Spika, kuhusu nyumba za watu binafsi wenye fleti katika nyumba za maendeleo hao watashirikishwa nao watakuwa wanawajibika kuchangia matengenezo kwa mujibu wa Sheria ya *Condominium.*

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba kuna sheria iliyopitishwa ya *Condominium* kwa ajili ya kuwafanya wanaoishi katika nyumba za maendeleo waweze kuchangia. Lakini katika swali la msingi alilouliza Mhe. Viwe Khamis Abdalla ni kwamba kuna

nyumba ambazo ni mbovu sana na hazikaliki na nyumba hizo bado hawajauziwa wananchi na zinaweza zikaleta maafa.

Kwa mfano, nyumba zilizoko Kengeja ni mbovu kupita kiasi, wakati wizara hii imeshafanya utafiti kuona kama zile nyumba kweli ni mbovu na wananchi bado wamo wanaishi.

(a) Je, ni lini hasa nyumba zile zitafanyiwa matengenezo.
(b) Je, Wizara itafanya jitihada gani ya kuwahami wale watu waliomo ili serikali isije ikapata maafa ya msiba wa kitaifa kwa nchi nzima.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwanza nakubaliana nae kwamba nyumba zilizopo Kengeja kweli ni mbovu sana na baadhi ya maeneo mengine. Lakini Wizara yangu kupitia Idara ya Majenzi tutazishughulikia nyumba hizo kwa kadri ya vile ambavyo tutakavyopata fedha kwa sababu tatizo hili si wananchi tu lakini hata sisi linatuathiri.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Asha Bakari Makame (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari):** Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa dhati kwa kunipatia nafasi hii leo asubuhi ya kutoa hotuba ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu ambaye ametujaalia uzima na afya njema ya kuwezesha kukutana leo hapa ndani ya Baraza lako tukufu kwa minaajili ya kujadili Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, kimsingi kamati yetu imekuwa ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa yanayoleta tija na ufanisi wa hali ya juu. Nachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa kuijadili Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa umakini na umahiri wa hali ya juu.

Naomba niwatambulishe kwa majina Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:

1. Mhe. Asha Bakari Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Mohammed Said Mohamed - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Assaa Othman Hamad - Mjumbe
4. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
5. Mhe. Abdi Mosi Kombo - Mjumbe
6. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
7. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe
8. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
9. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mapato ya Wizara kupitia Mradi wa Ukodishaji wa Vipaza Sauti yamepungua kidogo na kufikia milioni 2 kutokana na kuwepo kwa ukodishaji binafsi wa vipaza sauti hivyo. Aidha, kodi ya minara nayo pia imepungua kutoka milioni 35 kwa mwaka 2010/2011 hadi kufikia milioni 20 kwa mwaka huu wa fedha kutokana na ujenzi wa minara binafsi kwa makampuni ya mawasiliano. Hivyo, Kamati inashauri Wizara kubuni miradi mbadala itakayoingiza fedha na kuchangia vyema kwenye pato la taifa.

Mhe. Spika, Kamati yetu imebaini mapungufu makubwa kwenye kifungu na malipo ya huduma za studio. Afisi Kuu Pemba kutokana na hali mbaya ya studio zetu hasa zile za Pemba hatukutegemea kutengewa fedha kabisa kama inavyoonekana kwenye kasma 220111. Hivyo, tunaiomba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kurekebisha kasoro hiyo.

Mhe. Spika, Afisi ya Idara ya Habari Maelezo imetengewa jumla ya shilingi milioni 5 kwa ajili ya matengenezo makubwa ya kiwango ambacho Kamati

yetu kwa kauli moja imekisema kuwa ni kidogo. Pamoja na maelezo ya Maafisa wa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba matengenezo makubwa ya ofisi ya Serikali hii jukumu lao kama Kamati inashauri kugawanywa kabisa fedha hizo kwenye bajeti kwa mujibu wa mahitaji ya matengenezo yaliyoainishwa na kila Wizara, ili yaweze kutengeneza ofisi zao wenyewe kwa nia ya kupunguza msongamano na majukumu huko Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, idara hii imebeba majukumu makubwa katika nchi yetu ikiwemo kusimamia mikutano ya vyombo vya habari, kuratibu mikutano ya kitaifa na kimataifa ya serikali, kutoa ufafanuzi wa taarifa zilizopotoshwa, kusambaza habari katika vyombo vyote vya habari ndani na nje, kuhifadhi nyaraka mbali mbali za serikali, Gazeti rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuhifadhi picha za viongozi na za matukio mbali mbali ya jamii. Magazeti na majarida.

Kwa msingi huo basi, jumla ya kifungu cha idara hii ambayo ni shilingi milioni 2,200,000 ni ndogo mno. Pamoja na kufanyiwa matengenezo ya jengo la idara hiyo bado idara inaonekana ina matatizo makubwa ambayo ni aibu kwa taifa letu. Idara inakabiliwa na upungufu mkubwa wa vifaa hivyo vilivyopo, pia ni vya zamani na chakavu mno hasa vifaa vya ufundi wa vipaza sauti. Jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa idara hii ina kipaza sauti kimoja tu ambacho baadhi ya siku viongozi wakuu wa Kitaifa hufanya shughuli muhimu za serikali katika sehemu tofauti na wakati mmoja. Hivyo, hukosa huduma muhimu kupitia idara hiyo kutokana na upungufu huo mkubwa wa vifaa.

Aidha, uhifadhi wa nyaraka mbali mbali muhimu za serikali hauridhishi kabisa kwani maktaba ya idara hii haiko katika mazingira ya kimaktaba, ni chakavu mno na haina hata computa. Hivyo, ni wajibu wa serikali kuyatambua matatizo yanayoikabili idara hii muhimu ambayo ndio mdomo wa serikali yetu na kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa idara hii inapatiwa fedha za kutosha ili taifa letu liondokane na aibu hii kubwa. Aidha, Wizara itilie mkazo juu ya uimarishaji wa uwekaji kumbukumbu kwa kutumia kompyuta.

Kamati pia inaishauri wizara kufikiria uwezekano wa eneo la kuegesha gari katika idara hiyo kujengwa ukumbi wa mikutano ambao utaweza kutumika kama chanzo cha kuongezea mapato ya serikali kupitia idara hiyo.

Mhe. Spika, kituo cha kimataifa cha *Aecrotenal* ambacho kwa muda mrefu kilikuwa kikifanya kazi mbalimbali za utafiti wa lugha za kigeni sasa kimekufa. Licha ya hatua kadhaa ambazo serikali imekuwa ikizichukuwa kukifufua, bado kituo hiki hakifanyi kazi zilizokusudiwa. Nchi wanachama wa kituo hiki wamesita kutoa michango yao na hivyo michango ya kituo hiki imebaki kutolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar na ile ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Kutokana na hali hiyo, Kamati imeiagiza wizara ifuatilie kwa

makini hatua za kukifufua kituo hiki na kisha kuleta taarifa rasmi kwa Kamati hii kwa hatua zaidi**.**

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza wizara kwa kuona haja ya kuifanyia marekebisho sera ya Habari, Utangazaji, Michezo na Utalii. Ni jambo la busara na hekima kubwa kwa kufanya marekebisho hayo kwani sera hizo zimepitwa na wakati.

Mhe. Spika, napenda kuishukuru wizara kupitia Tume ya Utangazaji kwa kufanikiwa kupata uanachama ya Jumuiya ya Mawasiliano ya Afrika Mashariki (*East African Communication Organization*) bila ya kutumia mgongo wa Tanzania Bara mnamo mwezi April, 2011. Kadhalika, mwongozo wa pamoja wa matumizi ya vifaa vya dijitali kwa nchi zote za Afrika Mashariki umeandaliwa.

Mhe. Spika, kamati ina wasiwasi na kasma iliyotengwa kwa ajili ya ununuzi wa mashine na zana katika Idara ya Televisheni kwani inaonekana kuwa ni ndogo mno. Fedha hizo 1,000,000/- ni chache sana, ikilinganishwa na gharama halisi za ununuzi wa vyombo hivyo vya usafiri na inawezekana chombo kimoja tu kikanunuliwa kwa mwaka huu. Kwa mantiki hiyo basi, Kamati inashauri kuongezwa kwa kasma hii kwenye bajeti ya mwaka ujao.

Mhe. Spika, kutokana na hali mbaya ya kituo cha televisheni Zanzibar hususan kwa upande wa Pemba, Kamati imefarajika sana kuarifiwa kwamba mitambo mikubwa miwili ya transmita ya Digitali ya kurushia matangazo ya televisheni imenunuliwa na tayari imeshawasili Zanzibar. Ni jambo la kusikitisha sana kwamba ununuzi wa vifaa hivyo muhimu kwa taifa umefanywa bila ya kuishirikisha kikamilifu wizara, matokeo yake mitambo hiyo yenye thamani ya mamilioni ya shilingi kukwama Uwanja wa Ndege kwa kisingizio eti mnunuzi hana fedha za kuilipia ushuru. Hata hivyo, Kamati yetu inalenga kuifuatilia kwa makini taarifa iliyotolewa ndani ya Baraza lako tukufu kwamba mitambo hiyo tayari imeshaondolewa uwanja wa ndege na ile ya Pemba tayari imeshawasilishwa na hatua iliyobakia ni ufungwaji tu.

Mhe. Spika, Kamati yetu inatoa pongezi maalum kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, utalii na Michezo Pemba kwa kulifanyia matengenezo makubwa jengo la makao makuu yake pamoja na kununua samani zinazohitajika, jambo ambalo limepelekea kutohitajika fedha kwenye kasma (220603) ya ununuzi wa samani kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Kwa sasa, Kamati imearifiwa kwamba hali ya wizara ni nzuri na inawaruhusu watendaji wa Wizara hii kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mhe. Spika, tunaipongeza sana wizara kwa kushiriki katika maonesho tisa ya utalii ya ndani na nje. Kimsingi, maonesho hayo yametoa fursa ya kuitangaza Zanzibar kuitalii. Aidha, chuo cha maendeleo ya utalii Zanzibar kimepata usajili rasmi wa *NACTE*, lakini cha kusikitisha ni kwamba usajili huo ni wa miaka miwili tu. Kutokana na changamoto kubwa ya uhaba wa majengo, vifaa vya kufundishia, walimu wenye sifa zinazostahiki na maktaba inayokikabili chuo hicho, kasma iliyotengwa ya shilingi 200,000,000/= kwa ajilii ya gharama za uendeshaji haitoshi, hivyo tunaiomba serikali kukitengea fedha zaidi chuo hichi ili kuinua hali ya chuo ambacho ni kichocheo kizuri kwa ajira za vijana wetu.

Mhe. Spika, kamati yetu ina kila sababu ya kumpongeza Mkurugenzi wa chuo cha maendeleo ya utalii kilichopo Maruhubu kwa jinsi anavyosimamia vyema majukumu yake. Hii inadhihirisha wazi kuwa "Wanawake wanaweza wenyewe hata kama hawakuwezeshwa", kwani pamoja na mazingira magumu yanayomkabili, anaendelea vyema na majukumu yake katika kulitumikia taifa lake. Aidha, Kamati inaiomba Wizara kulifuatilia kwa kina suala la uvamizi wa eneo la ufukwe wa chuo hicho linaloendelea kufanywa na muekezaji alie jirani na chuo kwani pamoja na jitihada za Mkurugenzi huyo, jukumu hilo ni zito na liko nje ya uwezo wake.

Mhe. Spika, Kamati inatoa shukurani za dhati kwa Wizara kupitia Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) kwa kufanikiwa kuchapisha kamusi la Kiswahili sanifu. Kazi inayoendelea ni kulitangaza na kuliuza kwa watumiaji mbali mbali. Kamati inaunga mkono kampeni ya uuzaji wa Kamusi hili na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kuendelea kujinunulia Kamusi hili ili kuikuza lugha yetu ya taifa.

Mhe. Spika, tunaipongeza sana Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa timu yake ya netiboli ya wanawake kunyakua kombe la *NSSF*, jambo ambalo limeleta faraja kubwa kwa taifa, wizara, na wananchi wote kwa ujumla.

Mhe. Spika, pamoja na ushindi huo uliopatikana, Serikali kupitia Wizara hii haina budi kufanya uchunguzi na utafiti wa kina ili kujua sababu za msingi zilizopelekea kushuka kwa hadhi ya michezo hapa Zanzíbar. Hii inatokana na kushindwa kwa timu za Zanzíbar katika mashindano mbali mbali na kupungua kwa kiasi kikubwa kwa ari, mwamko na upenzi wa michezo kwa wanamichezo na wapenda michezo wengi hapa nchini. Aidha, wizara inapaswa kuandaa utaratibu maalum wa kuvichunguza vyama vya michezo ili kuwabaini na kuwachukulia hatua watendaji wanaoonekana kudhoofisha maendeleo ya michezo hapa nchini. Mkazo maalum uwekwe katika kurudisha heshima ya Zanzíbar katika michezo.

Mhe. Spika, imebainika kuwa viwanja vingi vilivyotengwa kwa ajili ya michezo vimeonekana kuvamiwa kwa shughuli mbali mbali. Hivyo, Wizara inayohusika inapaswa kushirikiana na serikali za Wilaya na Mikoa kuvitambua, kuviorodhesha na kisha kuvisajili viwanja vyote vya michezo vilivyopo ili kuepusha uvamizi zaidi unaoweza kufanywa dhidi ya viwanja hivyo vya michezo.

Mhe. Spika, hatua za Zanzíbar za kujiunga katika uwanachama wa Shirikisho la Soka Duniani(FIFA) zinaonekana kuzorota. Hivyo Kamati inaiomba Wizara itafute njia zaidi za kukisaidia Chama cha Soka,Zanzíbar (*ZFA*) ili Zanzíbar iweze kupata uwanachama huo ambao ni haki yake,

Mhe. Spika, kamati inatoa pongezi kwa Wizara kwa jitihada mbali mbali inazochukua katika kuimarisha Chuo cha Uandishi wa habari Zanzibar zikiwemo zile za kukitafutia chuo hicho usajili kutoka Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (*NACTE*), uanzishwaji darasa la Kichina pamoja na utayarishaji wa michoro ya jengo jipya la chuo hicho linalotarajiwa kujengwa huko Tunguu.

Kwa upande wa jengo linalotumiwa na chuo hicho hivi sasa, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha taratibu za kulifanya jengo hilo kuwa ni milki ya Wizara. Kamati pia imeishauri Wizara kufuatilia kwa karibu suala la *NGO* iliyomo ndani ya jengo la chuo hicho. Ili kukipandisha hadhi chuo hicho, Wizara inashauriwa kufikiria haja ya kukifanya chuo hicho kuwa sehemu ya Chuo cha Taifa cha Zanzíbar (*SUZA*).

Mhe. Spika, wananchi wanaomiliki maeneo ya utalii wamebainika kutonufaika na matunda ya utalii katika nchi yao. Kwa vile wengi wao huwa hawana uwezo wa kuanzisha miradi kama ya hoteli za kitalii, hivyo huingia katika mikataba ya ushirikiano na wawekezaji kutoka nje kwa ajili ya kujenga na kuendesha hoteli. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa mikataba hiyo inaonekana kuwanufaisha zaidi wawekezaji kutoka nje, ambao hupata mgao mkubwa unaotokana na mapato ya hoteli husika na wazalendo huambulia asilimia ndogo tu ya mapato hayo.

Aidha, mfumo wa watalii kulipia gharama zote huko huko nchi za nje wanakotoka (*package tourism*) unaonekana kuwa na matatizo sana. Mfumo huu huzifanya hoteli za hapa nchini ambako ndiko watalii wanapofikia kukosa fedha za kuendeshea hoteli hizo mpaka fedha hizo ziletwe kutoka huko nje zilikolipwa ambapo huwa zinachelewa sana kufika nchini. Hali hii huwafanya wazalendo wanaoendesha hoteli hizo kushindwa hata kuwalipa wafanyakazi mishahara yao na maslahi mengine kwa wakati. Pia waendeshaji hao wa hoteli

hushindwa kulipa madeni makubwa wanayodaiwa na wachuuzi na wafanyabiashara wanaopeleka bidhaa mbali mbali katika hoteli hizo.

Vile vile hoteli zenye mfumo huu zinaonekana kukosa kumbukumbu sahihi za mapato yanayotokana na watalii kwa vile kumbukumbu hizo hubaki huko nchi za nje kunakofanywa malipo hayo. Kutokana na hayo, Kamati inaishauri Wizara kujipanga upya ili kutoa elimu ya kutosha kwa wazalendo wenye maeneo ya Utalii juu ya sheria na umuhimu wa ardhi pamoja na njia bora zaidi ya kutumia pindi wanapohitaji kuingia mikataba na wawekezaji wa nje. Aidha, elimu pia inapaswa kutolewa kwa waendeshaji hoteli wazalendo juu ya mfumo bora zaidi wa kuendesha hoteli ukiwemo ule wa upokeaji wa watalii na ulipaji wa moja kwa moja wa gharama za watalii hao.

Pamoja na hali hiyo, Kamati imebaini kuwa wizara haina taarifa za kutosha juu ya matatizo mengi yanayojitokeza katika sekta ya utalii hasa katika maeneo ya vijijini. Hivyo kuna haja kubwa kwa wizara sasa kubadilika kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika na masuala ya uwekezaji na utalii kuandaa utaratibu maalum utakaoiwezesha wizara hii kushirikishwa katika kila pahali penye miradi ya utalii. Kwa mnasaba huu Kamati imeiagiza Wizara kuandaa kwanza mkutano kati yake na Kamati hii pamoja na taasisi zinazohusika na mikataba na Utalii zikiwemo Kamisheni ya Utalii, Mamlaka ya Vitega Uchumi (*ZIPA*), Bodi ya Mapato (*ZRB*) na Ofisi ya Mwanashria Mkuu ili kujadili matatizo mbali mbali ya sekta hii na kutafuta njia muafaka za kuyapatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Utalii ni moja kati ya taasisi muhmu inayotegemewa na serikali katika kuitangaza Zanzíbar kiutalii na pia kukusanaya mapato yatokanayo na Utalii. Kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012 Kamisheni hii inatarajia kukusanya jumla ya Tsh. 842,000,000 /- kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Pamoja na majukumu makubwa iliyonayo, baadhi ya ofisi za kamisheni hii hasa ile iliyopo bandarini hailingani kabisa na hadhi na umuhimu wake kwa taifa. Ofisi hiyo ina majukumu mbalimbali yakiwemo kuwapokea na kuwapa taarifa za Zanzíbar wageni pamoja na kuweka kumbukumbu za watalii wanaoingia nchini kupitia bandarini. Licha ya umuhimu huo ofisi hii inaonekana imekosa nafasi nzuri ya kuendesha shughuli zake hapo bandarini na hivyo shughuli zote huendeshwa kibandani, hali ambayo haitoi taswira nzuri kwa wageni wetu. Hivyo Kamati inaiomba wizara kushirikiana na Wizara ya Muindombinu na Mawasiliano kupitia Shirika la Bandari kutafuta sehemu muafaka kwa ajili ya ofisi hiyo muhimu ya Kamisheni ya Utalii hapo bandarini.

Aidha Kamati inaiagiza wizara kufuatilia kwa karibú maombi ya Kamisheni hiyo ya kurejeshewa mapato yake ya fedha inazozikusanya (*Retention*) ili

kuondoa usumbufu wa upatikaniji wa fedha ambao huzorotesha utekelezaji wa majukumu ya Kamisheni hiyo.

Kamati pia kwa upande wake inaiomba Serikali kuiruhusu Kamisheni ya Utalii kuwa na akaunti yake yenyewe, badala ya kutegemea kasma inayotoka Wizara ya Fedha, ambayo husababisha usumbufu mkubwa wanapohitaji kufanya matumizi.

Mhe. Spika, kamati inaiomba serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ifuatilie kwa kina suala la kupatikana kwa utambulisho wa kisheria (*legal status*) kwa Hoteli ya Bwawani kwani kukosekana kwa utambulisho huo kunaikosesha fursa za kukua na kujiendeleza zaidi.

Kamati pia imeiagiza Wizara kutafuta kumbukumbu ili kulifahamu vizuri eneo halisi linalomilikiwa na hoteli ya bwawani pamoja na mipaka yake ili kuzuia uvamizi wa eneo hilo.

Vile vile, Kamati imeelezwa kuwepo kwa wadaiwa sugu watano kati ya watu waliokodshwa ofisi za chini za hoteli hiyo, ambapo tayari mikataba ya wadaiwa sugu hao imeashpelekwa Wizarani. Hivyo, tunaiagiza Wizara kuhakikisha kuwa wadaiwa sugu hao wanalipa madeni yao, vyenginevyo iichukue hatua kali za kisheria dhidi yao haraka iwezekanvyo, kwani wanaikosesha hoteli hiyo fedha nyingi.

Mhe. Spika, Baada ya maoni hayo ya kamati, niwaombe Wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu, wakubali na kuidhinisha makadirio ya mapato ya shilingi za Kitanzania 1,202,800,000/= fedha zinazoingia kwenye mfuko mkuu wa serikali. Shilingi 1,709,440,000/= ambazo Wizara inatarajia kuzitumia katika shughuli za uendeshaji baada ya kuzikusanya. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya shilingi 6,457,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 560,000,000/= kwa kazi za maendeleo kwa ajili ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Vile vile, Kamati inaipongeza wizara kwa kupata msaada wa Tsh. 2,400,000,000/= kwa ajili ya mradi wa matangazo ya masafa mafupi huko Dole kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, kwa heshima na taathima naunga mkono hoja, na kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi asubuhi hii kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari na Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha na kutupa pumzi ili kuweza kufika hapa katika Baraza lako tukufu. Vile vile nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kumchagua kijana wetu waziri wetu, kwa kweli amejitahidi katika kipindi kifupi sana, kwa hivyo Mhe. Rais hakukosea hata kidogo.

Pia Mhe. Spika, niwapongeze watendaji wake akiwemo waziri mwenyewe, katibu na wakurugenzi wake wote. Ndio maana hata ikafikia pahala na kuonesha hata hotuba yake ikawa nzuri zaidi kutokana na mashirikiano ya hao watendaji wote.

Mhe. Spika, sitaki kupoteza muda, naomba niingie kwenye ukurasa huu wa 16 katika sekta ya habari pamoja na ukurasa wa 17 kuhusu Shirika la Utangazaji. Kwa kweli Mhe. Spika, ndio maana zile sifa hasa za waziri zinapojionesha katika ukurasa huu. Mhe. Waziri kwa kweli amejitahidi sana na ndio maana sasa hivi ikawa Baraza lako tukufu linapendwa sana kutokana na kitendo ambacho amekifanya kijana kwa muda mfupi sana. Pamoja na hayo Mhe. Spika, zuri na baya linakuwepo, sasa ubaya wake uko wapi Mhe. Spika.

Sasa tukiingia kwenye Baraza kama hukuonekana nyumbani ugomvi huo ndio ubaya wake. Mimi naulizwa mbona mheshimiwa sijakuona, sasa nabakia la kusema silijui. Sasa hii kuonesha kuwa sasa Baraza lako linaonekana Zanzibar nzima. Lakini sio hivyo tu, mheshimiwa ana lengo kubwa la kutaka kuitangaza zaidi, wakati wa kipindi hiki cha Baraza lako tukufu amekusudia sio lazima hapa Zanzibar hata Bara ni lengo lake hilo. Ndio maana akasema kuwa ataleta zana za kisasa ili liweze kuonesha hiyo hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, naomba rasmi nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada zake hizo. Mhe. Waziri hongera sana pamoja na watendaji wako. Vile vile katika kitabu chake nimejaribu sana kutafuta baadhi ya mambo hivi. Hasa juzi tulikuwa na tamasha lile la Oman, lakini sasa niseme hiki kitabu kimechapishwa mapema na tamasha limekuja nyuma. Lakini pamoja na hilo, lile tamasha kwa kweli ni zuri sana na Mhe. Waziri bado anaendelea kupata sifa kutokana na tamasha lile. Tamasha lile Mhe. Spika, tumejifunza mambo mengi.

Mhe. Spika, moja kubwa ambalo mimi nimeliona pale kuwa wenzetu bado wanathamini utamaduni wao. Sasa na sisi tumeletewa kama ni somo la kusoma ili na sisi utamaduni wetu tuushike na tuweze kuuendeleza. Ndio maana mheshimiwa kavutiwa zaidi kuleta tamasha lile ili Wazanzibari wajuwe sasa

utamaduni wetu unapotea. Kwa hivyo, mimi ningeomba serikali kuu ikamuwezesha Mhe. Waziri wetu kwa kumpatia fungu ili na yeye akienda kule Oman, katika hao wawakilishi kama kumi basi mmoja niwepo mimi katika safari hiyo.

Mhe. Spika, nikiendelea kuchangia nija katika ukurasa wa 25 sehemu ya magazeti. Kwa kweli Mhe. Spika, magazeti yetu ni mazuri sana, kwa maneno ya vijana yana vina vizuri sana, yana uhakiki mzuri na wala hayapotoshi. Mhe. Spika, niseme wizara yake yote inastahili sifa kutokana na kuwa magazeti yetu bado hayajapata changamoto ya kulaumiwa kutoa habari zilizokuwa hazina uhakika. Mhe. Waziri anajitahidi katika hilo ili asipotoshe umma, kwa sababu magazeti ni moja katika njia ya watu kupata taarifa.

Mhe. Spika, siku moja Dk. Shein alisema tutumie vyombo vya habari, tujitangazie zile *activity* zetu waheshimiwa tunazozifanya katika majimbo. Lakini yeye hii shughuli tayari anatusaidia vizuri sana katika magazeti haya. Mhe. Spika, kidogo niseme hapa kwamba huko nyuma wale wafanyakazi wa Zanzibar Leo, waliifanya kazi ile kwa ushujaa kabisa, gazeti hili likawa zuri wakalipamba, lakini hatimaye hawajalipwa mpaka leo. Mhe. Waziri hebu hili suala lifuatilie hawa watu wanapata tabu sana. Lakini nimeambiwa hiki kiwanda kiko kwa Mhe. Makamo wa Pili mwenyewe.

Kwa hivyo, hapa mimi sisemi kitu kwa sababu ndio liko kwa mwenyewe baba Makamo wa Pili. Lakini yeye anajua nini madhara ya wafanyakazi na hitilafu yake. Wanaathirika sasa hivi hawapati maziwa yale kwa mujibu ya sheria, maposho yale hawapati kwa wakati, wanajitahidi kuchapisha magazeti mazuri sana na vitabu vyetu ambavyo tunaviona sasa hivi hapa. Lakini maposho yao ni pungufu, hata yale maziwa. Kwa sababu mule kunatumika *chemical*, ukifanya uchunguzi wa mule basi baada ya miaka miwili au mitatu wale vijana pale wataathirika na kupata *cancer*. Kwa hivyo, suala hili ningeomba kwa makusudi kabisa kwamba Mhe. Waziri wafuatilie hawa watu lile posho lao wakati ule ilivyokuwa haijaondoshwa hii na mpaka leo hii hawajalipwa.

Mhe. Spika, nikiendelea nija kwenye ukurasa wa 35. Katika ukurasa huu kuna kilio kikubwa sana kwa Wazanzibari. Mhe. Spika, siwezi kusema kwamba tunashindwa na sekta hii ya utalii, lakini nitathubutu kusema hivyo kwa sababu tu serikali imeleta utalii kwa malengo makuu mawili.

Kwanza kujiinua uchumi na pili kuwaondolea umaskini wananchi wao. Pamoja na kuwa huko nyuma hatukujitayarisha, kwa sababu tumeleta hiki kitu lakini hatukujitayarisha. Lakini *speed* ya serikali imejitayarisha na imeweka chuo, sasa Wazanzibari wengi ambao wana sifa za kwenda kufanyakazi mahotelini.

Kinachojitokeza Mhe. Spika, kwa bahati mbaya jana mimi sikuwepo, lakini nilikuwa naitaka sana ile wizara ya Mhe. Waziri wetu Haroun, mimi ningekuwa mkali sana na mimi ningesema ile ina mapungufu irejeshwe. Mhe. Makamo wa Pili angepata kazi ya kusema kuwa na wao angewapa muda wa wiki mbili au tatu kama wenzetu kule bungeni. Kwa sababu Mhe. Spika, bado tunafanya mzaha katika sheria, wanafanyaswa wafanyakazi wetu na ndugu zetu, nikisema Wazanzibari pamoja na Watanzania Bara.

Mhe. Spika, kuna ma-PO ambao ni Wakenya, unafikiri wewe unategemea nini wale kumsaidia Mtanzania au kumsaidia Mzanzibari. Wanafanya wanavyotaka wao wenyewe Mhe. Spika. Kwa hivyo, dhana ya uzuri inakuja na ubaya ndani yake. Leo kabla sijaja sijui walijuaje watu kama nitachangia, maana masimu kibao Mhe. Spika, unyanyasaji umekuwa mkubwa sana. Mhe. Waziri mwenyewe ni shahidi. Kitu ninachompenda Mhe. Spika, siku moja mimi hapa nilitoa hoja, Mhe. Waziri alikwenda mbio kule akafanya utafiti kule na akamletea Mhe. Makamo wa Pili, akamwambia hii ni kweli Mhe. Mshimba kasema kitu cha ukweli na alianzia katika Hoteli ya *Blue Bay*. Mhe. Spika, yeye yuko kule mimi napigiwa siku napewa hongera mimi. Nikawaambia mpeni hongera Mhe. Waziri kwa sababu kakubali ukweli ulivyo. Kwa kweli hili suala linasikitisha ambapo bado serikali yetu inafanya mzaha.

Mhe. Spika, ingekuwa kama sio swahiba wangu huyu Mhe. Waziri basi ningesema hii leo nitaipigia buti sana tena ningekuwa mkali, lakini kwa kuwa ni mwanagenzi na juu ya uwanagenzi wake ametuonesha mambo ambayo anakoelekea ni kuzuri zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba sekta hii tunaifanyia mzaha na hatujawa tayari kuisaidia.

Mhe. Spika, mimi ningependa sheria ile angepewa yeye kuliko kuachiwa ile sheria wakakaa nayo watu wa *labor* mpaka leo wanaichezea tu. Angepewa mwenyewe basi angekuwa *active* kweli kweli, kwa sababu ana watu wazuri, ana katibu wake yuko *serious* sana, katibu wake ni *hard work* sana. Kwa mfano katizame tamasha alilolifanya juzi Nungwi kule, limeleta mfano mzuri sana tena limefana kabisa, sasa tena kitu gani kama sio mtu hodari, angekuwa sio hodari angelifanya lile. Kwa hivyo, na hii sheria kama tungempa mwenyewe huyu, basi ingekuwa sasa hivi tayari kule kunawaka moto kwenye mahoteli.

Vile vile Mhe. Spika, vijana wetu wanataka kupewa elimu na elimu yenyewe inahusia na na mikataba ya kuungiana na wale watu wa mahoteli. Nikatoa mfano na mpaka leo hii. Namtaka Mhe. Makamo anisaidie aliunda tume ya kuifuatilia hoteli ya Venta, lakini mpaka leo hakuna ripoti ambayo inaonesha kwamba Venta sasa hivi imeshapata mwekezaji mwengine au Venta sasa hivi tayari imeshakuwa na pesa za kuwalipa wale wananchi wetu. Mhe. Makamo wa Pili inasikitisha sana watu wako mahakamani vijana wetu, sasa hivi

wanashtakiwa kwa kosa la kuwa hawana fedha zile za kuwalipa wale ma *supply* wao waliokuwa wakichukua vile vitu. Mhe. Makamo tafuta sheria ili uuze ile hoteli na tuweze kuwalipa wale wananchi, kwa sababu tayari athari kubwa. Ramadhan hiyo hapo watu wanakwenda mahakamani. Mhe. Spika, tutawapa tafsiri mbaya sana hawa vijana wetu, sasa hivi tayari tafsiri ipo, hili tulikubali kwamba tafsiri sasa hivi tayari ipo ya hiki kitu kizuri ambacho tumekitengeneza na hivi sasa kina tafsiri yake kuwa ni kibaya.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Makamu wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, angaalu wale wananchi wetu waliowekeza kule Hoteli ya Venta wajue lini watapata mafao yao au lini hoteli ile itafanyakazi. Mhe. Spika, nadhani si vibaya ikiwa hatuna budi basi tuwape wao hoteli ile kwa ajili ya kuiendesha na kuweza kujilipa fedha zao na wala hakuna zaidi.

Kwa kweli nafikiri ni vizuri wajikusanye na baadaye tuwape wao na benki Mhe. Waziri atawasimamia kwa ajili ya kwenda kuchukua fedha za mkopo na waendeshe wao na itakuwa tayari *refunding* kwa upande wao.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri sekta hii ni ngumu sana, kwa sababu tunapata mapato makubwa sana, lakini bado tunaichezea na hali hii inasikitisha sana.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niingie kwenye ukurasa wa 45 kuhusu Hoteli ya Bwawani. Mhe. Spika, alizungumza hapa Mhe. Asha Bakari Makame (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari) kuna wateja sugu. Nadhani tusiwafiche hata kama mimi kiongozi silipe basi nitolewe hadharani na hilo ni kosa, kwa nini tunaficha, haiwezekani ile ni ofisi na watu wanahitaji kupata mapato na wizara iweze kujiendesha, kwa sababu fungu kuu lenyewe hawapati asilimia inayotawika, mimi naona hawa tunawachelewesha.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anitajie hao wateja sugu ambao hawataki ni nani hao na kama hukunitajia nakuzuia kifungu chako.

Vile vile nimefurahi sana baada ya kuona asilimia 80 ya watoto wetu pale tayari wameshaajiriwa. Kwa kweli hilo nalo lazima nikupe hongera, kwa sababu panapo suala zuri basi lazima nitakusifu, kwa sababu vijana wale tumewatumia muda mrefu. Kwa mfano, nilipokuwa kwenye Kamati ya Fedha nilisema sana kuhusu suala hili.

Lakini mara hii *Alhamdulilla* wenzetu inavyoonesha *speed* yao inakwenda vizuri na wamebana vizuri na Mhe. Waziri amekubali, kwa sababu Mhe. Waziri mwenyewe kijana na amepitia sekta hizo, basi tayari amewaajiri wale

vijana. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na wizara yake kwa jumla, kwani suala hili ni zuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna watu wa *Rock Cafe* tunaomba mikataba yao tuione na kama ina mapungufu basi tuweze kuwasaidia na wala tusione haya, kwa sababu wengine wanakodishwa kwa bei ndogo sana. Kwa kweli inafika pahala tunakosa mapato Mhe. Spika.

Kwa maana hiyo, masuala haya ya kukodisha mara nyingi sana ni vyema tukatoa *tender*, yaani tukimbilie kunako *tender* tutapata angalau kiwango kizuri cha fedha ambacho kitakachoweza kutuwezesha vizuri, lakini kama tutakuwa tunaweka kinyemela, basi tutashindwa kuendesha. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba hao wateja sugu watuletee.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 56 kuhusu Lugha ya Kiswahili. Mhe. Spika, juzi tuliuziwa Kamusi moja ambao ni zuri sana tena ninalo hapa kwa bei ya shilingi 10,000/=. Kwa kweli lina lugha nzuri, fasaha inayoeleza kwamba Wazanzibar tunatumia lugha hii.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri akutane na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali walitie kwenye elimu kama hakuna kule, yaani iwe ni *special subject* hii, kwa sababu hivi sasa vijana wetu wanapotosha Lugha ya Kiswahili lahaja yake hakuna sasa.

Kwa maana hiyo, kamusi hii isiwe kama ni biashara tumeletewa tununue Waheshimiwa tu, hata Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wao tunawaomba watengeneze *special subject* ya kuwasomesha hawa vijana wetu, ili lugha isipotee ya Kizanzibari, yaani Lahaja ya Kizanzibari isipotee Mhe. Spika, kwa sababu tunaletewa mambo ya ajabu na wala hayastahiki Wazanzibari kuweza kutamka matamshi yale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa niingie kwenye ukurasa wa 67 kuhusu mambo ya Michezo. Kwa kweli suala la zoezi la riadha linanisikitisha sana tunaelezwa hapa kwenye ukusara wa 67 kifungu cha 3, naomba kunukuu Mhe. Spika.

Ukurasa wa 67 kifungu cha 3 kinasema hivi:-

> “Baraza la Taifa la Michezo limemudu kusimamia marekebisho ya Katiba za vyama vifuatavyo:-…”

Lakini kwenye ukurasa wa 68 na pia unaeleza, naomba kunukuu Mhe. Spika.

Ukurasa wa 68 unasema hivi:-

> "… Chama cha Riadha (*ZAAA*) na Chama cha Mpira wa Kikapu (*BAZA*) wametakiwa kukamilisha marekebisho ya katiba zao kabla ya kufanya uchaguzi".

Mhe. Spika, hapa kidogo namuomba Mhe. Waziri anisaidie lugha. Kwa kweli tunavyojua mpaka leo hii Chama cha Riadha bado hakijafanya uchaguzi, sababu gani hatuelewi. Mhe. Spika, chama hiki tunakiua kwa makusudi hili tukubali.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri usikubali urithi huu, kwa sababu huko nyuma kumefanyika manyago makubwa sana, watu wa riadha Mhe. Spika chama kimeuliwa tofauti na zamani, kwa nini na kasma inakwenda kwenye vifungu vyao, lakini hatimaye tunakuta wanahangaika na hali hiyo inasikitisha. Jambo la kushangaza watu hao wanatuletea medali na wakati tunapoletewa medali tunawasifu, lakini kuwasaidia hatuwasaidii ni kitu ambacho kinasikitisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna kipindi ambacho Mhe. Rais Mstaafu alitoa fedha kwa makusudi za kuwasaidia kwa ajili ya kuwapa zawadi vijana wako kwa kufanyakazi nzuri. Lakini hatimaye fedha hizo mpaka leo hajulikani amekula nani, isipokuwa kuna dhana amekula kiongozi wa chama hicho. Sasa Mhe. Waziri utanijuilisha ni kweli hizi fedha zimeliwa na kiongozi huyo, kwa sababu ameua hii moral ya vijana wetu, kwani baadaye wanaweza kushindwa.

Kwa mfano, tunakwenda Bara na tunashinda vizuri Mhe. Spika, lakini inaweza tukafika pahala na jambo baya zaidi hata lile posho, yaani vijana wanatilishwa saini na wala posho hawalipati, kwa kweli hali hii inasikitisha sana. Kwa hivyo, ninaomba Mhe. Spika, kuwa serikali kiipe nguvu kifungu hiki, kwa sababu wametuwekea heshima yetu nzuri ya Zanzibar. Vile vile naomba unisaidie kuhusu Uwanachama wetu wa nchi za Jumuia za wanachama wako wani na wepi?

Kwa maana hiyo, tunayo haki ya kuwa tumo kwenye jumuia na kama tumo kwenye jumuia, basi nakuomba Mhe. Waziri utuoneshe umuhimu wetu kuwemo katika hiyo Jumuia au Vyama vya Afrika ya Mashariki au Kimataifa vya Wakimbiaji wenzetu huko. Kwa kweli hivyo ndivyo vitu ambavyo tunaviona kweli tunanyimwa kabisa na wala hatupati fursa za kuweza kutusaidia.

Mhe. Spika, suala la mwisho kama nilivyosema kwamba niwasifu kutokana na jitihada zao na hii nielekeze kwa Mkurugenzi wa Mambo ya Kale. Kwa kweli namuomba sana Mkurugenzi wangu ajitahidi kuuleta ule mfumo hivi sasa wa kuwa utaratibu mzuri wa mambo ya kale na hizi zana asilia zetu zidizi kupaa juu siku hadi siku. Kwa mfano, hivi sasa utakuta vitu ambavyo viko nje ya maadili yetu viko katika mitaa.

Kwa hivyo, namuomba Mkurugenzi *special* suala hilo ajitahidi sana katika kujaribu kuurudisha utamaduni wetu wa Kizanzibari, hasa katika masuala ya usukaji wa akinamama kama vile mambo ya mikopa pamoja na mengine.

Mhe. Spika, namuomba sana Mkurugenzi, kwa sababu yeye ni msikivu sana na suala hili atalifuata, isipokuwa sisi tumtilie fungu lake liwe kubwa kwa ajili ya kuweza kufanya marekebisho hayo, kwa sababu tusiseme kwa nyimbo tu hapa na fungu tumtilie kubwa lenye kustahiki na kuweza kufanyakazi zake vizuri. Mhe. Spika, haya yote yanawezekana na yatawezekana kwa sababu anao uwezo wa kuyamudu kuyatekeleza Mhe. Waziri.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, naomba na ilikuwa nimnyime Mhe. Waziri nimwambie 25 *percent*, lakini hivi sasa namkamilishia nampa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope. *(Makofi)*

Ahsante sana.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia asubuhi hii kutupa uhai na uzima na kuweza kuendelea na Kikao chetu hiki cha Baraza la Wawakilishi.

Pili Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa mara nyengine katika Wizara hii sasa tunaijadili, ambayo ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. *(Makofi)*

Nimshukuru Mhe. Waziri na nimpongeze kwa *speed* yake jana ya *Marathon* katika kuisoma hotuba hii, maana yake hata wewe Mhe. Spika ulisema kwamba alimaliza juu ya nukta. Kwa kweli tulikuwa tukiulizana huku *backbenchers* kwamba tutaongeza muda wa Baraza, lakini akatuonesha kwamba kumbe anaweza kuwa mwanamichezo mzuri kwa *speed* kama ile. Kwa hivyo, tunampongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kuichangia bajeti hii kwanza naomba nianze na Sekta ya Habari. Kwanza nianze kwa kuipongeza wizara kwa mambo matatu.

Kwanza kufanikisha Tume ya Utangazaji ya Zanzibar kuwa mwanachama wa *East Africa Communication Organization*, ambalo umelitaja kwenye kitabu cha hotuba yako. Kwa kweli tunafurahi na kumbe inaonesha kwamba inawezekana Zanzibar kuwa mwanachama wa Jumuia za Kimataifa kwa yale mambo ambayo si ya Muungano. Kwa hiyo, nataka kumpongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Pili nataka nimpongeze kwa kulisimamia hili kwamba sasa Vikao vya Baraza la Wawakilishi vinaoneshwa live kama ilivyo kwa wenzetu kule Tanzania Bara. Mhe. Spika, kama unavyojua suala hili limeliongezea hadhi Baraza la Wawakilishi, nadhani hata kuwafanya Wajumbe nao wafikirie mara mbili wanachochangia humu ndani, kwa sababu wanajua wananchi huko nje wanatuona na wanaweza kutupima. *(Makofi)*

Tatu Mhe. Spika, nataka nimpongeze katika Sekta hii ya Habari kuhusu suala zima la Gazeti la Zanzibar Leo. Kwa kweli Gazeti la Zanzibar Leo limepiga hatua na wala siwezi kusema kwamba limefikia kilele cha mafanikio bado kuna kazi kubwa ya kufanyika. Lakini ukilitizama lilikokuwa na liliko leo imefanyika kazi na vijana wale tuna kila sababu ya kuwasifu na kuwapongeza pamoja na kuwatia moyo waendelee zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi ni mnunuzi mkubwa wa magazeti, kwa sababu siku zote ukienda pale ulikuwa unakuta magazeti yote yanaweza kwisha, lakini Zanzibar Leo ukalikuta limedoda pale na siku hizi Gazeti la Zanzibar Leo linashinda na magazeti yanayotoka Bara. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kiasi fulani limekuja na watu kuona kwamba sasa wanahamu ya kusoma habari zao zinazoandikwa na Zanzibar Leo limebadilisha hata mwelekeo *Editorial Policy*, kwa sababu zamani ulikuwa hukuti habari za *critical* ambazo zinazokosoa mambo ya serikali zinaandikwa mule. *(Makofi)*

Lakini hivi sasa tunaona na hii inaonesha kwamba wananchi wanafuatilia mambo haya. Sasa unapotoa habari zile na kuona kunandikwa ukweli na masuala yao yanayowagusa, upotevu wa fedha zao yanaandikwa mule, basi watu wanatuatilia. Kwa hivyo, nataka kulipongeza sana Gazeti la Zanzibar Leo kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizo Mhe. Spika, sasa nije kwenye masikitiko yangu na hasa nataka kuzungumzia kwa upande wa hivi Vyombo vya *Broadcasting*. Mhe. Spika, tumebadilisha muundo na tumeunda Shirika la Utangazaji la Zanzibar, ni *spirit* nzuri kuwafanya waweze kujitegemea vizuri zaidi na waweze kujiendesha kibiashara imani yangu. Kwa kweli bila ya shaka tumeona

mafanikio labda yaliyopatikana kwa wenzetu Bara kuanzisha *Tanzania Broadcasting Cooperation TBC*.

Lakini Mhe. Spika, huwezi kubadilisha mwenendo wa vyombo kama hivi na kuvutia watazamani pamoja na wasikilizaji kwa kubadilisha muundo tu wake au kubadilisha kutoka katika *Analogy* na kwenda *Digital* haitoshi Mhe. Spika. Kwa hivyo, kinacho-*matter* kikubwa katika vyombo kama hivi Mhe. Spika, ni nini kinaoneshwa na kinachotangazwa, yaani namna ya kutangaza na kuonesha, kwa maana nyengine ni suala la *content* na *presentation*. Mhe. Spika, bado Vyombo vyetu vya TVZ na STZ viko nyuma sana katika hili.

Mhe. Spika, sisi wengine kwa sababu ya uzalendo wetu kwa Zanzibar tunasikitika sana tunapoona watu hawaangalii vyombo vyetu. Lakini wakati mwengine wanatuambia tunatizama kitu gani na ushahidi wa hilo umo kwenye hotuba ya Mhe. Waziri, kwa sababu niliposema nini kinaonesha au kinatangazwa ni *content*. Mhe. Spika, tuangalie kwenye hotuba ya Mhe. Waziri ukurasa wa 19 unaozungumzia vipindi vya mwaka mzima, naomba kunukuu Mhe. Spika.

Ukurasa wa 19 kifungu cha 27 (iii) kinasema hivi:-

> "Jumla ya vipindi vya taaluma visivyopungua 140, habari ndio zinazoongoza kwa sababu zipo kila siku 3,275 na vipindi 40 vya kuburudisha jamii vimetayarishwa na kurushwa hewani kupitia Shirika hili."

Sasa huwezi Mhe. Spika, kwa mwaka mzima umetayarisha vipindi 140 vya taaluma na vipindi 40 ukasema hapo watu watavutika kuangalia vyombo vyetu hivi, haiwezekani Mhe. Spika.

Kwa kweli najua kiasi kikubwa haya yanachangiwa na upungufu wa bajeti zinazotengewa vyombo hivi. Vile vile kwa kiasi fulani Mhe. Spika, na wataalamu wa kutengeneza vipindi hatuna. Kwa mfano, TVZ ambayo ilikuwa ni harari katika eneo hili ukanda wa Afika Mashariki, ndio Televisheni ya mwanzo kuanzisha Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara na leo tumeifikisha pale.

Sauti ya Tanzania Zanzibar tokea ilipoanzishwa Sauti ya Unguja nafikiri Mhe. Spika, zama zenu nyie ndio mnakumbuka sisi tunasikia tu, kwamba ilikuwa ni fahari katika Afrika ya Mashariki nzima kwa mtu kusikia Lugha ya Kiswahili inavyotangazwa pale, yaani ile *content* ya vipindi vyake, lakini leo tunapokuwa hatuitilii fedha za kutosha wanashindwa, pia kwa namna tunavyoshindwa kuwatunza, basi wataalamu wetu wengi wazuri wameondoka. Kwa mfano,

zilipoanzishwa TV za Bara wengi wamekimbilia kule kwa sababu yapo malipo mazuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika tunahitaji kuangalia sana *content* ya vipindi pamoja na *presentation*, yaani yule mtangazaji anavyokaa na kumuona kwenye TV lugha anayotamka. Mhe. Spika, TVZ na Redio Zanzibar hivi ni vyombo vya kitaifa na katika Lugha mambo haya wanaita *Public Broadcasting* kama ilivyo *BBC* kwa Uingereza. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, pale ulitegemea upate kwa mfano unazungumzia lugha, yaani kile Kiswahili Fasaha ukisikie pale, lakini leo tunaona watangazaji wetu wanavyotutangazia Kiswahili, badala ya sisi kukopiwa kwa sababu sisi ndio wenyewe Kiswahili sasa imekuwa sisi tunakopia watu wengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna matatizo mengi sana katika hili na Mhe. Spika, naomba tuangalie sana kwenye suala la mafunzo wanayopatiwa vijana wale, pengine sio matatizo yao lakini sisi tunashindwa kuwapatia mafunzo ya kutosha kuweza kumudu kazi zao pia pengine *management* ni mbovu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hili nataka kusema mimi nimesikitishwa tena nimeshtushwa kwamba haionekani kuwa kweli tunayo dhamira ya kuvifanya vyombo hivi viwe fahari ya Zanzibar na Zanzibar iki-*claim* nafasi yake katika suala hili la habari, kwa nini nasema hivyo Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa kwlei tuliposikia uongozi mpya wa wizara hii tumekuja kushtukizia Wakurugenzi ambao tayari wameshastaafu wakaagwa na zawadi wakapewa wanarejeshwa tena. Mhe. Spika, katika wizara nafikiri inayoongoza kwa kurejesha watu hawa ni Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Sasa tunawathamini sana, lakini ukeshafika pahala kwamba umestaafu, kwa sababu hao walioweka mambo ya kustaafu Mhe. Spika walifanya kwa maana yao, kwani wako vijana wapya ambao wanao uwezo, basi tuwape nafasi ili waoneshe uwezo wao. Kwa mfano, tunapolisifu Zanzibar Leo ni kwamba Zanzibar Leo linaendeshwa na vijana na wamefanya ubunifu pale, hube tuwape nafasi Mhe. Spika hawa. *(Makofi)*

Kwa kweli unarejesha watu ambao waliongoza vyombo hivi kwa muda na wala hatukuona mabadiliko na wengine pia walichangia kuvifikisha hapa vilipofika. Kwa hivyo, tayari tumeshawapumzika na leo tunawarejesha tena pale na hawa ndio wanaowavunja moyo hawa vijana wetu na wala hawawapi nafasi, kwa sababu mara nyingi ukeshafika umri fulani kuna kawaida ya kuwa king'ang'anizi na wala sio katika madaraka tu, lakini hata namna ya kuendesha pale huwapi uhuru wa kutosha watu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka tuseme hebu Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa jumla iliangalie hili kwa uongozi tunaouweka pale sitegemei mimi kwamba tukiweka mtambo wa *Digital* kuwa tutapata mabadiliko, hivyo *content and presentation* itaendelea kuwa tatizo Mhe. Spika. *(Makofi)*

Suala jengine sio kuwapa mafunzo au uhuru wa kuendesha, lakini vijana wetu wanatakiwa wapewe motisha. Kwa mfano, tunawapeleka kufanyakazi wenzetu tunawaona wanapokuja kwenye vyombo vyao hivi, lakini kuwahudumia posho zao hazipo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, leo nashuhudia bajeti ya wizara hii katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi safari za ndani na nje zimetengewa shilingi milioni 86/=, lakini posho hata hawa wanaotuhudumia humu ndani Mhe. Spika sijui kama wanatizamwa kiasi gani. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Spika, hili tulitizame. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nasema tunakwenda katika hatua ya kuvipeleka vyombo hivi kutoka kwenye Mfumo wa *Analogy* kwenda katika *Digital*. Lakini kulikuwa na swali mara nyingi tumeliuliza kuhusu mitambo hii ya *Digital*, tumeuliza taarifa na Mhe. Waziri alituthibitishia humu Mitambo ile ya Serikali ililetwa kwa jina la mtu binafsi na tulipombana hapa alituambia kwamba ni *Officer* fulani wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Kwa kweli huu umejenga utaratibu katika Wizara ya Fedha, kwamba ukeshafika matumizi au manunuzi ya chombo kinachofikia kiasi fulani cha fedha basi wang'ania wanunua wao, sasa kama ingekuwa wananunua wao kwa niaba ya serikali, lakini kinanunuliwa kwa jina la *Officer* wa Wizara ya Fedha. Mhe. Spika, hapa kuna harufu ya rushwa na wala haiwezekani taratibu za serikali zikiukwe. *(Makofi)*

Sasa siku ile tulimuuliza Mhe. Waziri alituambia jina halikumbuki nadhani leo ameshapata muda wa kutosha kwa ajili ya kwenda kujiandaa na majumuisho, basi atakapokuja Mhe. Waziri atutajie jina la huyo *Officer* wa Wizara ya Fedha aliyeshiriki, ili itakapokuja bajeti ya Wizara ya Fedha basi tumbane Mhe. Waziri wa Fedha na tuambie kinaendelea nini katika Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nasisitiza kama hili hatukutajiwa basi mimi bajeti hii nitaizuia. Kwa hivyo, tutajiwe na Mhe. Waziri anaona tabu ya nini kututajia huyu mtu ambaye anakwambisha, vyombo vile vimekaa muda mrefu mpaka leo watu wa Unguja wanafaidika kuona TVZ na Pemba hawaoni, kwa sababu mitambo imekwama *Airport* muda mrefu hapo mpaka wakaingilia kamati na kwa kupiga kelele mambo mengine ndio imekwamuliwa.

Lakini bado suala lile halijapata majibu Mhe. Spika, fedha za wananchi tusichezee kama hivi, kwa sababu kuna watu *ICU* tumeshindwa kuipatia fedha, lakini kuna watu wengine wanachezea fedha katika ofisi tulizowakabidhi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, suala hili tuelezwe.

Mhe. Spika, naomba nizungumzie kwa kifupi sana suala la Chuo cha Habari. Kwa kweli imezungumzwa hapa kuna matatizo kwenye tunaambiwa wakati fulani hapa chuo hiki ile kwamba hakipewi nafasi yake sio kama kinatengewa fungu dogo, lakini kile wanachotengewa kinanyang'anywa.

Kwa mfano, tunaambiwa mwezi wa Disemba mwaka jana Mhe. Spika, shilingi milioni 92 zilizokuwa *allocated* pale zilichukuliwa na uongozi wa wizara, baada ya kelele nyingi ndio zikaanza kurejeshwa kidogo kidogo, lakini ziliathiri pa kubwa utendaji wa Chuo cha Habari. Kwa hivyo, nadhani hiki kinapaswa kutizamwa kwa vizuri sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tusiichie katika mafunzo kukiangalia Chuo cha Habari, kwa sababu hivi vyuo vinavyochipuka kila pahala vinavyoambiwa vinatoa mafunzo ya uandishi wa habari mara nyengine haya matatizo ya waandishi kutokuwa na maadili ni kwa sababu mafunzo yenyewe wanayopata si mazuri. Kwa kweli mafunzo hao wanapewa na vyuo ambavyo uwezo wao ni mdogo. *(Makofi)*

Sasa pia nataka wizara iviangalie hivi vyuo kama viko kwa wao au vinasimamiwa na Wizara ya Elimu, wanaotoa leseni za vyuo hivi ku-*operate* hasa katika mafunzo ya uandishi wa habari, kwa sababu waandishi wa habari wanabeba dhamana kubwa sana katika nchi, ikiwa mtu hakuelimishwa vizuri basi anaweza kupoteza taifa zima Mhe. Spika na hayo yanatokea.

Kwa hivyo, naomba hili nielezwe wizara inachukua hatua gani kuona kwamba inadhibiti leseni za vyuo kama hivi, ili tusijetukazalisha taifa la waandishi wa habari wanalipeleka pabaya taifa, kwa sababu tu ya kukosa mafunzo. Kwa kweli ndani yake kuna masuala ya *Social Responsibility, Ethics* pamoja na masuala ya kujua maslahi ya taifa yote hayo waandishi wanafunzwa, lakini ukija kupeleka vyuo vya mitaani pengine hao walimu wenyewe wanaosomesha hawazielewi fani hizi.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie suala la utamaduni. Kwanza hapa naomba ni-*declay interest* kama kanuni zinavyotaka. Mhe. Spika, hivi karibuni niliteuliwa Mjumbe wa Bodi ya Taasisi mpya yenye Makao Makuu Mji Mkongwe inayoitwa *Swahili Performing Art Centre*, kwa hiyo kwanza naomba ni-*declay interest* kwa sababu nimeteuliwa kuingia kwenye Bodi na vijana wa Mji Mkongwe.

Baada ya ku-*declay interest* Mhe. Spika, naomba niseme. Katika suala la utamaduni tunapiga kelele sana kuporomoka kwa maadili katika nchi yetu. Lakini ni kiasi gani sisi wenyewe tunachukua hatua kudhibiti hilo. Mhe. Spika, mara nyengine na kwa bahati nzuri mambo haya yote yako katika wizara moja, vyombo vyetu vya habari vyenyewe vinachangia kupotosha maadili pamoja na kuharibu utamaduni wa Mzanzibari. *(Makofi)*

Kwa mfano, mimi nakumbuka nilipokuwa kijana mdogo tulikiangalia TVZ ulikuwa huoni vituo unavyoviona leo, kwa sababu kulikuwa na udhibiti pamoja na sensa ya hali ya juu ya vipindi vilivyokuwa vikioneshwa pale na leo halipo hilo. Kwa hivyo, si lazima uone labda mambo ya ngono tu, lakini hata zile ngoma zinazooneshwa nyengine zinakiuka utamaduni wetu. Kwa mfano, kulikuwa na ngoma zikeshafika *stage* fulani kwa Zanzibar inakuwa ni mwiko kuoneshwa hadharani. *(Makofi)*

Sasa leo TVZ mambo yote imeweka hadharani na wala sio TVZ peke yake hata hizi *Cables* ambazo tumeziruhusu, hebu tutizame tunavuatilia kiasi gani hivyo vipindi vyao wanavyovionesha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wakati wetu sisi kulikuwa na Vipindi vya Watoto kuanzia saa 1:00 usiku mpaka 2:00 usiku na halafu kuna muda wa nusu saa wa mambo mbali mbali na wakati ule ilikuwa mwisho saa 4:00 usiku, halafu wakati wa vipindi vya watu wazima, basi mzee hamuachii hata siku moja mtoto akatizama. Lakini hata hivyo wa watu wazima ukivitizama vilikuwa havifikii *stage* ambavyo tunavyoviona leo. Kwa hivyo, katika suala la utamaduni kwanza vyombo vyetu vinapaswa visimamie vizuri.

Vile vile na hayo matamasha tuyatazame Mhe. Spika. Kwa kweli Mhe. Waziri ameyasifu sana matamasha na mimi nakubali yanachangia pa kubwa katika kukuza utalii, kuvutia wageni kuja, lakini ni kitu gani kinachooneshwa kwenye matamasha haya au kitu gani kinachoshirikishwa katika matamasha haya.

Mhe. Spika, tunalo tatizo moja na ninaomba Mhe. Waziri alitizame sana, kwa sababu si nchi nyingi duniani labda nchi ambayo haina wenyewe inayowachia uendeshaji, yaani *management* ya masuala ya utamaduni kwa wageni, kwani utamaduni wa nchi ndio utambulisho wa taifa au roho ya taifa.

Kwa mfano, leo sisi kama tumechoka kila jambo hata uendeshaji wa Matamasha ya Utamaduni tumewaachia wageni watupu na tukaangalie Bodi inayosimamia wengi si Wazanzibar na hawa wana-*commercialize* mambo ya utamaduni haya yamefanywa yamekuwa ni mambo ya kibiashara sasa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, huwezi kuiachia roho ya taifa au utambulisho wa taifa ukamuachia mgeni kufanyia biashara na wala haiwezekani Mhe. Spika, tunazitaka fedha kweli na tunataka utalii ukue, lakini si kwa gharama ya mmong'onyoko wa maadili na kuharibu msingi ya taifa letu pamoja na utambulisho wa taifa letu.

Kwa maana hiyo, Mhe. Spika nataka Mhe. Waziri aje anijibu kwamba anayo mipango gani kuona kwamba masuala ya *management* katika *Policy* au Sera ya Utamaduni kiasi gani tuone Wazanzibari wenyewe wanaendesha. Kwa kweli tunao watu Mhe. Spika na wengine mpaka wamekufa hivi karibuni hata kukumbuka na kutunzwa tumeshindwa, hawa ndio ilikuwa tuwape kazi hii ya kusimamia utamaduni wa nchi yetu kuhusu matamasha haya na hao ndio watakaojua Utamaduni wa Mzanzibari kuliko mtu anayetoka nje ya nchi. Kwa hivyo, naomba suala hili litizamwe sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapo nataka kuunganisha na Bodi ya Sensa kuhusu masuala ya utamaduni na maadili. Kwa hiyo, naomba hii tuirejeshee meno yake kwa mfano kuna hii michezo na tunajua kudhibiti leo si kazi rahisi kama ilivyokuwa zamani, tunavyoambiwa utandawazi.

Lakini hivi vipindi vimejaa kwenye *DVD* na vinauzwa mitaani na vyengine havitoki mbali, yaani vinatoka upande wa pili tu wa bahari, sasa utamaduni wao na wetu sisi ni tofauti, kwa sababu mambo wanayoyaonesha mule na lugha zinazotumika kwetu sisi hapa ni mwiko. Kwa mfano, Mhe. Spika akina Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak wanajua mambo mengine au lugha zetu na mama zetu wanajua kwamba ni mwiko kwa Zanzibar.

Sasa vyengine ukiviangalia unaona haya hata kukaa na familia yako kwa ajili ya kuvitizama tena ni vipindi vya hapa Tanzania. Kutokana na hali hiyo, naomba Bodi ya Sensa ilichangamkie na wala nisifahamike vibaya, lakini hata michezo inayooneshwa kama vile ile inayotoka *Hollywood* au *Bollywood* ama popote hebu tuiangalie ni kiasi gani inasaidia kutunza au inavuruga maadili yetu.

Mhe. Spika, hapo kwenye utamaduni kwa upande wa *positive note*. Kwa kweli tunalo tatizo kubwa la kutothamini na kutokuwakumbuka kama nilivyosema kwamba watu ambao wametoa mchango mkubwa katika utamaduni wa nchi yetu. Kwa mfano, katika mambo ya sanaa, *music*, uigizaji kuna mambo mengi mpaka wengine wanafika kufa hata kuhudumiwa wanashindwa kuhudumiwa.

Mhe. Spika, leo kunafanyika matamasha nje wanakumbukwa wanamuziki wetu na kupewa tunzo na sisi wenyewe humu ndani tunawasahau humu ndani. Mhe. Spika, wakati wa uchaguzi kulikuwa na vijana wa Kizanzibari hawa wa Muziki

wa Kizazi Kipya walifanya nyimbo ile inayojulikana kwamba *Zanzibar We are Together*, yaani ilikuwa inasisimiwa ukiisikiliza jinsi ilivyokuwa ikihusia kuacha siasa za zamani za vurugu na kuelekea katika umoja na masikilizano. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nilitegemea vijana wale wangetunzwa, yaani wangekuwa *recognize* kwa ule mchango walioutoa, lakini hatukuwakumbuka. Mhe. Spika, wako wengi kama vile marehemu Maalim Seif Salim na juzi amekufa Moh'd Machaprala, marehemu Bakari Abeid na hawa wametoa mchango mkubwa, hivi tunasubiri mpaka wafe ndio tuwakumbuke. Sasa naomba suala hili tuliangalie vizuri Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa nizungumzi kuhusu suala la utalii. Katika utalii kwanza niseme naunga mkono ripoti ya kamati kwamba tuna haja ya kuangalia hizi. *Package Tourism* kiasi gani zinatusaidia sisi? Kama kuna mapungufu yako wapi? Kwa hivyo, tunaweza kurekebisha vipi, ili hayo mapato yafaidishe Zanzibar. Mhe. Spika, na hili naomba tuliangalie vizuri. Pia katika hili tuangalie kwenye *High Class of Tourism,* badala ya kutegemea hawa watalii ambao wanakuja hapa wengi wao wanachangia kuharibu maadili yetu, wanaokuja hapa ni watu wenye pesa zao, wameshastaafu wao wenyewe wanataka *class* ambayo inathamini utamaduni wao na wa nchi nyengine, kwa hivyo nilikuwa naomba hili tulitizame.

Lakini Mhe. Spika, jana tulipokuwa tunajadili hotuba ya Mwalimu wangu Mhe. Haroun Ali Suleiman nilizungumza suala hili la *tours* na umuhimu wa kazi hizi kuonekana kwamba zinafanywa na wenyeji kama sheria zetu zinavyotaka na sio zinafanywa na wageni, mahoteli yaliyoanzisha kazi hizi kuwanyima wageni naomba Mhe. Waziri alitizame kwa karibu.

Hapo hapo awaangalie hawa *guide* wanaotembeza watalii hawa ambao wengi ukiwasikiliza historia ya Zanzibar hawaijui wanapitisha watu mitaani wakiwapotosha tu, tunakutana nao mara nyingi tu sasa nashangaa Wizara ina taratibu za kuwajua hawa na kujuhua kwamba wanaijua historia ya Zanzibar ni sawa sawa, sio kuchukua watu humo nje wakenda kuchukua watu humo mitaani akawaambia wageni anawaondosha na taswira ile ya Zanzibar pengine mwingi inakuwa ni sahihi, kwa hivyo naomba aliangalie.

Lakini katika utalii naomba nije na mambo mawili, kwanza suala la kisiwa cha Changuu Mhe. Spika, nilipokea ripoti za kamati zako hizi mwezi wa machi hapa na Kamati ya *PAC* ilihoji kwa nini shirika la Utalii limekodisha kisiwa cha Changuu kwa dola 3,500 lakini shirika lenyewe lilikuwa linakusanya zaidi ya dola 8,000. Sasa Mhe. Spika, unapokodisha unategemea upate faida sio upate hasara kama Wizara ya Utalii ilikuwa inapata Shs. 8,000 kwa nini

ukamkodishe mtu ambae katoa dola 3,500 angalau angekuwa katoa hizo na kufanya kazi kubwa ya kukiendeleza na kukijenga hakuna chochote kinachofanyika pale.

Kwa hivyo nilikuwa naomba hilo Mhe. Spika, akija Waziri anipatie maelezo lini atachukua hatua ya kukirejesha kisiwa cha Changuu katika mikono ya Shirika la Utalii, ili kiendelezwe kama kilivyokuwa mwanzo.

Lakini hapa sasa nizungumzie suala la Bwawani, hoteli ya Bwawani pia katika ripoti hii ilizungumzwa kwamba palitangazwa tenda na katika tenda ambazo Mhe. Waziri kaja nazo katika kitabu chake kwenye viambatisho pale amezungumzia hili katika kiambatisho namba 4 kwenye tenda namba 2 ya mwaka 2011 ukodishwaji wa ukumbi wa Komba Disco, kazitaja kampuni pale *Zanzibar Medium Corporation, Star times Production, National Marketing Corporation na Prime time Promotion.*

Mhe. Spika, tulihoji hapa kwamba miongoni mwa hawa wako ambao walitoa milioni sitini kwa mwezi, wako ambao walikubali kutoa milioni arubaini hawakupewa wamepewa *National Marketing* yenye kutoa milioni kumi na tano kwa mwezi, tulipouliza tukajibiwa kwamba ni kwa sababu ya uzoefu, lakini najiuliza huu uzoefu wa kupiga disco huyu si kaupatia pale Bwawani maana hii *National Marketing* kabla ya hapo haikuwa na biashara hii. Sasa kama yeye kaupata uzoefu hao wengine udhoefu wa kupiga disco wanataka mafunzo gani ambao wengine hawawezi kuupata Mhe. Spika, hapa pana harufu ya mchezo mchafu na hasa ukitizama kwamba imesemwa analipa milioni kumi na tano alichotakiwa, lakini anacholipa pale ni milioni kumi na tano anasema anatuwekezea. Wakati mkataba ulisema mkodishwaji ndio ahudumie yule matengenezo ya ukumbi.

Sasa yeye anakata milioni tano na Wizara imemuwekea wakati mkataba umefungwa vyengine pana kitu gani hapa Mhe. Spika, hebu naomba katika hili pia Mhe. Waziri akija atueleze tena kwa kina kabisa turidhike si hivyo kutakuwa na matatizo makubwa katika kupitisha bajeti hii Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nimalizie kwenye Idara ya Makumbusho nilikuwa naomba kuzungumzia hali ya majumba yetu ya kihistoria na magofu ya kihistoria, Mhe. Spika, hali ukitizama inasikitisha sana Zanzibar ni kitovu cha utamaduni na kitovu cha historia katika ukanda huu wa Afrika ya Mashariki na sio Afrika ya Mashariki tu lakini katika yote inaitwa *The Indian Ocean rell*, bahari ya hindi dola hizi zilizokuwa zikitapakaa katika ukanda huu sasa sisi tumeachiwa dhamana ya kutunza majengo ambayo ni urithi sio kwetu sisi tu, lakini kwa dunia nzima na nchi ambazo zimeathirika na sisi katika historia.

Lakini utunzaji wake umekuwa mbaya sana mengi baadhi yao yako Mji Mkongwe ukenda ukiangalia jengo lilokuwa Makumbusho pale Mnazi Mmoja ile lilijengwa baada ya vita vya kwanza vya dunia ikaitwa *Peace Memoriam Museum* tumehama pale makumbusho tumeyahamishia Beit el Ajab lakini hivyo kuhama ndio kuliacha lile jengo mpaka liporomoke, hivi sasa hivi hali yake mbaya linavuja ukitazama ni jengo lililokuwa la fahari likipendeza pale tunashindwa kulitunza, nenda katika kasri Forodhani pale hata kuipaka rangi nyeupe inatushinda, linatumia lile kama sehemu pa kufanyiwa Baraza la Iddi kila mwaka mara mbili lakini hata kulipaka rangi tunashindwa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, *Livingston house* ukiitizama hali yake sijui kama halitoanguka tunalifahariddha *Livingston House* Mhe. Waziri kasema humu kwamba kuna taasisi inakuja kulitengeneza, lakini nasema hili mpaka tupate taasisi zije kulitengeneza za nje Mhe. Spika, lakini hata magofu haya uendeshaji wake ukenda pale Pemba Chake Chake kuna Ngome Kongwe, hali yake tumekwenda kukagua ilikuwa mbaya kweli kweli kwa sababu humo ndani pia ndio kwenye Idara hii ya Nyaraka. Lakini hata hapa ukitizama magofu yote ya kihistoria.

Lakini Mhe. Spika, kuna wasi wasi huko nje kwamba magofu haya yamegeuzwa mirathi ya watu vile vile, utolewaji wake wa nani anapewa pale umekuwa unategemea mtu labda anafaidika vipi, naomba hili tulitazame sana Mhe. Spika, kwa sababu kama nilivyosema ile kumilikisha wageni kila pahala hata haya mengi tumewapa watu ambao wamekuwa wakiyatumia vibayka. Kwa hivyo nilikuwa naomba Waziri atupie jicho la rehema haya majengo ya magofu na majengo mengine.

Mhe. Spika, unapoachia wageni ni kama pale Mtoni pana msikiti pale karibu na ile kasri ya zamani ya Mtoni ambayo wanaita Mtoni *Palace* yule aliyepewa kusimamia yale anataka kufanya mpaka ule msikiti kufungia watu wasiende pale, kwa sababu pana geti ukitaka kuingia pale mpaka upite. Kwa hivyo sehemu kama zile kuwaachia wageni wao hawajui vitu kama hivi na matumizi yake. Kwa hivyo nilikuwa naomba tuyatunze tuyafanyie matengenezo kila wakati ili ile historia ambayo tumeachiwa Mhe. Spika, tuendelee kuilinda.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nazuia kwanza kuiunda mkono bajeti hii mpaka nitakapopata matumizi ya kina kwa yale mambo niliyotaja hapa kuhusu mitambo ya *digital* aliyoleta hatujatajiwa, suala la Bwawani na suala la Kisiwa cha Changuu. Mhe. Spika, nakushukuru sana *(Makofi).*

**Mhe. Mahamoud Muhammad Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia salama, lakini pia nikushukuru wewe kwa namna

unavyoendesha shughuli zako kwa umakini zaidi na sisi tukaweza kujifunza na kuelewa zaidi.

Jengine Mhe. Spika, napenda kuchukua fura hii pia kumshukuru Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Naibu wake na uongozi mzima wa Wizara husika kwa mujibu wa kutuletea hutuba hii ambayo ni safi na murua kabisa pamoja na kwamba kutakuwa na mambo ya hapa na pale, hii ni kawaida ya kibinaadamu tunaweza kusaidiana mawazo na maarifa.

Mhe. Spika, mimi kwa kuanza naanza na suala zima la watangazaji na maslahi yao, waswahili tuna msemo unaosema kila ukikiona kizuri basi ujue kwamba kimetunzwa, ndugu yangu hapa Mhe. Makame Mshimba alipoanza ameanza na jitihada za kuwasifu ndugu zetu waandishi wa habari na watu ambao wanatuangalia kwa kina huko nje tunapokuwepo, wao wakikaa kule nje wanaona hali halisi inavyoendelea humu ndani ya Baraza letu, sasa hizi ni juhudi ambazo zimechukuliwa na Wizara hii lakini zaidi na watendaji ambao wanaendelea na shughuli hizi, sasa na hawa watendaji wenyewe basi waangalie namna wao wanavyoifanya kazi yao na namna ya maslahi ambayo wanayapata katika kazi hizi.

Mhe. Spika, Zanzibar ni ndogo na sote ni wamoja tumepata bahati ya kukaa nao na kuzungumza nao na kubadilishana nao mawazo, lakini wana malalamiko hawa huwa wanalalamika juu yetu, wanakaa wanaangalia na wanasikia wale wenzao kule bara ambao wanaingia kwenye bunge kule bara nao vile vile wanatengenezewa maslahi mazuri kidigo. Sasa na wao wana vilio vyao hawa tuwaangalie zaidi katika namna ambavyo wanafanya hizi kazi na kuweza kutufurahisha Wazanzibari wote, Watanzania na dunia kwa jumla kwa hivyo na wao tuwaangalie zaidi katika maslahi yao kama ambayo wenyewe wanakaa wakawa wanalalamika.

Mhe. Spika, nikienda katika kitengo cha pili kwa sasa ilikuwa naangalia zaidi eneo la TVZ, Sauti ya Tanzania Zanziabar, Masingini na Idara ya TVZ kule Pemba, Mhe. Spika, fahari ya Wazanzibari na furaha yao zaidi ni mambo mawili, kwanza kabisa unapokosa mchele Zanzibar basi tatizo linakuwa katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Lakini jambo la pili hususan kwa wazee wanapokaa na wanapokosa matangazo hususan yale ya vifo na taarifa za habari inakuwa ni tatizo kubwa zaidi, Mhe. Spika, wakati umefika sasa kwa sababu katika maelekezo humu tumeona kwamba kuna mitambo mipya ambayo baadae nitakwenda kuzungumzia kidogo, lakini sasa mitambo hii mipya ambayo imekuja naomba iende sambamba na suala zima la kuboresha huduma hii muhimu ili isiwe ya kubahatisha.

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba tunakuwa hatuna huduma za uhakika ya mawasiliano kama Televisheni na Redio ndani ya nchi yetu tunakwenda tukisua sua, pamoja na juhudi za serikali kuona kwamba tutapatiwa na vimeshakuja vifaa hivyo ambavyo baadae tutavielezea huko mbele, lakini tunaomba kupitia bajeti hii ya mwaka huu vifaa hivi vitumike kwa uhakika zaidi. Isiwa masuala ya kusua sua yakawa tena yanaendelea leo matangazo yapo machana yanaendelea, lakini jioni yanakosekana tunaomba tufanye uhakika wa masuala haya na yasiwe mambo ya kubahatisha kwa mara nyengine tena.

Jengine ambalo nilikuwa nataka kuchangia zaidi ni jinsi ya hii mitambo ambayo tayari imeshafika, mimi nimepatwa na wasi wasi kidogo kuona kwamba hizi taarifa za hii mitambo ambayo imekuja na namna ya utoaji wake na utoaji wake katika maeneo yetu ya bandari, mimi nimeshituka bandari ya *Air Port* nimeshtuka kidogo. Kinachonishtua zaidi inaonekana kwamba mitambo hii pamoja na kwamba imewasili ina maana itakuwa hakuna wataalam ambao watakuwa wanakuja kuhusika na mitambo hii, kikawaida wataalam mitambo inapokuja katika sehemu yoyote pale na mtaalam huwa yuko nyuma yake yeye huwa anatoa shindikizo kwa sababu aweze kuweka vifaa vile ili aweze kurudi katika maeneo yake mengine kuendelea na mambo mengine.

Lakini vifaa hivi tokea vimefika naona kuna hadithi za kusua sua kidogo sasa naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze hasa hivi vifaa vimekuja vimeletwa tu au vimeletwa na wataalam wambao watakuja kuvishughulikia na kuona kwamba vitakuwa sio vya kuja mara moja, au siku mbili au tatu baadae tukaanza kutafuta vyengine.

Mhe. Spika baada ya hatua hiyo sasa nije kwenye jenereta, kwa mujibu wa taaarifa ambazo Mhe. Waziri wa Ardhi na Majenzi hapa alizozitoa juzi alisema kwamba suala la mgao wa umeme ni la kuendelea, sasa tumepata taarifa hapa kwamba kuna vifaa na mashine mpya ambazo zimekuja kwa ajili ya mawasiliano, lakini sijasikia taarifa kuhusiana na majenereta haya majenereta yana umuhimu wake kuhakikisha kwamba lile tatizo ambalo wananchi wanalipata la kutokuwa na uhakika wa kusikiliza taarifa linamalizika. Naomba sana Wizazara kama tutakuwa na mapungufu ya bajeti basi tuhakikishe kwamba tunamuomba Mhe. Waziri wa Fedha hapa anasaidia na kuona kwamba jenereta linapatikana la uhakika katika maeneo haya ya vyanzo vya habari ili mawasiliano yawe ya uhakika katika nchi ya Zanzibar.

Jengine Mhe. Spika ni suala la utalii wenzangu wameogolea katika suala hili na wengine nawaachia nafasi ili waweze kuogolea zaidi lakini mimi nilikuwa nataka kugusa sekta hii ya *tour operator* zaidi katika suala la usafiri wa

magari, tayari Mzanzibari ambae anamiliki gari anakwenda kufanya kazi ya *tour operator* tunampa leseni kila mwaka ili aweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Lakini pamoja na leseni ambayo anapewe kuna tatizo la kwamba kila anapopakia wageni dereva huyu lazima aende akatafute na vibali vyengine vya ziada, lakini tayari huyu mtu tumeshampa leseni kwamba afanye kazi ile hivi vibali vidogo vidogo vya kila wakati anapokuwa na wageni vya kazi gani.

Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelezee sababu za msingi zinazosababisha baada ya kwisha kumpa leseni dereva huyu na gari yake tukawa na vibali vyengine tena, wakati tayari yule amepewa leseni kwa ajili ya kazi ile.

Mhe. Spika, kwa kuendelea zaidi nakuja hotali ya Bwawani, tumeona hapa katika taarifa ambazo zimezungumzwa ndani ya kitabu hiki kwamba hoteli ya Bwawani ipo na inaendelea na baadhi ya shughuli zake, lakini hatukuona eneo ambalo kuna mapato katika hoteli hii. Hoteli hii kile ukienda unaambiwa kumbi zimejaa lakini humu hatukupewa nafasi ya kuweza kuangalia mapato gani yanapatikana kuhusiana nasuala la ukusanyaji au ukodishwaji wa zile kumbi na maeneo mengine ndani ya hoteli ile, kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja hapa tunaomba atusaidia zaidi hili.

Jengine nakwenda katika hali ya makumbusho na hadhi zake, Mhe. Ismail Jussa Ladhu amelizungumzia suala la makumbusho na zaidi akaumwa zaidi na kumbusho lililokuwepo pale Mnazi Mmoja, lakini mimi nazidi zaidi kwenda mpaka yale Mahamam yaliyokuwepo maeneo mengine vile ndio vitambulisho vyetu Mhe. Spika, katika nchi yetu ya Zanzibar. Sasa kwa mujibu wa hali tunayokwenda nayo tutafika pahala makumbusho yale yatakuwa hayapo tena na yatakuwa yameanguka wenyewe na itakuwa hatuna historia ya kuweza kuwaelezea wageni na wajukuu zetu ambao tutakuwa tunawazaa katika nchi hii.

Mhe. Spika, kwa fursa hii ambayo tunaipata hapa sasa hivi namuomba Mhe. Waziri, kutengeneza utaratibu maalum na mikakati maalum kutunza na kuendeleza kumbu kumbu za Zanzibar ili zisiweze kupotea.

Ka kuendelea zaidi nakuja katika suala la lugha na utunzaji wake, Mhe. Spika, kama alivyoendelea mwenzangu hapa kuzungumza kwamba lugha ya Zanzibar sasa inapotea kwa nguvu, Kiswahili asili yake ni Zanzibar lakini kwa namna tunvyokwenda sasa tumefika pahala sisi tunasomeshwa Kiswahili haya ni mambo ya maajabu makubwa sana Mhe. Spika. Tunaomba Mhe. Waziri na wasaidizi wake katika wizara yake husika kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inatunzwa, inaenziwa na kuendelezwa ndani ya Zanzibar kwa manufaa ya Wazanzibar na watanzania na dunia kwa jumla.

Mhe. Spika, juzi katika sherehe nilikuwa na Mkuu wa Mkoa Mhe. Abdalla Mwinyi tukawa tunasikiliza utenzi pale, sasa maalim akanitania akaniuliza Mheshimiwa Mahamoud huu ni utenzi ashairi, mbona mimi sifahamu kama utenzi au ushairi. Sasa haya yanatokana na jinsi hali halisi inavyojiendesha sasa hivi ndani ya nchi yetu kwa kuweza kuitupa hii lugha ya Kiswahili na ikawa muelekeo wake sasa unapotea.

Mimi siwezi kuzungumza mengi sana kwa sababu mwalimu wangu yupo pale Maalim Mshindo katika fani hii, lakini namuomba maalim yale aliyotupa sisi wakati tupo taasisi pale ayaendeleze na ahakikishe kwamba yanakuwa na manufaa na kuenziwa kwa manufaa ya Wazanzibari wote kwa ujumla.

Mhe. Spika, nije katika tamasha la Mzanzibari katika sekta hii ya utamaduni na kuenzi tamasha letu la Mzanzibari naomba jamani pamoja na hali na mwelekeo mzuri ambao tunaelekea kuuona katika utunzaji wa matamasha yetu, pamoja na utamaduni wetu wa Kizanzibari naomba tuwe makini sana kuhakikisha kwamba tamaduni na ile hali ya Wazanzibari iweze kutekelezwa na kutunzwa kwa mujibu wa taratibu zetu. Mwaka jana katika shehere za Tanganyika pale Dar es Salaam tulipata fursa ya kuwakilisha baadhi ya wajumbe wenzetu wa Baraza la Wawakilishi tukenda pale uwanja wa Dar es Salaam kilichotokea pale kilitushtusha, tuliona ngoma pale tukaambiwa kwamba hii ni ngoma asilia ya Kizanzibari ikalizwa katika uwanja ule wa sherehe kwa kweli tulishtuka sana, kwanza ile ngoma iliyokuja pale haina hasa muelekezo wa Kizanzibari lakini wachezaji na waendelezaji wa ngoma ile ilikuwa sio Wazanzibari wenyewe.

Lakini tukaambiwa kwamba lile ni tamasha la Utamaduni wa Kizanzibari tulishtuka sana Mhe. Spika, sasa hii inatuonyesha jinsi gani ambavyo utamaduni wetu na matamasha yetu hatuyaenzi katika nchi yetu na badala yake tunakimbilia tamaduni za wenzetu, ningeliomba sana utambulisho wa nchi pamoja na utamaduni vile vile. Kwa hivyo hili Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuhakikishie kwamba analitengenezea utaratibu maalum na kuona kwamba Wazanzibari tunajitunza wenyewe sio tusubiri kutunzawa na watu wengine.

Mwisho Mhe. Spika, kwa kumalizia ni suala la bodi ya sensa . Mhe. Spika, sijui bodi hii kama ipo au sijui labda wenyewe wamekwenda likizo kidogo, kwa sababu hatali halisi tunavyokwenda katika nchi yetu sasa hivi inatisha, tukiangalia tuna maendeleo na maendeleo yanapokuja pahala popote pale na fujo zinaongezeka Mhe. Spika, sasa tumefika pahala watoto wetu wenye umri wa miaka kumi na mbili, kumi na tano na kuendelea ikifika Magharibi wanakwenda zao kwenye *internet*. Mhe. Spika, huku kuna mambo mengi sana sasa wamekuwa wao ni mafundi na walimu wazuri zaidi kuliko sisi wenyewe

hili ni jambo la kutizamwa sana, sasa hii bodi kama ipo sijui itakuwa na mkakati gani kuhakikisha mambo kama haya yanaangaliwa na kuendelezwa katika mila na silka za Kizanzibari kama ambavyo wazee wetu walikuwa wakitufahamisha huko nyuma.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo ili sote tuweze kukpata nafasi ya kuchagia kwa heshima na taadhima, kwa niaba yangu , kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa umoja wao naunga mkono hoja. Ahsante sana Mhe. Waziri. *(Makofi)*

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Asante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo hotuba ambayo nzuri tunampongeza sana Mhe. Waziri kwa kuandaa hotuba hii ambayo ina mwelekeo mzuri.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba hii kwanza nachukua fursa hii kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa jana timu yako ya Baraza la Wawakilishi kwa kupata udhamini wa vifaa vya michezo vyenye thamani ya shilingi milioni kumi nakupongeza sana na naipongeza sana timu ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya hapo na mimi pia kama waziri alivyozungumza nachukua nafasi hii kuwapongeza timu yetu ya Judo kwa kuweza kutuletea ushindi ambao wamepata medali tano za dhahabu na kuiletea sima Zanzibar. Niwapongeze sana kwa sababu huu ndio mwelekeo ambao Zanzibar tunahitaji katika kuleta medali na vikombe hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi nitaanzia sekta ya habari pia katika Idara ya Habari Maelezo, nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi Idara ya Habari Maelezo pale kwa kuweza kufanya ukarabati mzuri lile jengo la idara ya Habari ukweli hali yake ilikuwa ni mbaya na kwa kweli hivi sasa ukipita pale Idara ya Habari ambayo imo katika jimbo langu la Rahaleo ukipita pale unafurahia sana kwa kuona jengo lile linapendeza. Mhe. Spika, vile vile niipongeze idara hii kwa kuweza kueneza habari zote zinazotokea hapa Zanzibar katika vyombo mbali mbali vya habari pamoja na kuzitangaza balozi zetu katika nchi mbali mbali,

Mhe. Spika, sasa nije katika gazeti la Zanzibar leo gazeti letu katika miaka ya nyuma tulikuwa tunalisoma kwa sababu ni letu lakini lilikuwa katika hali mbaya, lakini hivi sasa gazeti la Zanzibar leo linapendeza, linajiuza kwa hivyo nachukua fursa hii kuipongeza Wizara kwa kuweza kulifanyia ukarabati gazeti lile na kuweza kutoa sura ya kuuza gazeti lile ukiliona tu linapendeza. Lakini Mhe. Spika, gazeti ni zuri lakini nyumba yake mbovu tena inasikitisha sana kuona ofisi za Gazeti la Zanzibar leo ukipita pale linasikitisha, jumba lile ni

jumba la historia, jumba lazamani. Ningemuomba sana Mhe. Waziri akaliangalia lile jengo na kuweza kulifanyia ukarabati japo wa rangi, namuomba sana Mhe. Waziri kwa sababu ukipita pale jengo lile la redio unaona linapendeza, Jengo la Habari Maelezo linapendeza lakini jengo la Zanzibar leo liko katika hali mbaya, namuomba sana Mhe. Waziri alifanyie ukarabati jengo lile.

Mhe. Spika, baada ya kutoka haop nielekee kwenye kamisheni ya utamaduni na Michezo ambayo ipo katika ukurasa wa 48 mpaka 52, suala la michezo Zanzibar na duniani kote kwa ujumla michezo inaleta afya, michezo inaleta udugu, michezo inatukusanyisha wananchi na binaadamu wote katika hali ya kujuana na kupendana. Lakini cha kusikitisha michezo Zanzibar inakufa tena sio mchezo mmoja ni michezo yote, tukianzia na viwanja vyetu vya michezo sio mpira wa miguu, sio *net boll* na michezo mingine hali ya viwanja vya michezo havifai hatuna viwanja vya michezo.

Mhe. Spika, leo umefika wakati tunashindwa kuandaa mashindano kwa sababu hatuna viwanja vya michezo, mimi nakumbuka katika miaka ya nyuma tu Uwanja wa Amaan ulikuwa ndio uwanja Bora kwa nchi za Afrika ya Mashariki na Kati, leo katika uwanja mbovu basi ni uwanja wa Amani mbali na matengenezo yaliyofanywa katika kipindi cha nyuma wa kuweza kutumia dola milioni moja takriban 1.5 bilioni. Lakini uwanja ule tokea kutengenezwa haujachezewa mechi ya ligi hata siku moja, mimi nakumbuka tuliutumia uwanja ule kwenye Mechi ya ufunguzi tukautumia uwanja ule kwa mashindano ya Kombe la Mapinduzi hatujautumia uwanja ule katika mashindano mengine.

Kama nilivyozungumza hapo nyuma juzi tu Zanzibar ilikuwa iwe mwenyeji wa mashindano ya Kagame lakini hatukuweza kuandaa mashindano yale na sababu ni kwamba hatuna uwanja, hii ni aibu kubwa ningemuomba sana Mhe. Waziri akaangalia sana katika suala la kujenga viwanja vya michezo, katika suala la kuvienzi viwanja vyetu vya michezo.

Mhe. Spika, ukija katika uwanja wa Mao tse tung, juzi timu yako ya Baraza la Wawakilishi tumecheza pale mechi na timu ya Mameneja wa mabenki na sote waheshimiwa tulikuwa mashuhuda, uwanja ule umetupa maumivu kwa mchezaji wetu tegemeo Mhe. Abdalla Moh'd Ali kutokana na uwanja mbovu, kwa hivyo ipo haja ya kuviangalia viwanja na yeye mwenyewe Mhe. Waziri alikuwa mchezaji pale namba 4 ni mchezaji mzuri nampongeza sana. *(Makofi)*

Halafu Mhe. Spika, ukija katika Uwanja wa Gombani kule Pemba nakumbuka Mhe. Waziri hapa alitwambia kwamba uwanja baada ya kikao hiki utakuwa uko tayari, lakini mpaka leo uwanja ule haujakuwa tayari. Nataka anieleze Mhe. Waziri ni sababu gani zilizofanya uwanja ule wa Gombani mpaka leo

haujakuwa tayari na kusababisha timu zetu ambazo zinashiriki katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika na kombe la Shirikisho, hivi sasa kutaka kujiondoa katika mashindano haya kwa sababu hakuna viwanja. Sababu ya pili ni kwamba timu zetu ni masikini hazina pesa. Lakini kiwanja pia ni sababu kwa ingekuwa viwanja vile ni vizima pengine wangeweza kujisaidia katika mashindano yale. Mhe. Spika, sababu kubwa ni kwamba viwanja hatuna inabidi waende Dar es Salaam kwenda kucheza mashindano yale. Kwa hivyo, nimemuomba Mhe. Waziri akija hapa atueleze ni lini viwanja vyetu vitakuwa viko tayari.

Mhe. Spika, nakuja katika migogoro ya vyama. Mhe. Spika, hivi sasa imekuwa ni nyimbo katika vyombo vya habari redio na televisheni, magezeti kila siku tunaangalia migogoro ya vyama vyetu vya michezo kama vile mpira wa miguu, riadhaa na michezo mengine. Mhe. Spika, ni kwamba kila siku kuna migogoro, kwa nini inafika wakati vyama hivi vinapelekwa Mahakamani.

Mhe. Spika, gazeti la juzi mpaka vyama vya Wilayani sasa hivi vinapelekwa Mahakamani, hilo ni jambo la aibu sana. *ZFA* Taifa wana kesi Mahakamani, *ZFA* Wilaya wana kesi Mahakamani, hili ni jambo la aibu jamani. Mhe. Spika, sisi tunaelekea katika kuomba uanachama wa *FIFA* na siku hizi ni mtandao Mhe. Spika, habari zote hizi zinaenea katika ulimwengu. Kwa hivyo, ukionekana katika ulimwengu kwamba huko tunapelekana Mahakamani, hivyo kweli ndio tutaupata uanachama wa *FIFA*. Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri akahakikisha kwamba anakaa na vyama hivi vya michezo kupanga mikakati ya kuhakikikisha kuwa migogoro inamalizika, yaliyopita si ndwele tugange yajayo. Mhe. Spika, ni kwamba uchaguzi katika chama cha *ZFA* umepita lakini sasa ni vizuri tupange mikakati yakuleta maendeleo na kuinua mchezo wetu wa mpira wa miguu.

Mhe. Spika, mchezo wa mpira wa miguu unapendwa sana hapa Zanzibar nakuthibitisha hivyo ni kwamba wananchi wanapenda mpira hata Mhe. Rais wetu mpendwa ni nambari moja katika kupenda mpira. Mhe. Spika, Mhe. Rais amenunua jezi ya Timu ya Taifa ya Zanzibar kwa shilingi milioni mbili, hii ni kuonesha wazi kwamba Rais wetu anapenda michezo. Lakini mchezo huu sasa hivi unakufa kutokana na migogoro ambayo imo katika chama hicho. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba mambo ya migogoro yanamalizika katika vyama vyetu vya michezo.

Mhe. Spika, lakini michezo yetu haiwezi kwenda mbele bila ya kupata wadhamini, na kutokana na hayo migogoro na uongozi wetu tulionao hatuwezi kupata wadhamini bila ya serikali au wizara husika kukipigia kifua kuweza kupata wadhamini. Mhe. Spika, udhamini katika mipira na katika michezo mengine hivi sasa kwa sababu bila ya fedha hakuna michezo, wenzetu wa

Tanzania Bara baada ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuekeza katika michezo ndio wenzetu wameweza kupiga hatua, na tunaona mambo yao yalivyokuwa mazuri.

Mhe. Spika, mechi ya juzi ya Simba na Yanga imeingiza milioni 600, timu yetu ya hapa Zanzibar ambayo ndio ilikuwa wawakishi wa Zanzibar timu ya *Zanzibar Ocean View* siku ambayo waliocheza na timu ya Simba waliingiza shilingi milioni 200. Hii inaonesha wazi kwamba michezo inapendwa lakini bila ya wadhamini haiwezi kukua. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri apange mikakati kuhakikisha kwamba Zanzibar tunapata wadhamini katika timu zetu za taifa, za wakubwa pamoja na vijana pia na *league* yetu ya Zanzibar. Mhe. Spika, bila ya wadhamini hatutaendelea na hatutapiga hatua katika kuinua michezo yetu hususan mpira wa miguu. Mhe. Spika, "mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni".

Mhe. Spika, *ZFA* mbali na matatizo waliyonayo ya uongozi wao, lakini masikini hawana kitu ni kwamba aibu ya maiti aijuaye ni mwoshaji na mimi naijua *ZFA* vizuri. Mhe. Spika, ni kwamba *ZFA* hawana uwezo wa kuendesha timu hata kwa wiki moja, kwa sababu hawana kitu na bila ya kupata mdhamini hatuwezi kuendelea. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri Mhe. Rais wetu ni mpenzi mkubwa sana wa michezo, tumtumie Rais wetu kuweza kupata udhamini.

Mhe. Spika, jambo jengine nataka kujua Mhe. Waziri akija hapa anijuilishe, huu uanachama wa *FIFA* kweli tutaupata au hatuupati? Sio tunakaa tunazungumza tu *FIFA* je, tunataka kujua mikakati iko na matumaini yako vipi ili tujue kwamba kweli tutaupata uanachama wa *FIFA*. Namuomba sana Mhe. Waziri akija atueleze suala hili.

Mhe. Spika, vile vile nije katika Baraza letu la Michezo. Mhe. Spika, Baraza la Michezo linaongoza vyama 30 ambavyo vinatengewa shilingi milioni 140, katika milioni 140 kuna pesa za uendeshaji wa Baraza ambayo ni milioni 20 zinabaki milioni 120. Mhe. Spika, ukizigawa katika hivi vyama 30 labda utapata milioni 4. Mhe. Spika, hivyo ni chama gani kitaweza kujiendesha kwa milioni 4 hasa *ZFA* kwa sababu hivi vyama vyetu hasa kama *ZFA* sio mwanachama wa *FIFA* na wala hana ruzuku nyengine yoyote anayoipata ila ruzuku hii ya serikali kupitia Baraza la Michezo.

Mhe. Spika, hapo hapo pesa hizo zinatumika kuzisaidia vilabu vyetu ambavyo vinashiriki katika mashindano ya klabu bingwa Afrika. Mhe. Spika, vilabu vyetu vinapata shilingi milioni 10 nii kwamba vilabu vyetu ni masikini namuomba Mhe. Waziri akae afikirie milioni 10 haitoshi. Mhe. Spika, gharama za kuisafirisha timu na kuileta timu ngeni kuja hapa si zaidi ya shilingi milioni

60. Leo tunawapa milioni 10 hizo hazitoshi nimemuomba sana Mhe. Waziri aone jicho la huruma awaongeze vilabu vyetu ambavyo vinashiriki katika mashindano haya fungu kidogo japo milioni 20 au 30 ili waweze kujisaidia katika kushiriki kwenye mashindano haya na kuna fununu kwamba vilabu vyetu hivi tayari vinataka kujitoa katika mashindano kwa sababu mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nije katika sekta ya utalii. Mhe. Spika, sekta hii ni muhimu sana ambayo tunaitegemea katika kuongeza uchumi wetu wa Zanzibar. Mhe. Spika, lakini kuna mifereji ambayo inafunguka, ningemuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba mifereji ile inafungwa ili kuweza kupata fungu la kusaidia nchi yetu hii kwenda mbele. Mhe. Spika, ukenda *air port* pale mifereji iko wazi inamwagika, ukija bandarini mifereji inamwagika. Mhe. Spika, wageni wanapokuja huwa wanalipa, lakini pesa zile hazipatikani watu wanaingiza katika mifuko yao. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri aangalie sana suala hili kuhakikisha kwamba yale mapato ambayo yanapatikana katika sekta ya utalii, basi yawe yanaingia katika mifuko ya serikali ili kuweza kuinua uchumi wetu wa taifa.

Mhe. Spika, baada ya kusema haya na yote niliyoyasema lakini nina asilimia 99 asilimia 1 ni baada ya kupata majibu ya Mhe. Waziri. Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii, ahsante sana.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuleta hapa asubuhi hii tukiwa katika hali ya uzima na afya. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa na mimi fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu mdogo katika wizara hii. Pia nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na watendaji wake wote wa wizara hii, nawapongeza na nawashukuru sana.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu nianze katika ukurasa wa 17 unaoelezea Shirika la Habari. Mhe. Spika, shirika hili lina jukumu kubwa lakutuelimisha, kutuburudisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala ya kiuchumi na kisiasa. Suala la kujiuliza majukumu haya kweli yanatekelezwa ipasavyo? Mhe. Spika, maana ya kusema hivyo nianze kutoa shukurani zangu kwa jamadari wetu Rais wetu wa mwanzo Marehemu Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi kwa kutuletea hii televisheni na akiwa ana maana ya kuwa Wazanzibari tutapata maendeleo ndani yake. Mhe. Spika, niseme wakati huo TV hii basi iliwekwa katika maandalizi mazuri na vipindi vilikuwa vizuri ambavyo vikioneshwa na tulikuwa Wazanzibari sote tunafurahia.

Mhe. Spika, kulisema hilo kwanza kulikuwa na maandalizi ya vipindi vya watoto ambavyo vilikuwa vinawatenganisha kati ya watu wazima na watoto na

vikioneshwa na baadae watoto wakenda kulala. Lakini hata ikitokea athari yakuwa mtoto pengine hakwenda kulala, basi kipindi kilichokuwa kikioneshwa mbele pale ilikuwa hakina athari jinsi ya utaratibu wa kuvichunga vipindi visiathiri jamii yetu. Mhe. Spika, leo hii TV yako mwenyewe umeinunua kwa pesa zako na iko ukumbini kwako una haja ya kuangalia, basi kama pana mtu unayemstahi inakushinda inabidi uondoke uiache TV na hali unataka na wewe kufuatilia vipindi. Mhe. Spika, hili nimuombe Mhe. Waziri pamoja na mikakati yake anayopanga lakini aliangalie suala hili kwa umadhubuti mkubwa kwa sababu pamoja na hayo yote tukubali kama chombo chetu hiki nacho kimechangia kwa kiasi kikubwa mmong'onyoko wa maadili yetu.

Mhe. Spika, niende katika Kamisheni ya Utalii. Mhe. Spika, kweli sekta ya utalii ina manufaa makubwa kwetu na inaingiza fedha nyingi katika nchi yetu, lakini pia sekta hii inaleta mmong'onyoko mkubwa wa maadili yetu ikiwa hatukujipanga vizuri. Mhe. Spika, mimi leo naomba uniruhusu nimkumbuke tena jamadari wetu muasisi ambaye ni mkombozi wetu aliyetufikisha hapa Hayati Abeid Amani Karume. Niseme mzee huyu Mwenyezi Mungu alimpa kipaji na upeo wa kuona mbali.

Mhe. Spika, enzi hizo walikuwa wakija watalii basi wakifika bandarini tu pale wanapelekewa kanga na vikoi ili waweze kujistiri wasije wakaathiri mila na utamaduni wetu. Mhe. Spika, kama tunavyoelewa na wataalamu wanavyotwambia watoto ni watu wakuiga sana, alijua hicho kinaweza kutokea na watoto wanaweza wakafuata mila na utamaduni ambao sio wa kwao. Hivyo, Mhe. Spika, aliweza kuyatekeleza hayo na tukawa kwa wakati huo hatukuweza kupata athari yoyote katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hatimae hivi sasa tulivyoacha kauli na vitendo vya jemedari wetu huyu athari tumeanza kuiona katika utalii jinsi wimbi la maambukizi makubwa ya ukimwi yanavyopatikana kwa kuacha zile mila na desturi zetu, na kufuata mila za watu wengine. Mhe. Spika, sisi tuna msemo huwa tunausema ningeomba usemi huu tunaousema tusiwe tunausema na baadae ikawa hatuufuatilii kwa vitendo. Mhe. Spika, sisi tulikuwa na kawaida yakusema viongozi wetu hawa wanapofariki basi kilichokufa huwa ni kiwiliwili lakini maneno na vitendo vyao bado vipo. Mhe. Spika, laiti tungelifuata mwenendo na vitendo vya hayati Karume tusingelifikia hapa tulipofikia kwa sababu alikuwa anajali sana utamaduni wa nchi yake.

Mhe. Spika, sasa niende katika Kamisheni ya Utamaduni. Hapa ndipo penye hasara kubwa sana. Mhe. Spika, ni kwamba utamaduni wetu umekuwa ukiyoyoma siku hadi siku na hatimae vizazi vyetu sijui vitakuja kurithi kitu gani.

Mhe. Spika, nianze kwa kusema kwamba hivi sasa Zanzibar tumebadilika sana wanawake tumekuwa tukifuata mila ambazo haziendani na utamaduni wetu, tumekuwa tukivaa mavazi ambayo hayaendani na utamaduni wetu, tunavaa suruali za kiume ambapo hizi tunaelewa kama kuvaa vazi la kiume kwa mwanamke limegharamishwa na pale utakapovaa wewe suti nzuri tu ikakupendeza akitokea atakaevutiwa akimuona fulani kavaa kapendeza basi ujue kwako wewe adhabu itakuwa mara mbili zaidi.

Kwa hivyo, mimi nasema tungeweza kujiepusha na hili na wanawake wa Zanzibar mimi nichukue fursa hii niwasifie sana jinsi Mwenyezi Mungu alivyotuumba ni wazuri, tunavutia na hasa pale ambapo tunavaa yale mavazi ambayo yametokana na urithi wa mabibi zetu na mababu zetu huko nyuma. Mhe. Spika, inatakiwa wanawake lazima tujiamini kwa sababu tunapovaa nguo zetu zile ambazo zinaendana na mila zetu tunapendeza zaidi. Kwa hivyo, tusiuache utamaduni wetu ukavurugika na kutegemea kufuata utamaduni wa watu wengine hautatusaidia katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nalisema hili tena kwa kurejea kule kule kwa kukumbuka maneno na vitendo vya hayati Karume. Hayati Karume alipoona nchi yake inataka kuvurugika katika mila na utamaduni huu basi aliweza kupiga marufuku uvaaji wa nguo fupi, masuruali yale yaliyokuwa yakiitwa mabuga, kulikuwa na shati za kubana alizizuia, hii yote alikuwa akifanya kwa sababu utamaduni wa nchi hii usipotee. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nimuombe Mhe. Waziri wanaume wakati ule walikuwa wakifuga machwele makubwa na pia alitaka ayakate. Wanaume waliweza kukatishwa nywele wakati ule ili na nadhani alichelea mtindo huu ambao uko hivi sasa.

Mhe. Spika, hivi sasa wanaume wanasuka, wanaume wanatia hereni, wanaume wanavaa vidani ambayo hii sio mila na utamaduni wetu. Mhe. Spika, hiki ni kilio kikubwa kwetu na ni hasara kwa taifa letu huwezi kumbagua kati ya mwanamme na mwanammke hivi sasa. Mhe. Spika, hiki ni kilio kikubwa na tunapaswa Wazanzibari tulizingatie hili tumefika pahala ambapo tunapokwenda siko, hivyo turudi nyuma na tuuendeleze utamaduni na mila yetu ambacho hicho ndio kitakuwa ndio kigezo kikubwa kwa watoto wetu na wajukuu zetu waje kufuata mila zetu.

Mhe. Spika, Mhe. Karume alipiga marufuku kwa kuona wale wenye nywele kubwa alihofia huu usukaji huenda ikawa usiku wanasuka pengine asubuhi wanachana na alijua tendo hilo sio zuri kwetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nimuombe Mhe. Waziri hili aweze kulitilia mkazo hasa ili liachwe na lisiendelezwe. Mhe. Spika, mimi ilikuwa shida yangu nimuombe Mhe. Waziri akija hapa anieleze kuna suala moja ambalo linanitatiza na mimi kidogo kuhusu watu wa habari wale wa vipaza sauti.

Mhe. Spika, nimeona wakati mwengine huwa wanachelewa katika *function* pengine Mhe. Rais ana *function* pahala huona wanachelewa, hili nilitaka kujua ni kwa sababu gani wanachelewa ama ni uzembe wa wafanyakazi au ni vitendea kazi vimekuwa pungufu kwao. Hili Mhe. Waziri atakapokuja hapa angelitueleza kwa sababu linaathiri kuona viongozi wetu wameshafika pale na ndio harakati zinaanza sasa. Mhe. Spika, mimi mchango wangu hapa ulikuwa ni mdogo na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini basi naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Spika, nianze kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa baraka zangu katika wizara hii muhimu. Kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kutokana na kuteuliwa kwake kushika nafasi hii. Pili nimpongeze Al-hajat mtarajiwa Mhe. Bihindi Hamad Khamis na yeye kwa kuteuliwa kumsaidia Mhe. Waziri katika kulitekeleza jukumu hili na kuisimamia wizara hii.

Mhe. Spika, naomba nianze tena na pongezi zangu kwa kuipongeza wizara jinsi walivyokazana katika kuwasomesha wafanyakazi wake. Ni ukweli kwamba ukikiangalia kitabu hiki kwenye viambatanisho utaona kwamba wizara nathubutu kusema kuwa ni ya kwanza kwa kuwasomesha wafanyakazi wake. Hii inatupa matumaini makubwa kwamba katika kipindi kifupi kijacho wizara hii itakuwa ina wataalamu katika kila fani ndani ya wizara hii.

Mhe. Spika, baada ya pongezi sasa naomba nitaje hili pungufu la kibajeti na naomba nitoe ushauri sio kwa wizara tu, lakini kwa serikali nzima katika uandaaji wao wa bajeti. Mhe. Spika, naishauri serikali wakati wanapoandaa bajeti iwe na *format* moja kwa sababu wizara nyengine zinapoleta bajeti zao hutueleza kabla fedha walizoziomba mwaka jana, fedha walizoingiziwa mwaka jana na fedha wanazoziomba mwaka huu.

Mhe. Spika, wizara nyengine huwa zinafanya hivyo lakini wizara nyengine hazifanyi hivyo, hutwambia tu waliomba kiasi gani bila ya kutueleza wameingiziwa kiasi gani na matokeo yake huja kutwambia mara hii na mimi nategemea kuomba kiasi fulani. Mhe. Spika, hii haitupi kipimo kizuri sisi kama wawakilishi kuweza kuona utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana ili tuwe na uwezo sasa wa kuangalia hicho wanachokiomba katika bajeti hii. Hicho ni kipimo kizuri sana kinachoweza kutufanya wawakilishi tuwe na mizani ya kupima utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana. Kwa hivyo, naomba wizara zote ziwe na *format* moja katika uandaaji wa bajeti.

Mhe. Spika, umuhimu wa sekta hii ya habari, utamaduni, utalii na michezo ni muhimu sana kwa sababu habari kama ilivyoelezwa kazi yake kubwa ni

kuelimisha, kupasha habari, kuburudisha kwa mambo yanayohusiana na kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kwa hivyo, ili jamii iweze kujua kinachoendelea hutegemea sana na uwepo wa sekta ya habari katika nchi. Lakini vile vile utamaduni Mhe. Spika, imeeleza kwamba utamaduni ndio kielelezo cha utaifa, mataifa yote hutofautiana baina ya taifa moja na jengine kutokana na mambo ya utamaduni. Mhe. Spika, mtu yeyote anapokwenda katika taifa moja ama jengine hulazimika kwanza kuangalia utamaduni wa taifa linalohusika.

Kwa hivyo, utamaduni ndio kielelezo na utamaduni wetu Wazanzibari ndio kielelezo cha taifa letu la Zanzibar, kama hatukutilia maanani au hatukuzingatia mambo ya utamaduni hiki tunachokipigania kwamba Zanzibar ni nchi au sio nchi, huu utaifa wetu kielelezo cha kwanza cha utaifa wetu pamoja na mambo mengine lakini itategemeana sana na kuwepo utamaduni wa Mzanzibari katika hili. Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa utalii ni moja kati ya sekta ya uchumi na kwa sasa kama inavyoelezwa utalii ndio tegemeo la uchumi wetu. Kwa hivyo, utalii kuwepo katika wizara hii tunategemea kwamba utaleta faraja na matumaini katika uendelezaji wa uchumi wetu.

Mhe. Spika, lakini michezo kama ilivyoelezwa na wenzangu hapa ni kwamba inahusiana na uchumi wa mtu mmoja mmoja mpaka kwa jamii. Lakini vile vile michezo sasa hivi ni utambulisho wa taifa, mataifa mengi yanajuulikana kutokana na michezo na unapotaja mchezo fulani basi moja kwa moja akili yako inakulenga kulitambua taifa fulani. Kwa hivyo, na michezo nayo ina umuhimu mkubwa sana katika utambulisho wa taifa. Mhe. Spika, kwa hiyo kwa ujumla wake wizara hii ni muhimu sana katika maendeleo ya uchumi, maendeleo ya kijamii na utengamano wa siasa katika maisha ya kijamii.

Mhe. Spika, leo naomba nianze kwa kuchangia kwa njia ya kuuliza uliza masuala kuliko kuzungumza. Naomba nianze na Idara ya Uendeshaji na Utumishi hii inahusika sana na suala la maslahi kwa wafanyakazi. Mhe. Spika, idara hii kwa kweli wafanyakazi wake wanafanyakazi katika mazingira mazito sana, ni tofauti na sekta nyengine za umma wakati mwingi watumishi katika sekta hii kweli hufanya kazi mpaka wakati wa usiku, ama hulazimika kwenda kazini muda sio ule wa kawaida kwa sababu vipindi vinaanza kuwekwa alfajiri. Kwa hivyo, hulazimika kuingia kazini nyakati za alfajiri.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huo basi ni suala zima la wizara ama suala zima la idara kuangalia maslahi na kuboresha maslahi ya wafanyakazi wake. Kwa mfano, mzuri Mhe. Spika, katika Baraza hili wawakilishi tangu tunapoanza kukaa kitako katika viti vyetu tunao wafanyakazi hapa, na wao tofauti na sisi, sisi tunakaa kitako lakini wengine wanasimama na husimama kuanzia saa moja za asubuhi mpaka saa saba na husimama kuanzia saa kumi na moja mpaka saa mbili za usiku. Mhe. Spika, wakati mwengine ukiwaangalia kwa kweli ile

kusimama wanachoka utawaona wanainama. Kwa hivyo, Mhe. Waziri katika bajeti ya mwaka jana, mwaka juzi tulikuwa tunazungumza sana na Mhe. Shamuhuna katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi wake hawa. Mhe. Spika, taarifa tulizonazo eti tunaambiwa wanalipwa posho la shilingi 2000 kwa siku, na hizo sijui mpaka wasubiri bajeti ya mwaka mwengine ndio walipwe posho zao hizo.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri katika utekelezaji wa agizo lile tulilompa Mhe. Waziri aliyetangulia hebu tueleze maslahi na posho za watendaji hawa kwa sababu na wao ni wanadamu na wana familia na wanafanyakazi ngumu sana. Mhe. Waziri utakapokuja hapa Mhe. Waziri tueleze katika hilo ni kiasi gani wanapata na ni kweli wanalipwa hawa. Mhe. Spika, bahati mbaya utakaporuhusu watendaji kama ambavyo wawakilishi tunakuwa na kanuni maalum ya kuruhusu mavazi na wao vile vile inawabana hiyo kwa sababu huwa wanaingia ndani ya ukumbi huu na wao wanahitajika kuwa na suti. Lakini taarifa nilizozipata kwamba hizo suti huwa wanaazima, hivyo wafanyakazi hawa maana yake haipendezi hata siku moja kwamba na hili ndilo tunalolipigania.

Mhe. Ismail Jussa kazungumza hapa *appearance* ya watangazaji wetu itofautike na wachuuzi sokoni, ile *appearance* ina-*matter* katika utangazaji. Hivi Mhe. Spika, Mhe. Waziri naomba nimuulize huwa kuna posho maalum la kununulia kivazi? Kwa sababu ikiwa wanatakiwa wajitegemee kutokana na wanachokipata katika mshahara wao itakuwa hatuwatendei haki, hilo hatuwatendei haki hata siku moja, tunachotegemea hawa wapewe posho maalum kwa ajili ya mambo ya mavazi, wapewe posho maalum wale wasichana kujirembaremba, kwa sababu lazima ukikaa pale katika televisheni uonekane *appearance* yako iwe nzuri. Sasa kama hatuwapi itakuwa hatuwafanyii haki na ndio kile kinachowatosha watazamaji wa televisheni yetu wakaangalia kwenye televisheni nyengine.

Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja katika hili aweze kutueleza hilo ili na sisi tujue namna ya kumsaidia kama mafungu yake hayatoshi tuangalie tubane pahala, kuna sehemu zinatengewa huko sijui mbwa wapandishwe na nini, tunaweza tukachukua kule.

Mhe. Spika, nije sasa katika Shirika la Utangazaji. Hizi hadithi za kuwa na Shirika la Utangazaji zimeanza kusikilikana katika kipindi cha miaka ya karibuni. Mimi binafsi nilikuwa najiuliza lini sheria hii ilikuja katika Baraza la Wawakilishi? Lini tulikaa Barazani kuipitisha hii? Ingawa sheria Nam. 4 ya mwaka 2002 ya *Public Investment Act* inauruhusu serikali kuweza kuunda shirika, na nadhani serikali itakuwa imepitia huko kuunda shirika bila ya kuleta sheria, lakini Mhe. Spika, kama hivyo ndivyo itakuwaje tuwe na shirika ambalo

hatujaliundia sheria. Na kama hivyo ndivyo hatuoni kwamba tutakuwa tunarudia yale yale makosa ambayo mara nyingi huwa tunayakataza. Kwa hivyo, hilo naomba lipate maelezo na Mhe. Waziri atapokuja anieleze shirika hili lipo kisheria au halipo kisheria.

Mhe. Spika, katika kazi ya shirika hili ni kuwa na programu ya kuelimisha. Mhe. Spika, katika nchi yetu katika miaka miwili tuliyonayo hii kuna kitu kizito sana kimetokea na ni muhimu sana kwa taifa letu. Suala la Serikali ya Umoja wa Kitaifa na suala zima la umoja wetu wa kitaifa tulionao Zanzibari. Siubishi kwamba katika kipindi cha miaka mingi iliyopita Zanzibar ilikuwa ikisemekana vibaya kwa sababu tulikuwa tuna matatizo makubwa sana ya migogoro ya kisiasa. Leo Mwenyezi Mungu katuletea heri kubwa sana, tunamshukuru sana Dkt. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad kwa kulianzisha hili na leo tukawa tunafaidi, kilichopo hapa leo Mhe. Spika, tunafaidi matunda ya kazi yao viongozi wetu waliyotufanyia.

Sasa hili tunategemea liendelee miaka nenda miaka rudi umoja huu usivunjike. Jambo ili iliendelee umoja huu uendelee kudumu maana yake lazima kuwe na mprogramu maalum ya kuelimisha jamii umuhimu wa suala hili la Umoja wa Kitaifa.

Lakini Mhe. Spika, katika kitabu cha Mhe. Waziri idara zake nyingi zinajishughulisha na mambo ya elimu ya UKIMWI, maana yake sasa nahofia badala ya kwamba tuna kitendo maalum cha UKIMWI na hiki nacho kitakuwa ni kitengo (B) cha UKIMWI hii wizara. Kwa nini wizara haifikirii kuanzisha programu ya kuendelea kuelimisha juu ya umuhimu wa umoja wetu. Kwa sababu sina hata pahala pamoja ndani ya hotuba yote nililoliona hili kwamba likitiliwa mkazo katika idara yoyote ile kuwa kuna programu iliyoandaliwa ya kuelimisha juu ya umoja wetu huu tulionao.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri aje anifafanulie hili kaliweka pahala gani, suala la kuandaa programu ya kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutunza na kuendeleza umoja wa taifa letu.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, naomba niende sasa katika Idara ya Habari Maelezo ambayo imetwambia moja katika kazi yake ni kuuza picha za Mhe. Rais, imeuza picha nyingi za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano na picha 980 za Rais wa Zanzibar. Suala langu liko katika picha za Rais wa Zanzibar. Mhe. Spika, katika taifa lolote au kimataifa picha ya Rais wa Zanzibar huwa inatakiwa iwe na hatimiliki, picha ya Rais wa Zanzibar itofautiane na picha yangu mimi ambayo unaweza ukaiokota okota tu pahala popote pale ukaichapisha. Sasa naomba niulize Idara ya Habari Maelezo je, serikali inayo hatimiliki ya picha ya rais?

Kwa sababu taarifa tulizonazo kwamba serikali haina hatimiliki ya picha ya rais, sasa hapa ndio pahala pake Mhe. Waziri kuja kututoa wasiwasi kwamba kuna raia mmoja wa kigeni ndiye mwenye hatimiliki ya picha ya rais. Hapa sasa tunataka kujua hilo ni kweli na kama sikweli itabidi tuzungumze vyengine. Kwa sababu tuna hofu ikiwa picha hii ina mtu binafsi anaweza kwa kweli picha hii akaifanya anavyotaka yeye mwenyewe, akaitolesha vikatuni akamkashifu rais wetu kitu ambacho kama wawakilishi hatutolikubali hili tunahitaji tuione picha ya rais ikiwa na hatimiliki inayomilikiwa na serikali wenyewe ili kuondosha lile tatizo la picha ya rais kutumika katika mambo ya vikatuni na vitu vyengine ambavyo havistahiki.

Mhe. Spika, nije sasa kwenye Shirika la Magazeti. Niipongeze wizara, nilipongeze pia Baraza la Wawakilishi kupitisha sheria hii ya kuunda Shirika la Magazeti. Ni kweli kwamba sasa hivi Gazeti la Zanzibar Leo linauzika, mimi nilikuwa sitaki hata kuliona lakini sasa katika gazeti siku hadi siku lazima nipate nakla ya gazeti ni Gazeti la Zanzibar Leo. Ni gazeti ambalo liko sokoni sasa na lina ushindani mkubwa sana, ukichelewa ikifika kiasi cha saa saba gazeti hilo hulikuti tena sokoni. Kwa hivyo, tunapongeza na tunataka liendelee.

Lakini hoja yangu Mhe. Spika, uwezo sasa wa shirika namna ya kulichapisha gazeti. Shirika lina uwezo gani katika kuzalisha gazeti. Kwa sababu jana nilishituka kuambiwa kwamba gazeti fikira yangu kwamba siku zote gazeti linazalishwa Zanzibar, lakini kumbe gazeti mpaka livuke maji ndio lizalishwe, hii ni hatari. Na hivyo sivyo tulivyokubaliana, tulikubaliana kwamba serikali iwezeshe shirika ili liwe na uwezo wa kuzalisha gazeti hapa, leo ikiwa gazeti letu hapa mpaka litoke Dar es Salaam asubuhi mtu wa Dar es Salaam alisome kulikoni sisi wenyewe hapa hatuna uwezo wa kulisoma mpaka tusubiri boti lije, kwa kweli hilo ni kinyume na lengo la kuliundia shirika hili.

Mhe. Spika, taarifa tulizonazo kwamba gazeti hili kwa siku linagharimu si chini ya shilingi laki tano katika uchapishaji wake maana kwamba hatuna mitambo ya kuchapisha. Mpango huu tulipofuatilia tumeambiwa kwamba hauzidi shilingi milioni mia nane, ikiwa hivyo ndivyo Mhe. Spika, serikali inashindwa kutoa shilingi milioni mia nane kupata mtambo huu. Kwa sababu hesabu ukizipiga hapa utakuta sasa ikiwa ni kweli kwamba kwa siku shirika linatoa shilingi laki tano kwa ajili ya uchapishaji kwa mwezi maana yake ni shilingi 15 milioni, kwa mwaka ni shilingi 180. Sasa hizo tunazitoa fedha hizo kwa ajili ya kwenda kuwafaidisha wenye viwanda Dar es Salaam, wakati kumbe ilikuwa tutoe shilingi milioni mia nane mara moja faida hiyo tuendelee kuifaidi sisi wenyewe na kuchapisha gazeti. Hofu yangu katika hilo ni kwamba kwa mtindo huu gazeti hili hatuwezi ku-*sustain* katika soko.

Moja wakati nachangia hotuba ya serikali nilimshauri Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba kama Baraza hatutoruhusu tena kwa mashirika yanayoweza kujiendesha kuendelea kuyapa ruzuku, hatutoweza tena kuendelea kufanya hivyo. Kila aliyepewa mamlaka maana yake aweze kusimama kwa miguuu yake, hawezi kusimama kwa miguu yake akatafute makoongo akapige huko, tutaendelea kutoa ruzuku kwa sababu maalum katika mashirika maalum, lakini Shirika la Magazeti linaonekana kwamba lina uwezo isipokluwa ni tatizo dogo. Tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje atueleze hili kwa sababu tatizo letu tunavyoliona katika hili kama tutaendelea na utaratibu huu wa kutegemea wachapishaji kutoka Dar es Salaam gazeti hili litakuwa ni kwa kipindi kifupi na halitoweza ku-*sustain* katika soko hili la biashara ya magazeti.

Mhe. Spika, niende kwenye michezo. Michezo kama nilivyotangulia kusema na mwenzangu mtaalamu wetu hapa, kocha wetu Mhe. Nassor Salim Ali, michezo ni uchumi lakini vile vile ni utambulisho. Sasa hivi nikitaja mpira wa miguu kila mmoja nikitaja Brazil atajua nazungumzia kitu gani, lakini nikizungumzia *cricket* kila mmoja atafikiria taifa fulani, India, Wahindi hao. Nikizungumzia Marathon bbasi akili za kila mmoja zitazungumzia twende Eritrea, Ethiopia mpaka Kenya. Kwa sababu tunapotaja mchezo basi moja kwa moja ina-*reflect* utambulisho wa taifa fulani.

Mhe. Spika, lazima tufike pahala michezo yetu tukubaliane kwamba michezo imekufa na sasa serikali inahitaji juhudi maalum si suala la kunyanyua michezo tu, lakini tunahitaji tuwena mchezo ambao utaitambulisha taifa letu la Zanzibar, mimi sijui ni mchezo gani, sijui kama ni Kiumbizi au Kuogelea au vipi, lakini wakati umefika sasa tutafute mchezo mmoja ambao serikali uuendeleze ili tufike pahala ionekane kwamba mchezo huu ndio nembo ya Zanzibar kimataifa.

Mimi sidhani kwamba tunaweza tukafika pahala tukaendeleza soka mpaka soka ikawa ndio utambulisho wa Zanzibar hatuwezi tukafikia hatua hiyo. Tuendeleze kwa sababu ndio hali halisi ilivyo kwamba ndio mchezo unaopendwa, lakini pamoja na kuweza kui-*boost* michezo hii, lakini lazima serikali itafute mchezo mmoja uwe ndio nembo yetu na utambulisho wetu kimataifa, ushauri wangu ni huo.

Katika hilo niungane na Mhe. Nassor Salim Ali Uwanja wa Gombani haukuzungumzwa na tuliambiwa kuna uwekaji wa taa zile, uwekaji wa kapeti, lakini hatukuambiwa ni namna gani sasa hivi hatua imefikia. Namuomba Mhe. Waziri kwa faidai yetu atakapokuja atwambie hali ya Uwanja wa Gombani na hasa kwa kujua kwamba kuna kiwanja pembeni pale ambacho tuliambiwa itajengwa hoteli kubwa na ya kisasa, ile hatua imefikia wapi. Kwa sababu

tulikwenda wakati niko kwenye Kamati ya Ustawi wa Jamii kukipapatua kiwanja kile ambacho ilikuwa tayari kishajengwa. Sasa kama ikiwa hadithi zake kiwanja kile hazitoletwa hapa mimi nina hofu huenda wajanja wakarudi tena kile kiwanja wakakichukua. Mhe. Spika, naomba atakapokuja Mhe. Waziri atupe maelezo.

Na la mwisho katika suala la michezo nimuombe Mhe. Waziri, hii migogoro iliyotajwa na Mhe. Nassor ambayo kila mmoja anaifahamu tufike pahala serikali iingilie kati migogoro hii. Kwa sababu serikali inaendeshwa na sera na sera ni za serikali, ikiwa michezo hii inaharibika ni jukumu la serikali kuona kwamba sera zake haziendi kombo. Sasa ikiwa kuna matatizo ya *ZFA*, ikiwa kuna matatizo katika chama fulani mambo yasibakie mpaka yakaharibika yakafika kwenye mahkama serikali iingilie kati i-*rescue* mambo kama hayo. Kwa sababu sera hizi za michezo ni sera za serikali.

Mhe. Spika, baada ya ushauri huo mwisho kabisa naomba nimalizie Hoteli ya Bwawani na katika hoteli hii naomba nimtakie malazi mema Sheikh Abeid Aman Karume. Inasikitisha sana kwamba kila tunapokwenda mambo yote yaliyoanzishwa kila jambo linakwenda arijojo. Moja katika jambo zuri alilolianzisha nio hili la Hoteli ya Bwawani. Kwa kweli licha ya kumfumka mahoteli mengi lakini bado Hoteli ya Bwawani hadi sasa ina soko, ni kubwa, hoteli hii kwa kweli yule mzee alikuwa na *vision* kubwa sana, maana yake kwa miaka hiyo kujenga hoteli kama ile ambayo mpaka leo mimi nasema katika mji huu wa Unguja inachukua nambari, ina kumbi na hoteli yenyewe pamoja na mambo mengine mengi ambayo hadi leo kwa kweli soko lake ni zuri, lakini tumeiachia hoteli ile imekuwa katika hali kama ilivyo ni kitu cha kusikitisha.

Bado mimi nasema naishauri serikali itafute namna ya kuiendeleza Hoteli ya Bwawani. Hoteli ya Bwawani ilivyo sasa ni chaka tu la baadhi ya watu kwenda kufanya mambo wanayotaka wenyewe. Hoteli haijiendeshi na ni mzigo kwa serikali, sijui hii hesabu ni ya mwaka gani kwamba hoteli kwa mwaka huu imeajiri watu 135, imeajiri katika kiambatanisho hapa sijui ni kwa mwaka huu au ndio wafanyakazi wote. Lakini kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo hapa na uajiri mwengine inaonekana kwamba ni kwa mwaka mmoja. Kwa sababu idara nyengine katika kiambatanisho hiki hiki kwamba imeajiri mtu mmoja au wawili kwa hivyo, kwa namba hiyo inaonekana hii ni kwa mwaka mmoja.

Mhe. Spika, Hoteli ya Bwawani ni mzigo mkubwa kwa serikali na lazima serikali ifike pahala sasa iamue hoteli ile ama ku-*invest* wenywewe serikali au ifike pahala itafutiwe mwekezaji ili hoteli ile iendelee, lakini haiwezi hoteli ile kuendelea, siku zote tutakuja kugombana na tutagombana kikweli kweli. Kwa sababu  kwa mambo yanayoendelea katika hoteli ile Mhe. Waziri kwa kweli

hapa tutaleta hoja binafsi katika suala la Hoteli ya Bwawani. Kwa sababu inakuwa ni mzigo mkubwa sana wa serikali.

Moja kati ya kitu ambacho nasema kuwa hoteli ile isipewe ruzuku ina uwezo wa kujiendesha na lazima ijiendeshe. Mimi binafsi nazuia ruzuku ya hoteli ile hadi tutakapopata maelezo kamili. Hoteli ina uwezo mkubwa sana wa kujiendesha na lazima ijiendeshe wenyewe, kama haiwezi kujiendesha basi tutafute mwekezaji na tumeshatafuta wawekezaji wengi tu katika maeneo mengi na Hoteli ya Bwawani iwe ni sehemu moja ya kufanya hivyo.

Baada ya hapo Mhe. Spika, kwa sababu leo nilisema nichangie lakini kwa njia hii ya kuuliza maswali mara nyingi nikitaraji kwamba Mhe. Waziri atakuja kunijibu maswali yangu haya ili baadae nami niungane na wenzangu kuunga mkono. Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi kuweza kuchangia mchango wangu mdogo kuhusiana na bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Kwanza namshukuru Allah kutupa uhai na uzima na tukafikia hapa.

Mhe. Spika, suala la mwanzo kwa kuwa kuna Ofisi Kuu Pemba nimeshitushwa kidogo na maelezo yaliyotolewa humu, inavyofahamika Wakurugenzi wnaoteuliwa wanateuliwa wakiwa ni Wanzanzibari. Kwa hivyo, ikiwa kuna idara ina maana idara ile iwe ina-*cover* Unguja na Pemba, inakusanya baina ya Unguja na Pemba. Sasa unapoiona shughuli ya linaloitwa Shirika la Utangazaji kuhusu mambo ya redio ukaambiwa yamefanywa na Ofisi Kuu Pemba unajiuliza lile shirika linafanya nini sasa.

Mfano Mhe. Spika, katika kuelezewa bajeti ya Ofisi Kuu Pemba katika ukurasa wa 13, maelezo yake yameanza ukurasa wa 12, lakini katika ukurasa wa 13 utekelezaji halisi kifungu nambari 23(i) “Ofisi imefanikiwa kufunga mtambo mpya wa FM wenye uwezo wa 2KW” na kuendelea mbele kama ilivyo. Mimi nilipoisoma kwanza nilikuwa sikufahamu nikaona hii ofisi imefungiwa mtambo sasa hivi wa mawasiliano, lakini baadae nikagundua kwamba ni mtambo wa kurushia matangazo ya Sauti ya Tanzania Zanzibar. Sasa ndio nikajiuliza kwamba kunapita nini hapa? Tunavyojua sisi kwamba shirika lile likitajwa kwamba la Zanzibar ina maana ni Unguja na Pemba, Ofisi ya Pemba ni ofisi ya *co-ordination* ya kuratibu zile shughuli zote zilizomo katika ofisi ile. Sasa unapoifanya kwamba yeye ndio *responsible* na nafikiri ndio maana mpaka leo watu wa *TVZ* hawajaweka mitambo yao kule Pemba kwa sababu wanaingoja Ofisi Kuu ya Pemba ifanye na hali mambo hayajafanywa hapa.

Kwa hivyo, hebu Mhe. Waziri tueleze kumetokea mabadiliko gani ya kiuendeshaji hata kifungu hiki kikawekwa chini ya Ofisi Kuu Pemba wakati kilikuwa moja kwa moja kishughulikiwa na idara yenyewe ya Sauti ya Tanzanzia Zanzibar. Kwa sababu tukisema Sauti ya Tanzania Zanzibar ni mambo yote yanayohusu baina ya Unguja na Pemba. Ofisi ya Pemba ni ofisi ya uratibu na Mkurugenzi anapoteuliwa anateuliwa kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, hilo nalitaja kama moja lakini kama yako mengine zaidi ya hayo basi naomba tupate maelezo.

Mhe. Spika, baada ya hapo kidogo nimuulize tena Mhe. Waziri, kuna tabu yoyote anayoipata au kuunganisha baina ya hizi sekta alizokabidhiwa? Kuna sekta moja kubwa ya huduma ambayo inahusiana na habari, utamaduni na michezo; lakini kuna sekta nyengine zaidi ni huduma pamoja na uzalishaji (Sekta ya Utalii). Je, kuna matatizo yoyote ambayo yanakumbana kwa kuziunganisha sekta mbili hizi? Kwa sababu huko nyuma tumezowea kwamba utalii uliwekwa kwenye Sekta ya Kibiashara na hii ilikuwa ni sekta kiongozi, sasa mimi nina wasiwasi kwamba huwenda sekta moja ikakosa huduma ya kutosha ama Waheshimiwa wakubwa wakenda kule kwenye uzalishaji huku kwenye huduma wakakuacha au kwa sababu sekta hii ni kubwa kule wakakuacha. Sasa hebu tuelezeni kwa sekta kama hii zinapambana vipi ili zote zihudumiwe sawa sawa?

Mhe. Spika, tunacho Chuo chetu cha Uandishi wa Habari, taarifa ambazo tunazipata zenye usahihi kwa kiasi fulani ni kwamba wale vijana wanaotoka katika wizara na kwenda pale huwa mara nyingi wanasitishwa masomo yao, kwa sababu ya kutolipiwa na matokeo yake wao kile chuo kinatawaliwa zaidi na vijana au wanafunzo wanaotoka katika sekta binafsi. Hebu Mhe. Waziri uje utueleze hawapati bajeti hawa au inakuwaje kukwama kwamba wao hawalipiwi na baadae wanasitishwa masomo yao.

Lakini suala jengine ni kwamba ndani ya mpango wa wizara kuna utaratibu gani wa kuwasomesha vijana wake ili kuweza kumudu yale mambo ambayo wanakabidhiwa. Kwa sababu katika utaratibu ulioko huku katika jadweli zilizoko mwisho wa kitabu mimi nimepekua sana sikuona pahala ambapo pameandikwa kuwa kuna vijana wako masomoni kadhaa wa kadhaa, labda ilikuwa ghafla ghafla lakini sikuona. Kama ipo naomba radhi, lakini kama haipo namuomba Mhe. Waziri aje atueleze namna gani wanavyowapeleka vijana kusoma katika maeneo mbali mbali ya wizara hii.

Mhe. Spika, tuna Televisheni Zanzibar na Sauti ya Tanzania Zanzibar, kama nilivyosema kwamba namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kusema kwamba kunafungwa mtambo mpya na Sauti ya Tanzania Zanzibar sasa hivi inasikika kupitia *FM*. Hilo lazima tumshukuru na tumpongeze kwa kufikia hatua hiyo.

Lakini bado wananchi wa Pemba wanalia na TV, wengine wao ambao mawasiliano mengine hawayapati kwa kupitia zile antenna zao televisheni zao wamezifunga kabisa. Kwa sababu mpaka uwe na dishi waliokuwa hawana madishi ni wale karibu na pwani sana huko kama Mkoani au wapi ndio hunasa nasa, lakini wengi wao hawapati matangazo yoyote.

Sasa tunamuomba Mhe. Waziri kwa sababu hiyo mitambo ishafika sasa, hebu aje atupe katika maelezo yake tarehe hasa ya kwamba wananchi wetu sasa wataona *TVZ*. Kwa sababu tangu mwaka huu ulipoanza tunaambiwa Machi, April, Juni, Julai, mimi sitaki kuingia hiyo mitambo ilivyokwama aa, ishakwama imeshakwamuka hebu tupe tarehe sasa Mhe. Waziri ni lini hasa wananchi wa Pemba wataona haya matangazo ya TV? Kama hiyo mitambo hairuhusu tena kuona kwa Zanzibar basi ifungwe vianzishwe pale pale vipindi vya televisheni Pemba na tuna uhakika kwamba studio ipo na vipindi vinaweza kuoneshwa sio lazima itoke huku moja kwa moja.

Lakini Mhe. Spika, mimi nasema kwamba Mhe. Waziri namuomba sana awape taaluma za kutosha waongozaji wa vipindi. Mimi pengine siwezi nikawalaumu sijui taaluma gani waliokwishapewa, kwa sababu mimi bahati mbaya siwajui na sijawahi kubahatika kwenda katika kamati kwenye eneo hilo. Lakini Mhe. Spika, kuna msemo wa Kiarabu unasema *"Likulli makani, makkal".* Kila pahapa pana msemo wake, pana maneno yake na hivi vipindi vya TV kila wakati kuna mambo yake ya kuonesha.

Ukitaka kumsomesha mtu kuna wakati wake wa kumsomesha na ukitaka kumburudisha mtu kuna muda wake wa kumburudisha, ukiviparaganya wakati wa burudani ukaweka elimu watu hawatokufahamu na wakati wa elimu ukaweka burudani nalo watu hawatakufahamu. Hebu tuvipangeni hivi vipindi vyetu, ikiwa bado hatujapata taaluma ya kutosha hebu tukawape hawa wataalamu wetu taaluma ya kutosha ya kuvipanga hivi vipindi ili kila wakati uendane na vipindi vyake. Kwa sababu saa kumi na moja jioni utasikia pachanga limekata maji kwa lugha ya sasa linaitwa disko, lakini zamani lilikuwa linaitwa pachanga. Lugha ya sasa inaitwa disko, Bongo flavor, sijui nini yote utakayosema hayo hayo tu, lakini saa nne ya usiku wanasomesha, sasa ee saa nne atakaekusikia nani kusomesha kwako.

Kwa hivyo, mimi naomba sana *TVZ* kuna vipindi vingi sasa hivi vya kisayansi na teknolojia, ambapo TV zote za dunia zinatoa, lakini *TVZ* huoni. Hivi kwa nini hatuvipati sisi na hivi ni vya bure, teknolojia ilivyo, mambo ya kuelezea maradhi, mambo mengi tu ambayo yanafaida sisi hatuoni, akitoka huyu analetwa huyu. Lakini na watangazaji wenyewe pamoja na hao watangazaji wa vyombo binafsi ambavyo sisi tunatoa leseni, zile lugha wanazozitumia hebu tuzitazame zinalingana na vile vipindi wanavyoviendesha. Sasa ndio hapo

unapoingia hizo Bodi za Sensa ina maana ziweze kufanya kazi katika nyakati zote. Mmoja katika aliyekuwa akinipa mfano wa hili katika hizi redio za FM zilizoingia huwa wanapiga simu. Anamuuliza wewe uko wapi, niko nyumbani, uko na nani, na mke wangu, mnafanya nini saa hizi. Sasa kwa kweli hiyo inalingana. Kwa hivyo Mhe. Spika, lugha kama hizi hazilingani na utamaduni wetu wa Zanzibar, tutazame hizi lugha zinavyotoka na tuwaambie.

Mhe. Spika, nizungumzie suala michezo. Mhe. Spika, Zanzibar inakwenda mbele ikirudi nyuma. Kwanza nawaunga mkono wote ambao walisema michezo imekufa. Mhe. Spika, miaka mitano iliyopita kila mwaka ikija bajeti tunaelezwa kuhusu *academia* ya michezo, lakini mwaka huu hata kutajwa haikutajwa tena, imekwenda wapi ile. Mimi nilikuwa nikinyamaza kimya kwa sababu inataka kujengwa Mkokotoni nikajua kuwa japo Tumbe itajengwa siku moja, lakini sikuisikia japo Ziwani itakuwepo siku moja. Sasa nikiingoja hii ya Mkokotoni ijengwe nije niseme na sisi mkatujengee kule. Lakini la kusikitisha hata hii ya Mkokotoni haitajwi tena ile *academia* ya michezo imekwenda wapi.

Sasa hii michezo itakuwa vipi ikiwa hatuna hata nyenzo za kufanyia ile michezo. Siku moja nilisema humu lakini nikaonekana kwamba labda nilifanya masihara. Nasema hii michezo tunayocheza hapa tukenda kule nje tunaonekana kama Hagul Kafi, yaani tuliolala miaka 300 tukaja tukaamka halafu ndio tukenda tukaonesha michezo yetu. Kwa sababu watu siku hizi katika ile *swimming pool* wanataka kupiga ile zamani tukiita kachumbe *(head first),* basi unageuka juu mara nne tano kwanza ndio unafika kule huko huko juu ya hewa, sisi unataka kwenda moja kwa moja tu.

Mhe. Spika, ni lazima tufanye kazi ya ziada kuona tunaanza wapi ili na sisi angalau tuwemo. Hao waendesha pikipiki hapa wanakuja kujiumiza tu, watu wanageuka mara tano sita juu ya hewa na pikipiki yake halafu ndio anatua chini. Mhe. Spika, naomba sana suala la michezo na ndipo tuliposema mambo yote haya hayafanyiki ndani ya umaskini. Wewe ukisikia mchezo basi ujue mtu ameshashiba, hakuna mchezo na njaa, tokea hiyo zamani ya mabibi na mababu zetu wakishashiba ndio wanakwenda kwenye michezo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ihimizeni hii serikali tuchimbe mafuta tusiyatazame tu na mambo ndio haya yanatupita sasa duniani, kila kitu kina wakati wake ukishafika kitumiwe. Kwa sababu nyumbani tuseme huna fedha unangojea mwisho wa mwezi ili ukanunue vile vitu unavyovihitaji. Lakini watu wanatazama mwisho wa mwezi umeshafika mbona hakiji kitu hawatokuuliza, mwisho wa mwezi umeshafika mbona ndani hamna kitu. Sasa na sisi kila tukija tutauliza serikali unaona mambo haya michezo inakufa, kila kitu kinakufa, kwa kuwa rasilimali Mwenyezi Mungu ameshatuwekea lakini sisi wenyewe hatuitumii.

Mhe. Spika, nakwenda kwenye maamuzi. Mhe. Spika, wataalam wa fani ya uongozi wanasema ukiwa meneja, ukiwa *administrator,* ukiwa kiongozi, kazi uliyoajiriwa moja wapo kubwa ni kufanya maamuzi, mambo yote haya mengine wewe unakwenda tu kikawaida. Wenyewe wanasema *"You are employed to make decision."*

Mhe. Spika, tunayo hii Kamisheni ya Utalii, Shirika la Utalii, Hoteli ya Bwawani na Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Hebu tufanyeni maamuzi ambayo mambo yote manne haya yatakwenda na ikiwa hatuliwezi moja wapo tuachane nalo tuendelee na mengine, sio kila siku tuongeze tu lisiletwe humu. Mhe. Spika, naomba sana tufanye tathmini tunakwenda vipi.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya kwenye kitabu hatukuelezwa maendeleo ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika majumuisho yake atupe kwa muhtasari chuo hasa kiko *position* gani, ni cha kimataifa, ni cha kitaifa au kiko katika ngazi ya aina gani. Pia uwezo wake wa kutosheleza mahitaji ya Zanzibar uko kwa kiwango gani na kwa wafanyakazi wa kada gani. Kwa sababu wale wafanyakazi wanaambiwa katika mahoteli wako wa kada fulani ambao wanapata pesa nyingi sana. Je, chuo chetu kina mwelekeo gani.

Mhe. Spika, nije kwenye magazeti. Mhe. Spika, kama walivyosema wenzangu kwamba tunalipongeza Gazeti la Serikali. Lakini kwa sababu ya Sera ya Serikali ya kuingiza sekta binafsi hebu Mhe. Waziri atueleze amechukua juhudi gani ya kuona kwamba Zanzibar nayo inayo gazeti lake la binafsi. Kwa sababu pengine kuna hofu imejengeka kwamba sera ni ya kufungia, kwa hivyo waandishi wetu na wale watakaofadhili mradi huu wana wasi wasi bado kwamba je, gazeti la binafsi hapa litakuwa au halitokuwa.

Mhe. Spika, gazeti la binafsi lina faida kwa sababu linatoa habari ambazo serikali pengine kwake ni vigumu kuzitoa, ndio katika kuongeza demokrasi na uwazi. Lakini pia historia ya Zanzibar inaonesha kwamba ilianzisha magazeti binafsi miaka mingi sana iliyopita kwa nini leo ifike wakati hata gazeti moja la binafsi iwe hakuna. Si kwamba imeporomoka kiasi kikubwa kama hicho na sisi tunasema tunajenga Zanzibar mpya. Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri kuna uzito unaotoka serikalini au bado hawajajitokeza hawa watu ambao wanataka kuweka magazeti binafsi, au wamepewa masharti ambayo bado hawajaafikiana.

Mhe. Spika, mwisho kabisa suala la utalii. Mhe. Spika, mara nyingi husema kwamba sisi tunapata watalii wengi na hoteli zipo lakini watu wetu wengi hawafaidiki na hii biashara ya utalii kwa sababu hakuna uzalishaji. Sasa Mhe. Waziri hebu aje atueleze ni utafiti wa kiasi gani wameufanya kuhusu vitu

vinavyotumika katika mahoteli ambavyo vinaweza kuzalishwa Zanzibar. Pia wamezishauri vipi wizara zinazohusika. Hao samaki wanaoambiwa wanapata bei kwa sababu wanauzwa katika mahoteli ya binafsi wanatosheleza. Ikiwa hawatoshelezi wanamshauri vipi Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi angalau kuleta kimeli kidogo ili tukaanza kujitosheleza sisi wenyewe kwanza katika wananchi na hotelini.

Mhe. Spika, samaki akija akitoka nje ya hapa sijui tutakwenda kusema vipi, lakini na mwananchi nae anataka kula yule samaki. Sasa ikiwa samaki wengi wanapelekwa mahoteli na wananchi wanabakia kuambulia madagaa, basi amfahamishe Mhe. Waziri tuletewe kimeli kidogo hapa mshirikiane. Mhe. Spika, nauliza hivi. Je, mmefanya tathmini ya hizi hoteli ambazo zipo na bidhaa wanazozitumia. Ni kwa kiwango gani zinatoka Zanzibar na wanaofaidika ni Wazanzibari.

Mhe. Spika, baada ya hayo, naomba Mhe. Waziri aje anijibu maswali yangu. Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 80 na 20 namuwekea ili aje amalizie kunijibu maswali yangu.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wa wizara hii kwa kuandaa hotuba hii. Nimshukuru yeye mwenyewe Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake pale jana na kwa kweli nimeipenda ile kasi yake ni nzuri sana.

Mhe. Spika, nianzie katika ukurasa wa 6 wa kitabu hichi Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametueleza kwamba wamefanya ukarabati wa jengo la wizara kwa kuweka miundombinu mipya ya maji, umeme, kununua samani, vitendea kazi, kompyuta na mambo mengine. Mimi nimpe hongera sana kwa kazi hiyo nzuri na kweli jengo limefanyiwa ukarabati ukipita nje linang'ara rangi inapendeza.

Lakini kwa masikitiko makubwa juzi tulikuwa tuna mkutano pale tulikwenda sisi, tukafanya mkutano katika ule ukumbi ambao ulikuwa wa Baraza wenyewe mlikuwa mna joto kali kweli kweli, yaani tumekaa pale kwa kuvumilia tu. Sasa viyoyozi vyote vile ulivyoviacha Mhe. Spika, havifanyi kazi na wewe umeondoka vinafanya kazi. Sasa sijui kama hiyo kampuni ambayo imepewa kazi ya ukarabati pale imeshamaliza au inaendelea. Kama inaendelea nakubaliana na Mhe. Waziri na maelezo yake haya, kama imeshamaliza kazi

sasa sijui huo ukarabati uliofanywa upi pale maana yake zile *AC* za kwenye ukumbi hazifanyi kazi kabisa.

Mhe. Spika, pia katika vyoo vya chini pale nimekuta maji yanamwagika hata vile vichwa vya mifereji hamna. Sasa Mhe. Spika, sijui kama Mhe. Waziri anapanda juu tu kwenda kule ofisini kwake au na huku chini anazunguka. Ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake anisaidie kidogo maelezo katika hili ili tuone kama kweli kumefanyika hayo au la.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 17 Shirika la Utangazaji. Mhe. Spika, mimi niipongeze sana kazi inayofanywa na shirika hili. Wanafanya kazi moja nzuri sana ya kuelimisha, kutoa burudani na kuwapasha habari wananchi. Siku hizi Baraza lako Mhe. Spika, limekuwa linaangaliwa mno kupitia vyombo hivi na wananchi wanapenda kutupa muda wao wakaangalia habari zinazoendelea hapa kwa kazi nzuri inayofanywa na shirika hili. Kwa hivyo, napenda nichukue fursa hii kuwapongeza watendaji wa shirika hili kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Lakini Mhe. Spika, nilikuwa na masikitiko madogo hapa, wakati televisheni inaonesha *live* tunao wenzetu kule ambao wanatutazama wenye ulemavu wa kusikia. Ningependa kama itawezekana basi ni vyema na wao wakatengenezewa mkalimani akawa anawatafsiria ili wakaweza kufahamu kwa sababu kwa hivi wanakuwa hawatusikii wanatuona tu kama tunaocheza. Sasa ningeshauri kama itawezekana basi kukawa kuna mkalimani wa kutafsiri yale maneno yetu na wenzetu wale wenye ulemavu wakaweza kufaidika na mambo haya.

Mhe. Spika, nizungumzie katika ukurasa wa 39 Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Mhe. Spika, chuo hichi kinafanya kazi moja nzuri sana ya kutusomeshea vijana wetu na kinastahili pongezi. Mhe. Spika, hivi karibuni mimi nilikwenda pale nikaona zile jitihada zinazofanywa na uongozi wa chuo hichi. Lakini Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atusaidie ule mkakati ambao unafanywa na serikali wa kuhakikisha kwamba vijana wale wanaotoka katika chuo kile basi wanapata ajira za fani ile waliyosomea. Kwa sababu tumekuwa tunalalamika sana na wao ndio wanaotwambia sisi tulalamike hapa kwamba wanapokwenda kuomba kazi huko kwenye mahoteli hawapati, kinakuwa kama kile chuo hakitambuliwi. Wanaochukuliwa zaidi ni vijana ambao wanatoka nje ya
Zanzibar au waliosoma vyuo nje ya Zanzibar.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje atusaidie kidogo hapa ni mkakati gani ambao wanauandaa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii, Idara ya Kazi, pamoja na hao wenye mahoteli kuhakikisha kwamba vijana wale wanapata nafasi ya kwenda kufanya kazi na wao.

Kwa sababu chuo kile kinatambulikana kabisa kisheria lakini mara nyingi wakati wanapoomba ajira wale wenye mahoteli wanaangalia wale waliosoma vyuo vyengine zaidi kuliko chuo kile. Ningemuomba sana Mhe. Waziri akasaidia hili ili tukapunguza ule urasimu uliokuwepo wa kupatikana ajira kwa vijana wetu.

Lakini vile vile nigusie suala la ardhi ya chuo. Tulikwenda kukagua pale kulikuwa kuna mwekezaji amevamia eneo la chuo na Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo alikuwepo na watendaji wake tukaona yale mazingira. Sasa Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha hapa atusaidie kutueleza wamefikia wapi katika suala lile.

Mhe. Spika, pia kuna suala la makusanyo kwa sababu wale vijana wanaosoma pale wanalipia, ninahakika ni fedha zinaingia za serikali, lakini katika kitabu cha Mhe. Waziri mimi sikuona malengo yako ya makusanyo kwa mwaka huu katika chuo hichi. Nimeona maombi tu ya fedha unaomba ruzuku upewe lakini wewe pia hukusema unajitahidi kiasi gani katika kuisaidia serikali kwenye makusanyo. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja naomba na hilo pia atusaidie.

Mhe. Spika, nizungumzie ukurasa wa 43 Shirika la Utalii. Mhe. Spika, shirika hili ni mali ya serikali na limeanzishwa kwa madhumuni ya kuisaidia serikali katika shughuli zake na katika kupata mapato. Lakini cha kusikitisha shirika hili limekuwa kama yatima halina mtu, hata zile shughuli zake inaonekana kama liko legelege. Maana mpaka hii leo hili shirika hata bodi halina, sijui linajiendeshaje, maamuzi yake yanatolewa wapi. Ndio maana utakuta kuna mali zake nyingi hapa zinachukuliwa. Inaonekana hana hata meneja maana yake nguvu hana, nguvu yake ni bodi lakini haipo. Sasa serikali hebu itwambie kama inaamua inataka kulivunja kabisa hili shirika bora ilivunje liwe halipo, kuliko kuwepo lakini haliendi kwa mujibu wa utaratibu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha hapa atueleze kuna tatizo gani kwamba shirika hili sijui mwaka wa ngapi sasa halina bodi.

Mhe. Spika, pia shirika hili limekuwa likinyang'anywa sana mali zake na kwa sababu halina bodi halina mtetezi. Pengine anaamriwa na Katibu Mkuu fanya hivi, anafanya. Sasa kuna nyumba zile za Chwaka zilinyang'anywa kutoka kwenye shirika hili, mimi nasema zilinyang'anywa kwa sababu hazikufuata utaratibu, tumeshakwenda tukafanya ukaguzi pale. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atusaidie suala hili vipi, maana moja kachukua Chuo cha Fedha Chwaka, lakini ile moja mpaka leo hatujapata ufumbuzi wa kwamba anayo nani. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze ile nyumba ameizuia nani na nani anaimiliki. Kwa sababu hatimiliki bado ni za Shirika la Utalii lakini kuna watu wanazuia.

Mhe. Spika, nije Kisiwa cha Changuu, kisiwa hichi kilikuwa kinaendeshwa na Shirika la Utalii, lakini kwa masikitiko makubwa kabisa meneja anapewa taarifa kwamba kimeshakodishwa kwa mwekezaji mwengine, sasa hiyo bei ya kukodisha ndio shughuli yetu inayotufanya sisi tuulize mara mbili. Nafikiri Mhe. Ismail Jussa Ladhu alipokuwa akichangia alisema pale kwamba kimekodishwa dola 3,500 wakati wao shirika walikuwa wanakiendesha karibu kwa dola 8,000 kwa mwezi. Sasa tumetoka kuacha pesa nyingi tunakwenda kuchukua pesa kidogo, mimi hapa kidogo ninapata mashaka. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe ufafanuzi juu ya suala hili.

Mhe. Spika, nizungumzie uuzwaji wa magari ya shirika. Tulipita pale na kamati yetu tukakuta pana magari yanataka kuuzwa na tukatoa maelekezo ya taratibu. Tukawaambia kama mmeshaamua wenyewe kwamba haya magari yamechakaa na yauzwe lakini zile taratibu za uuzwaji wa mali za serikali zifuatwe. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja naomba atusaidie kwenye magari haya mawili, lile basi kubwa na ile *minibus* taratibu ambazo zilitumika mpaka kuuzwa kwake, ili tuweze kujua kwamba zile taratibu zilifuatwa.

Halafu Mhe. Spika, kuna madeni katika Kampuni ya *Royal Star* wanadaiwa pesa na shirika kwa ajili ya huduma ambazo ilikuwa inapewa ile meli. Kampuni hiyo ina meli yake iliyokuwa inafanya kazi ikishirikiana na Shirika la Utalii wanawadai hawa. Sasa kwa sababu ya ule unyonge wake iliokuwa nao lile shirika wanashindwa hata kuyafuatilia haya madeni. Mhe. Spika, sijui Mhe. Waziri wizara yake imewasaidia vipi Shirika la Utalii kuhakikisha kwamba madeni yale yanaweza kupatikana ili waweze na wao kumsaidia na waweze kujiendesha kama ambavyo nilizungumza kwenye Chuo cha Utalii. Shirika nalo limeomba ruzuku hapa, maana limeomba pesa kwa ajili ya matumizi, lakini nalo linafanya kazi, lakini halijatuonesha linategemea kukusanya kiasi gani. Nimejaribu kuyaangalia mahesabu yako ya kuomba kukusanya kule ni zile zile ambazo umezionesha. Kwa hivyo, Shirika la Utalii, Chuo cha Utalii na nyengine, hizi taasisi zote hazijaonesha zitakusanya kiasi gani au zinakusudia kukusanya kiasi gani. Sasa sijui kama hii hesabu ilisahauliwa au vipi, kwa hivyo nakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho yako hapa basi mutueleze, mnakusudia kukusanya kiasi gani katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nisogee kwenye ukurasa wa 45 katika Hoteli ya Bwawani

**Mhe. Spika:** Kwa dakika 4.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Ahsante Mhe. Spika. Hoteli ya Bwawani wachangiaji wengi wamechangia hii na wameichangia kwa sababu inaonekana zile zile ambazo mimi nilikuwa naziona na wenzangu kumbe wameona yale yale. Kwa hivyo, kunaonekana kuna tatizo pale, hasa la udhibiti wa fedha za serikali, hakuna udhibiti pale.

Mhe. Spika, kumbi zile zinakodishwa bila ya kufuata taratibu. Katika kitabu chake hiki Mhe. Waziri katika ukurasa wa 78, ametuonesha ukodishwaji wa ukumbiwa Komba Disco. Nimesoma hapa anasema tangazo la zabuni limetolewa kwenye gazeti la Zanzibar Leo, imeandikwa Zanzibar Leo, lakini najua itakuwa ni gazeti, lakini halikuandikwa ni la tarehe ngapi, ingawa hizi nyengine nyingi zimeandikwa mpaka tarehe lilipotoka. Kwa hivyo, hebu Mhe. Waziri hii tarehe ya Zanzibar Leo lilipotolewa hili tangazo ilikuwa ni tarehe ngapi.

Mhe. Spika, halafu kampuni ambayo imeshinda zabuni ni *National Marketing Company Limited*, kwa zabuni ya milioni 15. Sasa hii milioni 15 sijui ni kwa mwaka au kwa mwezi au ni kwa kipindi gani na hawa wengine tulikuwa tunapata maneno hapa kwamba kuna watu walikuwa wameitaka kwa milioni 40 kwa mwezi, kuna waliotaka kwa milioni 30 kwa mwezi. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja hebu tueleze katika sakata hii kidogo ikoje, kwa sababu panaonekana kama pana wasi wasi kidogo. Kwa sababu hata ule mkataba unaonesha hizi milioni 15 huyu ambaye amepewa bado atakuwa anaikata ile Hoteli ya Bwawani kwamba ana pesa za matengenezo kila mwezi. Sasa sijui matengenezo gani yanayokuwa kila mwezi ya milioni 5. Yaani huyu amekodishwa kwa milioni 15 lakini ajikate yeye kila mwezi tena mpaka anapomaliza mkataba, naona hii kidogo haikukaa sawa. Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri uje utusaidie hilo kutuwekea sawa sawa.

Vile vile nizungumzie kwenye suala la mmong'onyoko ule. Kwa kweli lile eneo linaharibika sana hasa hii barabara ya kutokea upande wa Msikiti Mabluu, hata ile barabara yenyewe imeshakuwa inaharibika. Mimi nakuomba sana Mhe. Waziri tuwaombe hawa watu wa Bwawani mshirikiane na hizo taasisi nyengine kwa haraka ili muweze kulirekebisha lile tatizo. La si hivyo kuna siku tataamka asubuhi pale hatuwezi kukatiza kuingia Bwawani, itabidi uzunguke kwa kupitia Malindi. Kwa hivyo, mfanye bidii pale ili kuweza kufanya ukarabati wa hilo.

Mhe. Spika, pia Hoteli ya Bwawani inaomba matumizi, lakini haikutuonesha kwamba yenyewe inakusudia kukusanya kiasi gani hakuna hayo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie hili, kwamba wao wanaomba lakini hii ni taasisi ambayoinatakiwa ijiendeshe, kwa sababu pale wanaendesha biashara. Sasa tutizame wao watatuletea ngapi, halafu na hiyo ruzuku ndio iweze kuwasaidia. Lakini wao wakiwa wanaomba zote, sasa hicho wanachokikusanya

wao ni kiasi gani na hakimu katika mahesabu yako ya wizara hapa. Katika mjumuisho wako wa hesabu kule unaonesha ni pesa zile zile ulizoonesha kwenye mashirika yale mengine, lakini hawa wengine wote hazikuonesha hapa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba utakapokuja utusaidie hilo.

Mhe. Spika, najua umeshanihimiza, lakini nisogee kidogo kwenye suala la hii Kamisheni ya Utamaduni. Wajumbe wenzangu wamezungumza sana kwenye masuala haya ya maonesho yale. Mimi nazungumzia kwenye masuala ya magofu. Mhe. Spika, magofu yetu yanafika pahala yanaanguka kwa sababu hayafanyiwi ukarabati.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika, magofu haya tuwe tunayafanyia ukarabati, sio ule ukarabati wa kuyageuza yakawa mapya, lakini mimi nimeona kule Bagamoyo wenzetu wanafanya ukarabati wanayageuza, lakini wanayarejesha katika hali ile ile. Kwa hivyo, na sisi hapa yale magofu yetu tusiyawache yakawa yanapotea, kwa sababu ule ukuta kama utauwacha ukaanguka haukujengwa tena basi baada ya muda hata hilo gofu lenyewe litakuwa halipo. Naomba tuwe tunayahifadhi vizuri, tuyafanyie ukarabati ili yaweze kukutana na kizazi kinachokuja, kama ambavyo sisi tumeyakuta.

Vile vile kulikuwa kuna suala la makumbusho ya mambo ya kale. Mhe. Spika, nilikwenda kule Unguja Ukuu, kuna jengo niliambiwa ni la makumbusho, sijui jengo lile vipi naona limeachwa tu, liko pwani kabisa kule. Limeachwa halifanyiwi ukarabati wowote, limejengwa jengo zuri tu, baadae limeachwa yaani halina uangalizi wa aina yoyote. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja utusaidie jengo lile vipi, mmeshalisamehe, mmemgaia mtu au mnafanyaje.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naona unanihimiza. Mimi naiunga mkono kwa asilimia 50 bajeti hii mpaka nitakapopata majumuisho ya Mhe. Waziri basi naweza nikarudi huku.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia mchana wa leo kuwepo hapa katika Baraza lako tukufu.

Pili, nimpongeze Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuteuliwa kwake kuwa waziri wa wizara hii, wizara ambayo ni muhimu inagusa watu wengi, wengine wanathubu kusema kwamba habari ni moja kati ya mihimili isiyorasmi, baada ya ile mihimili miwili mitatu ile ya dola, kwa hivyo na huu ni muhimili mwengine usio rasmi jinsi ya umuhimu wake.

Mhe. Spika, mimi nianze katika sekta ya habari, hasa katika eneo hili la Shirika la Utangazaji. Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa amesema kwamba shirika hili limeundwa baada ya serikali ya awamu ya saba kuamua kuziunganisha shughuli za matangazo ya televisheni, redio na serikali.

Mhe. Spika, jambo hili ni muhimu na hata katika Baraza lako lililopita tulishuhudia wajumbe wengi wakitoa mawazo kama hayo ya badala ya kila idara kuwa na majukumu yake, basi sasa ni vyema tukawa na Shirika la Utangazaji, kama walivyowenzetu wa Tanzania Bara, jambo jema huigwa.

Mhe. Spika, pamoja na nia nzuri ya serikali kuanzisha jambo hili, lakini inaonesha ni jinsi gani kwamba hatukujiandaa katika kuanzisha shirika. Chombo chochote ili kiwe na nguvu ni lazima kiundwe kwa mujibu wa sheria. Mhe. Mjumbe mwenzangu hapa Mhe. Omar Ali Shehe alilizungumzia, lakini na mimi kwa kuliona umuhimu wake na ni jambo ambalo tokea lilipoanzishwa Shirika la Utangazaji, lilikuwemo ndani ya kichwa changu, mbona hakuna sheria ambayo imepitishwa kwa ajili ya kuanzisha jambo hili ambalo ni muhimu na ni jambo ambalo linahitaji sheria. Leo hapa Mhe. Waziri ametueleza.

Mhe. Spika, pia nitajaribu kuangalia katika eneo hili la wizara yake ya mipango, nikaona angalau ile idara ya mipango, sera na utafiti. Nimepitia katika idara hii angalau nione ni namna gani walivyojipanga kuona kwamba wanaanzisha sera au sheria katika kipindi kijacho, sheria ambayo inaweza kuongoza shirika hili katika ufanyaji kazi wake. Pia inaonekana hata maandalizi ya kuanzisha sheria pia hayapo.

Mhe. Spika, vile vile niliangalia katika kitabu cha bajeti ya wizara sikuona eneo lolote linaloonesha kwamba kuna fedha zilitengwa kwa ajili ya kuendesha shirika. Ni bajeti ambayo ipo ya Idara ya Televisheni, lakini pia kuna Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar peke yake. Sasa Mhe. Spika, nilikuwa najiuliza shughuli hizi za shirika hili zitaendeshwaje, mamlaka ya shirika yakoje, muundo wa shirika ukoje, pia sikupata jibu. Katika maelezo yake Mhe. Waziri ametuambia hapa kwenye utekelezaji halisi ametueleza kwamba shirika limeshafungua ofisi yake katika jengo la Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo liliopo Magogoni Dar es Salaam. Nikasema hivi hili shirika sasa makao makuu yake yako Dar es Salaam Magogoni, pia sikupata jibu.

Mhe. Spika, kwa kweli nia ya kuanzisha shirika ni nzuri, lakini inaonekana hatukujitayarisha na wala hatukujipanga. Kutokujipanga maana yake sasa hivi kumeonesha kumekuwa na migongano. Sasa sijui Mhe. Waziri unaelewa kwamba kumekuwa na migongano kati ya viongozi wa idara hizi mbili.

Kunapokuwa na migongano maana yake ufanisi katika shughuli za kazi haupo. Sasa nataka Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze vizuri juu ya uanzishwaji wa shirika hili, nini *roll* yake, inafanyakazi vipi, muundo wake ukoje na ofisi yake ikowapi, ili tuone kuwa shirika hili linakwenda vizuri na kuweza kufikia yale malengo ambayo tumeyakusudia.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametueleza kwamba katika mwaka wa fedha 2011/12 Shirika la Utangazaji limepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo, ameyataja Mhe. Waziri. Moja anasema ni kuimarisha ubora wa matangazo yake ili kuweza kuwavutia wasikilizaji, watazamaji wengine na wafanyabiashara wa ndani na nje ya Zanzibar. Hili ni lengo zuri na kwa sababu vyombo hivi vinasikilizwa na wengi na vinatazamwa na wengi. Kwa hivyo, hili ni lengo zuri sana.

Mhe. Spika, hebu tujiulize azma hii ya kuimarisha ubora wa vipindi vyetu iko sawa. Kwa mfano, katika televisheni Zanzibar kuna taarifa za habari zinasomwa, taarifa ya habari ya mwanzo inasomwa saa 2:15, lakini ya pili inasomwa saa 4:15 ya kila siku. Kwa kweli Mhe. Spika, wananchi wengi wa Zanzibar wanapenda sana kuiangalia taarifa ya habari ya Zanzibar ili wapate nafasi ya kujua matukio ya kila siku, nawaza kusema kuliko vipindi vyengine.

Mhe. Spika, kuna jambo ambalo linafanyika wananchi wengi wanalilalamikia katika masuala yale ya taarifa ya habari, kwamba kwanza taarifa zetu za habari ni fupi mno ni tofauti na wenzetu. Kwa hivyo, wananchi hawapati nafasi ya kujua taarifa kamili juu ya jambo fulani, hiyo ni kasoro.

Lakini la pili, hii taarifa ya habari ya saa 4:30 inasomwa kwa dakika 5 tu, ambapo ile ya mwanzo angalau inapata robo saa, lakini ile ya saa 4:15 inasomwa kwa muda wa dakika 5 tu, inakuwa fupi zaidi kuliko ile ya mwanzo. Sasa Mhe. Waziri hebu tuambie kwa nini taarifa ya habari ile ya mwanzo pamoja na udogo wake na ile ya pili zinakuwa hazifanani, kwa nini kuna baadhi ya maeneo yanaachwa. Mhe. Spika, kuna watu hawapati nafasi ya kuangalia taarifa ya habari ya saa 2:15, wanafukuzia ya saa 4:15, lakini matokeo yake taarifa zile zinakuwa hazitimii, badala yake wanafukuzia kuweka sijui *moves*, wanafukuzia haraka haraka dakika 5 kisha wanaweka *moves*, wanafukuzia kitu ambacho hakina msingi wala faida yoyote. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri, wakati tunapoangalia, tunaposoma taarifa ya habari zetu za televisheni Zanzibar basi zikamilike, yaani taarifa zake ziwe kamili ili wananchi waweze kujua washibe kama walivyokuwa wenzetu.

Jengine Mhe. Spika, kuna kipindi ambacho kilikuwa kinaonyeshwa katika televisheni, kinaitwa *roving report.* Kipindi hiki siku hizi hakipo kimeondoshwa na ni kipindi ambacho kilikuwa kina watazamaji wengi sana,

ambapo watu wengi walikuwa wanapata nafasi ya kujua mambo mengi. Nahisi kipindi hiki kimeondoshwa kwa sababu pengine kilikuwa kinawagusa baadhi ya viongozi wa sekta na kwa sababu kipindi hiki kilikuwa kinaonyesha yale maeneo ya udhaifu ambayo yanaonekana yapo katika visiwa vyetu. Kwa bahati mbaya sana kipindi kile kimeondoshwa kwa mazingira ya kutatanisha na ni kipindi ambacho watu wanakipenda na wanauliza kulikoni.

Kwa hivyo, nimuomba sana Mhe. Waziri kipindi hiki ni muhimu na kwa sababu kinatoa msaada wa kujua matatizo yetu yakoje na serikali ipate nafasi ya kuyatatua yale maeneo ambayo yanaoneshwa ni kipindi muhimu ambacho kinahitaji kurejeshwa na kuona kinaendelea kufanya kazi.

Mhe. Spika, nije katika Shirika la Magazeti ya Serikali. Mimi nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa Shirika la Magazeti ya Serikali. Mhe. Spika, gazeti hili limepiga hatua kubwa sana na linastahiki pongezi, tukiangalia huko nyuma tunakotoka na sasa hivi lilivyo, gazeti limepiga hatua kubwa. Leo pia tumepata nafasi ya kusikia kwamba gazeti linasomwa katika redio mbali mbali na katika vipindi mbali mbali kwa wenzetu Tanzania Bara TBC na kwengine. Hiyo ni hatua moja kubwa. Pia gazeti hili sasa limekuwa ni la rangi, linakwenda na wakati.

Mhe. Spika, gazeti hili lina changamoto nyingi. Changamoto moja ya gazeti hili la Zanzibar Leo ni mtambo wa kuchapisha kama wenzangu walivyosema. Suala hili tumekuwa tukilizungumza kila wakati. Changamoto nyengine ni juu ya madeni ya serikali inayodaiwa na shirika hili. Mhe. Spika, nikikutajia hapa serikali jinsi inavyodaiwa na shirika hili ambapo fedha hizi zingeweza kusaidia katika kuliimarisha. Mhe. Spika, shirika linaidai serikali milioni 114 hiki ni kiwango kikubwa sana kwa shirika changa kama hili ambalo ndio kwanza tunalianzisha.

Mhe. Spika, inasikitisha kuona kuwa serikail imeanzisha chombo chake wenyewe, lakini badala ya kukisaidia ili kiweze kujiendesha kibiashara, basi fedha zile ambazo wanadai hawapatiwi. Kuna idara mbali mbali hapa, ningeomba nizitaje na wenyewe Waheshimiwa Mawaziri kama wapo wasikie pengine hawaelewi.

Idara ya Mazingira inadaiwa milioni 1,680,000, Idara ya Anga inadaiwa Shs. 300,000 na shirika hili. Wizara ya Katiba na Sheria inadaiwa milioni 1,095,000, Idara ya Nyumba inadaiwa milioni 2.5, Baraza la Manispaa linadaiwa Shs. 500,000, Idara ya Ardhi na Usajili inadaiwa milioni 1,475,000, Baraza la Wawakilishi linadaiwa milioni 1,700,000 katibu. Katibu anasikia kwa bahati nzuri. Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto inadaiwa milioni 4,594,000, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na

Nishati inadaiwa milioni 28,258,000, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inadaiwa milioni 9,000,000, tume ya ukimwi inadaiwa milioni 4,600,000, Mtakwimu Mkuu wa Serikali inadaiwa milioni 3,150,000, UUB wanadaiwa milioni 4,350,000, Wizaa ya Fedha yenyewe inadaiwa milioni 11,560,000, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais inadaiwa milioni 7,670,000, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inadaiwa milioni 7,700,000, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma Utawala Bora inadaiwa milioni 8,433,000, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inadaiwa milioni 11,568,000.

Hivi Mhe. Spika, madeni kama haya, shirika kama hili changa na fedha serikalini zinatoka kwa ajili ya hesabu hii halafu hatuwapi je, lengo letu ni nini. Mhe. Spika, naomba serikali ilipe madeni haya. Mawaziri wanaohusika wanatusikia, walipe deni ili shirika hili liweze kujiendesha kibiashara. Nimuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha au Kaimu Waziri wa Fedha, kama wizara zinashindwa kulipa moja kwa moja basi fedha hizi zichukuliwe katika fedha zao za *other charges*. Wizara ya Fedha ichukuwe fedha hizi moja kwa moja kutokana na *other charges* ambazo zinatolewa katika mawizara hayo, ili tuone shirika letu hili linasonga mbele.

Mhe. Spika, mwisho kwa kuwa nimechukua muda wako mwingi, nizungumzie katika sekta hizi za utalii. Mhe. Spika, sekta ya utalii ni sekta muhimu sana, nadhani ile dhana ambayo tulikuwa nayo hapo mwanzo ambayo tulikuwa tukisema kwamba utalii ndio sekta kiongozi imeshatoweka na kwa sababu tunahisi kwamba hatutowi msukumo unaostahiki ili kuona kwamba sekta hii ya utalii inaimarika. Mhe. Spika, bajeti ambazo tunazipa sekta ya utalii ambayo ndio sekta kiongozi, kwa kweli hazitoshi. Kamisheni ya Utalii imetengewa milioni 800,000,000 peke yake kwa ajili ya kuendesha shirika hizi ni fedha chache sana. Kwa sababu Mhe. Spika, utalii hauwezi ukaimarika bila ya kutangazwa.

Mhe. Spika, wenzetu hapa wamepanga mipango mbali mbali ya ku-*promote* utalii. Suala la ku-*promote* utalii ni gharama kubwa. Wenzetu katika nchi ambazo zimeendelea katika sekta hii ya utalii wanatenga asilimia maalum ya bajeti zao kuu kwa ajili yaku-*promote* utalii. Hii inaonesha ni jinsi gani walipotoa kipaumbele kwa sekta hii. Lakini leo kwa kweli inasikitisha kuona kwamba sekta ya utalii imetengewa fedha chache ambazo kwa kweli haziwezi zika-*promote* utalii. Utalii kama tulivyokubaliana mwanzo kwamba utalii ndio sekta kiongozi. Kwa hivyo, naomba niiombe serikali itowe kipaumbele katika eneo hili ili tuone kuwa utalii sasa unakuwa na bado utaendelea kuwa ni sekta kiongozi.

Mhe. Spika, Chuo chetu cha Utalii kiko katika hali mbaya. Mwaka jana serikali ilitueleza kwamba imetenga milioni 400,000,000 kwa ajili ya maendeleo ya Chuo cha Utalii. Lakini Mhe. Waziri kwenye hotuba yake hakutuambia kwamba mwaka jana amepewa kiasi gani, isipokuwa anatuomba na mwaka huu tukubali kumuidhinishia milioni 400,000,000 nyengine kwa ajili ya kukiendeleza chuo. Hii inakuwa haipendezi na kwa sababu tunapoidhinisha fedha kwa ajili ya kitu fulani, basi Waheshimiwa Mawaziri ni lazima watupe taarifa juu ya zile fedha walizoziomba wamepata kiasi gani, ili tuweze kuwaidhinishia fedha nyengine. Sasa hapa unakuwa ni mtihani na kwa sababu milioni 400,000,000 ambazo zimeombwa mwaka jana, hazioneshwi kwamba kuna mabadiliko yoyote katika chuo kile, bado majengo yake ni mabovu, bado watoto pale wanasoma chini ya mti na chuo kile ndio uti wa mgongo wa utalii.

Mhe. Spika, pale tunategemea kutoa vitu vya uhakika pale, tutowe wafanyakazi pale wenye vyeti vinavyostahiki, tutowe wafanyakazi ambao wanaweza kwenda kufanyakazi katika mahoteli makubwa makubwa. Lakini ni aibu kuona kuwa kile ndio Chuo cha Utalii, unapokwenda pale ukiambiwa hiki ndio Chuo cha Utalii cha Zanzibar tena chuo cha serikali, wewe mwenyewe utashangaa. Kwa kweli haipendezi. Mhe. Waziri, hebu tueleze kidogo tu mwaka jana ulipata kiasi gani katika fedha zile ambazo umeomba.

Jengine la mwisho Mhe. Spika, ni suala la Hoteli ya Bwawani. Hoteli ya Bwawani Mhe. Spika, tumekuwa mara nyingi tukisema kwamba hii hoteli wapewe watu wa chuo iwe ni miongoni mwa taasisi za chuo cha utalii, kuliko hivi ilivyo sasa hivi. Serikali huko nyuma ilikubali kwamba iko kwenye utaratibu wa kuona kwamba Hoteli ya Bwawani inakuwa ni sehemu ya Chuo cha Utalii na kwa sababu tulipendekeza vile, tulikuwa na malengo kwamba wanafunzi waweze kwenda pale katika hoteli ile kufanya mafunzo yao kwa vitendo na huku tukiamini kwamba hoteli ile itakapokuwa ni sehemu ya Chuo cha Utalii basi itaweza kutengenezwa na kuwa katika hoteli yenye *standard.* Leo Hoteli ya Bwawani kwa kweli hairidhishi. Historia ya hoteli ile imepotea. Ukienda kwenye vyumba vile ambavyo vinakodishwa kwa kweli haviendani na hadhi ya hoteli yenyewe. Hoteli ya Bwawani imebakia jina peke yake kwamba hii ni hoteli ya Bwawani, lakini hakuna huduma zozote ambazo zinalingana na hoteli, kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana. Tumuombe Mhe. Waziri kwamba ipo haja na ushauri ambao ulitolewa kwa siku za nyuma wa hoteli hii kuwa ni sehemu ya chuo cha utalii katika kuimarisha chuo kile na mambo mengine, basi muweze kulifikiria sana na kwa sababu sisi tunahisi litasaidia katika kukinyanyua kile chuo, lakini na kunyanyua ile hoteli.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda wako unakaribia kumalizika, nimalize suala moja la mwisho, kwenye Idara ya Habari Maelezo. Mhe. Spika, Idara ya Habari Maelezo siku hizi imekuwa haitumiki ipasavyo. Lengo la Idara ya Habari

Maelezo ni serikali kupitia idara hii kutoa maelezo yake pale ili wananchi wasikie. Lakini siku hizi kumekuwa na mitindo Waheshimiwa Mawaziri wanapotaka kutoa maelezo yao basi huwa wanawaita waandishi wa habari mmoja mmoja, wanawapigia siku katika ofisi zao, badala ya kuitumia hii Idara ya Habari Maelezo. Hili sio jambo zuri na badala yake taarifa zile zinatoka kama waandishi binafsi, kila mwandishi anatoa anavyotaka yeye, badala ya kuwa taarifa zile ziwe zinatolewa na chombo hiki muhimu tulichokiunda cha Idara ya Habari Maelezo. Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri na watu wengine. Tunapotaka kutoa taarifa zetu kwa umma basi tuitumie idara hii ili taarifa zetu zinapotoka basi ziwe ni za kiserikali kuliko ilivyo hivi sasa. Sasa hivi taarifa ambazo mnazitoa zinakuwa ni za kibinafsi zaidi kuliko chombo hiki ambacho kimeundwa.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja na nimuombe Mhe. Waziri kwa yale masuala ambayo nimemuuliza basi anitayarishie majibu ili bajeti yake iweze kupita bila matatizo, ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Tunakushukuru Mhe. Salmin Awadh kwa kutudai mbele ya hadhara ya watu leo. Lakini mimi na wenzangu tutajitahidi tulipe. Waheshimiwa Wajumbe, kutakuwa na mkutano wa Waheshimiwa Wajumbe wanawake hapa hapa ukumbini mara baada ya kuahirishwa kikao hichi, kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe wanawake mnaombwa mbaki kidogo kuna mkutano wa dharura, Mwenyekiti anataka mzungumze kwa pamoja.

Waheshimiwa Wajumbe, jioni tutaendelea na waheshimiwa wafuatao;

1. Mhe. Hija Hassan Hija
2. Mhe. Mohammed Said Mohammed
3. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
4. Mhe. Fatma Mbarouk Said

Nawengine wengi ambao nitawaomba. Kwa maana hiyo Waheshimiwa Wajumbe tujitahidini kufika mapema kama kawaida na tuje tupunguze muda, bado tuko nyuma ya ratiba, ili tuhakikishe kwamba shughuli yetu hii inamalizika kwa mujibu tulivyoipanga.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

*(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kama tulivyotangulia kusema mapema pale mchana kwamba tuko nyuma ya ratiba yetu. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe mnisaidie kuendesha kikao hiki, tupunguze kurudia rudia ilimradi tupate wachangiaji wengi ambao kimsingi nilionao nadhani wanatocheleza. Kwa hivi sasa ninao wachangiaji wapatao 17 nafikiri wananitosha sana. *(Makofi)*

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo, ili niweze kutoa mchango wangu kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja kusadia Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mhe. Waziri kama wenzangu walivyozungumza kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake kwa *speed* kubwa, lakini kwa umakini wa hali ya juu.

Mhe. Spika, pamoja na upya wake Mhe. Waziri nadhani sote tutakubaliana kwamba hotuba yake ameisoma kwa ufanisi mzuri na bila ya shaka Waheshimiwa Wajumbe wameifahamu.

Mhe. Spika, tukumbuke tu kwamba hii ni Wizara ya Habari ambayo duniani hivi sasa wenzetu wanazungumza kwamba habari ni muhimuli mwengine pengine wa dola ingawa sisi hatujafikia huko, lakini wapo wataalamu ambao wanapendekeza hivyo pengine ungekuwa muhimili wa nne wa dola suala zima la Vyombo vya Habari.

Mhe. Spika, kabla ya kwenda kwenye hotuba hii nikushukuru kwamba unilichagua kuwa Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii tena wenzangu wakanipa Makamu Mweyekiti wa kamati hiyo. Kwa niaba ya kamati yangu Mhe. Spika, nitoe masikitiko makubwa kwa tukio ambalo limetokezea jana Pemba la mwanamke mmoja kufanyiwa ukatili mkubwa. Mhe. Spika, kuna mwanamke mmoja jana akiwa mjamzito wa miezi minane alifungwa kamba miguu miwili na kuning'inizwa kichwa chini miguu juu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii nalaani sana tukio hili na suala hili pia tumelipata kwa msaada wa vyombo vya habari, laiti kama si waandishi wa habari na hasa wale wa *Zenji FM* ambao wanacho kipindi chao cha *Breaking News* nadhani zingelichelewa kufika kwetu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika mimi mwenyewe binafsi pamoja na kwa niaba ya kamati yangu tunalaani suala hili kwamba huu ni ukatili, kwa sababu kama angefariki basi maana yake wangelifariki watu wawili. Lakini kwa msaada mzuri kwa wasamaria wema na polisi hatimaye walimnusuru mtu yule na walimkatama yule mtu aliyefanya suala lile.

Mhe. Spika, baada ya msikitiko yangu hayo kwa niaba ya kamati sasa niende kwenye viambatanisho. Kwa kweli Mhe. Waziri ametuwekea viambatanisho kwenye ukurasa wa mwisho kiambatanisho No. 5 kuna wafanyakazi walioko kwenye masomo na idadi yao ni wafanyakazi 71, tena hao Mhe. Waziri ametuambia ni mwaka 2010 hadi 2011 maana yake ni mwaka jana. Wengine Mhe. Spika, wafanyakazi hao wanao miaka miwili, mitatu na wengine wanayo miezi 6.

Kwa hivyo, nimeona nilizungumze hili kwa sababu nimeona wafanyakazi wengi wako masomoni labda Mhe. Waziri aniambie tu ikiwa hawa wote 71 wako masomoni ofisi imebakiwa na watu wangapi kwa sababu ni watu wengi sana? Vile vile Mhe. Waziri atueleze wafanyakazi hawa ambao wamesomeshwa wametumia fedha zipi, yaani fedha zao binafsi au za wizara?

Mhe. Spika, kwenye kiambatanisho hicho kuna mfanyakazi Moh'd Nassor Moh'd Kamisheni ya Utalii tumeambiwa anasomea Sheria ngazi ya *PhD* lakini katika Chuo Kikuu cha *SUZA*. Sasa naomba kujua *SUZA* yetu sisi hapa Zanzibar au kuna *SUZA* nyengine nje, kwa sababu huyu bwana anasomea *PhD* miaka miwili lakini Chuo cha *SUZA*, hivyo ni *SUZA* ipi hii ya Zanzibar au nyengine iko nje. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri anifafanulie, ili niweze kujua.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba nitaendelea kuwa balozi wa waandishi wa habari, kwa sababu gani Mhe. Spika, laiti kama si msaada wao basi leo mwananchi wa Mwambe na Kiwani wasingesikia maneno ninayoyazungumza hapa. Kwa hivyo, siwezi hata siku moja kuwabeza waandishi wa habari pamoja na vyombo vyao vya habari.

Mhe. Spika, baada ya Mhe. Waziri kuingia tu, ameamua sasa kutangaza Baraza la Wawakilishi moja kwa moja kwa kutumia *television* na *radio*, kwanza nimpongeze kwa hilo, kwa sababu wamekaa mawaziri wengi wenye uwezo lakini hilo hawakulifanya na hii ni hatua moja ambayo Mhe., Waziri ambayo ameifanya. Hivyo, kwa niaba ya serikali Mhe. Spika, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, iwapo ameweza kuonesha vipindi vya *radio and television live*, kwa nini ashindwe kuwahudumia wafanyakazi wa vyombo hivi. Mhe. Spika,

nimefanya utafiti mdogo nimeona kwamba wafanyakazi wa *radio and television* ambao wanahudumia mijadala hii kuanzia hapa ndani ya Baraza hadi kwenye minara ni wafanyakazi 31, ambao kila siku wanahudumia huduma hizi. Mhe. Spika, nimefanya utafiti kuona kwamba kama hawa wangelipwa posho lote kwa siku 46 ambazo tutakuwa hapa maana yake wizara ingegharamia shilingi milioni 7,130,000/=.

Mhe. Spika, hawa ni waandishi wa habari ni wafanyakazi, lakini mwanzo ni wanaadamu. Kwa hivyo, Mhe. Spika kama ambavyo mimi siwezi kuishi hapa bila ya huduma, basi ndivyo ambavyo mwenzangu mwandishi wa habari hawezi kuishi bila ya huduma. Mhe. Spika, nasema kwamba Mhe. Waziri nimuombe sana asitafute ugomvi na wananchi wa Kiwani, isipokuwa atafute fedha kwa ajili ya kuwasaidia ndugu zangu hawa, kwa sababu ni haki yao tena niwajibu kuwasaidia.

Mhe. Spika, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imetenga shilingi milioni 86 kwa ajili ya safari za nje na ndani, lakini unashindwa kuwatengea posho wafanyakazi ambao wanaokaa hapa kutoa asubuhi hadi jioni. Mhe. Spika, lazima Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu wanikubalie kwamba fedha hii leo tuigawe, yaani tuwatolee waandishi wa habari zao kabisa na baadaye zilizobakia ndio wafanye safari.

Kwa kweli haitiliki maanani Mhe. Spika, kwamba wenzetu hawa wanakaa hapa na wala hawana mavazi ya kutosha, kwa sababu ni wajibu wao kwa mujibu wa shughuli zao za kazi, lakini watu wanatenge fedha kwa ajili ya safari za ndani na nje shilingi milioni 86.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na ninawaomba Waheshimiwa Wawakilishi na wanikubalie ombi langu, kwamba fedha hizi za Idara ya Utumishi na Uendeshaji za safari tuzigawe na tuzitoe kabisa kabla ya bajeti hii, yaani fedha za huduma za waandishi wa habari, vyenginevyo bajeti hii sitoikubali kwa msingi huo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mbali na hilo pia kuna waandishi wa habari ambao walitakiwa kupatiwa mavazi, kama wenzangu walivyosema hadi hii leo suala hili bado halijafanyika. Vile vile kuna waandishi wa habari ambao walisafiri mwaka jana kwenda nje ya nchi, wakapatiwa posho la shilingi 500,000/= na nyengine waliambia wakope na watakaporejea watapatiwa fedha zao, Mhe. Spika hadi hii leo fedha hizo bado hawajapewa.

Hivi kweli tunafanya nini? Mhe. Spika, ikiwa waandishi wa habari ndio tunawategemea watuuzie habari zetu, tunategemea waisemee serikali, tunategemea wawasemee wananchi tunawakopa na kuwaonea.

Mhe. Spika, hili haliwezekani na lazima Mhe. Waziri akubali kwamba fedha atufute kabla ya kesho, ili tuwape waandishi wa habari fedha zao, vyenginevyo Mhe. Spika Idara ya Utumishi na Uendeshaji itakuwa haina maana ya kuipatia fedha na mimi nitawashauri wenzangu sana, tena nitawashangaa sana wenzangu ikiwa watakubali waandishi wa habari waonewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa idhini yao pia tukuombe kwa vile tumeweza kuweka kanuni kando kuwaruhusu waandishi wa habari kuingia ndani ya Ukumbi huu wa Baraza la Wwakilishi, basi pia uje unikubalie kuweka kanuni kando tuwaruhusu waandishi wa habari waweze kukaa iwapo kuna haja ya kukaa. Kwa kweli Mhe. Spika, mwandishi wa habari anakaa hapa kuanzia saa 3:00 asubuhi mpaka saa 7:00 nadhani mkutano ukimaliza huu, basi waandishi wa habari wote wagonjwa.

Kwa hivyo, nikuombe Mhe. Spika, kwa idhini yako uangalie busara zako kanuni iwaruhusu wenzetu hawa kuwapatia viti pale wanapohitaji kupumzika basi wapumzike japo kwa dakika 5 au 6, vyenginevyo hatuwafanyii haki na Haki za Binadamu ziko wazi ambazo zinawafanya watu wote wawe huru na tuwasaidie. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine niseme kwamba haki ya habari Mhe. Spika ni haki ya binadamu na Katiba ya Zanzibar Mhe. Spika, imesema hivyo kwamba kila mwanadamu anayo haki ya kupata taarifa mbali mbali. Mhe. Spika, wananchi wa Pemba kwa muda mrefu hawapati taarifa za *television* na wakati mwengine hata *radio*.

Kutokana na hali hiyo, wafadhili wa Kichina wameona kuna haja ya kuwasaidia Wazanzibari kwa ujumla wao kwa kuwapatia fedha za mitambo ya *television*. Sasa leo anatokezea mtu mmoja na kuamua kununua mitambo ile kwa niaba ya serikali.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba wananchi wa Pemba wamekoseshwa haki yao muhimu kwa sababu ya kosa la mtu mmoja. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kuwa atutajie mtu huyu, kwa sababu tunajua si kosa la Wizara ya Habari, lakini kama watamfisha mtu huyu kumtaja, basi itakuwa wameshitikiana Wizara ya Habari pamoja na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kutufanyia maovu kwa wananchi.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri sana kwamba akaae na wataalamu wake pamoja na Serikali Kuu na mtueleze nani aliyechukua *tender* hii kwa niaba ya wizara yenu hadi akawaviza huduma zao pamoja na haki zao Wapemba na

Wazanzibari kwa ujumla kupata mitambo hii ya *television*. Mhe. Spika, hapa niseme kwamba ni dhahiri kuwa kuna mchezo mchafu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nikuombe tu kwamba kwa maslahi ya nchi hii, ututajie mtu aliyechukua *tender* hii akaviza mitambo hii hadi hii leo haijafungwa Pemba, wakati wewe mwenyewe umezungumza kwenye *hansard* zao kwamba ingefungwa tokea mwezi wa nne mwaka huu. Hivyo, utuambie nani aliyechuikua tender hii, ili Wazanzibari wamjue na kwa kweli ni kuombe sana kuwa hili ulifanye.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu Shirika la Magazeti. Mhe. Spika, shirika hili niwapongeze ni kweli wanatoa magazeti ya rangi tena ni mazuri. Taarifa ambazo nimefanya utafiti ni kwamba kila siku wanatumia shilingi 550,000/= na zaidi, yaani kwa mwezi ndugu zetu hawa wanatumia shilingi 22,000,000/= na mwaka wanatumia zaidi ya shilingi milioni 200,000,000/= kwa ajili ya kuchapisha magazeti Tanzania Bara.

Kwa hivyo, kwa muda wa miaka mitano Mhe. Spika kwa hesabu hiyo ikiwa kila mwaka wanatumia shilingi milioni 240,000,000/=, maana yake miaka mitano wanao uwezo wa kutumia shilingi bilioni 1.2/= na mtambo wa kuchapisha magazeti si zaidi ya shilingi milioni 700,000,000/= Mhe. Spika na serikali imeshindwa kununua.

Sasa Mhe. Waziri atuambie hapa kuna nini? Biashara hii ya nani? Kwa nini serikali ishindwe kununua mtambo huu kwa ajili ya kuwapatia wataalamu wetu hawa na badala yake magazeti haya washajihishe magazeti haya kuchapishwa Tanzania Bara.

Mhe. Spika, hili ni tatizo na lazima Wizara ya Habari au Mhe. Waziri wa Habari akubali kwamba serikali inajaribu kuwachezea wananchi, kwa sababu hatuwezi kuziidhinisha fedha na watu wakazipeleka fedha kwa watu wengine, hapa kuna ajira, kuna ushuru wa watu unapotea, yaani hapa kuna kila kitu kinapotea.

Kwa hivyo, kuchukua fedha kuzipeleka Tanzania Bara kwa kisingizio hatuna mtambo hili Mhe. Spika halikubaliki na lazima Mhe. Waziri leo atuambie kwamba kwa nini serikali inashindwa kutenga fedha shilingi milioni 700,000,00/= kwa ajili ya kununua mtambo huu.

Kwa kweli hili ni shirika na shirika maana yake linao uwezo wa kukopa, kushtakiwa na kustaki kwa nini Serikali Kuu isiwashauri wenzetu hawa kuingia mikataba na benki pengine kutafuta fedha, kwa ajili ya kutafuta mtambo huu na

badala yake waruhusu kutumia fedha za walipa kodi kiholele kwa ajili ya kuchapisha magazeti hayo.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba Mhe. Waziri nimuombe sana kuwa mtambo wa kuchapisha magazeti lazima upatikane haraka iwezekanavyo, kwa sababu ndio uchumi. Mhe. Spika, wenzetu hawa wako tayari kufanyakazi na uwezo wanao, lakini serikali kwa makusudi imeamua kuwaviza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Baraza la Kiswahili. Mhe. Spika, tutakumbuka kwamba miaka minne mfululizo tumekuwa tukiambiwa kuwa Baraza hili limekuwa lina mpango wa kuchapicha Makamusi ya Lahaja ya Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi.

Kwa hivyo, naomba kujua kwamba kwa nini hadi hii leo hawajakamilisha kazi hii na wapi wamekwama? Mhe. Spika, nadhani kuchapisha makamusi haya yatasaidia sana kukuza utamaduni wetu pamoja na Lugha yetu ya Kiswahili, lakini kuacha makamusi haya bila ya kuchapishwa nadhani itakuwa hatuwafanyii haki Wazanzibari.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningelisema kwenye TVZ ni pale mwaka juzi lilipotokezea tatizo la umeme Wizara ya Afya iliamiza janareta kwenye *Television Zanzibar* (TVZ). Kwa bahati mbaya mpaka hii leo janareta lile halijarejeshwa na wamepelekewa janareta ambayo haina kiwango. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nataka uje uniambie kwamba janareta ya *Television Zanzibar* iliyoaziomwa na Wizara ya Afya iko wapi na kwa nini haijarejeshwa hadi hii leo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye maeneo ya *Television Zanzibar* pale hupelekwa wafanayakazi wa vikosi kwa ajili ya kuchukua mazoezi ya vitendo. Lakini wakati wanapofika pale sasa inakuwa vigumu kuondoka na wanabakia pale na wanachukua nafasi za watu wengine ambao wangepaswa kuajiriwa kwa ajili ya kushughulikia maslahi ya *Television Zanzibar*.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri kwamba utaratibu wa kuwapeleka wafanyakazi wa vikosi mbali mbali, kwa ajili ya kufanya mazoezi ya vitendo na baadaye wakageuza kuwa ndio sehemu yao ya ajira nadhani ungezingatiwa, kwa sababu unawanyima watu wengine kupata haki ya ajira. Mhe. Waziri suala hili aliangalie na anisaidie.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu Bwawani wametuomba shilingi milioni 800/=, lakini Mhe. Waziri hakutwambia wao wanakusanya kiasi gani, maana wananchi watoe shilingi milioni 800, bila ya kuambiwa wanafanya biashara gani, Mhe. Spika, nadhani hiyo si busara. Kwa hivyo, lazima Mhe. Waziri

atuambie shilingi milioni 800/= ambazo Baraza la Wawakilishi litaidhinisha wao Hoteli ya Bwawani inazalisha kiasi gani cha fedha kwa mwaka, kwa sababu hatuwezi kutoa fedha na baadaye hatujui faida yake.

Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri atupe ufafanuzi wa kutosha kama wenzangu walivyozungumza, ili Wazanzibari waweze kujua uhalisia wa mambo.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba Baraza hili ndio dhamana wa maslahi na maisha ya Wazanzibari na Wizara ya Habari ni muhimu sana. Kwa kweli Wizara ya Habari ndio yenye haki ya kulinda na kusimamia utamaduni wa Mzanzibari. Mhe. Spika, lazima tukubali kwamba Wazanzibari utamaduni wao unaondoka kwa kasi sana, unaondoka kwa sababu ya utandawazi pia kwa serikali yenyewe haijakusudia kusimamia Utamaduni wa Mzanzibari.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri kwamba yeye ndiye mwenye dhamana ya suala hili kwa kipindi hiki basi ninamuomba sana asimamie masuala ya utamaduni, ili Wazanzibari hasa vijana yasimong'onyoke maadili yao kwa sababu ya utandawazi na tamaduni za nje.

Mhe. Spika, nimalizie kusema tu kwamba, hotuba hii inahitaji kuungwa mkono, lakini haiungwi mkono tu kwa sababu ya kusema, isipokuwa tunaomba hoja zijibiwe.

Kwa maana hiyo, niseme tu kwamba Mhe. Waziri iwapo atanijibu hoja ya wafanyakazi kuhusu maslahi yao na wenzangu watakubaliana kuwa Idara ya Utumishi na Uendeshaji tupunguze fungu, ili wafanyakazi wapewe fedha zao na kama atanijibu fedha kuhusu mtambo wa Pemba, basi nitaunga mkono hoja hii, lakini kwa sasa nabakisha hoja yangu siungi mkono mpaka nipatiwe majibu yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Ahsante sana Mhe. Spika, nami kwa kunipa nafasi ya jioni ya leo. Vile vile nachukua nafasi hii kumpa pongezi ndugu yangu Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa uwasilishaji wake makini kabisa. Pia nachukua nafasi hii tena kumpa pongezi Mhe. Naibu Waziri wajibu kwa kuweza kutujibu maswali yetu kila tunapomuuliza hapa. *(Makofi)*

Kwa kweli bila ya kuwasahau watendaji wakuu wa wizara hii pamoja na watendaji wengine kwa namna moja au nyengine walivyoweza kumuwezesha Mhe. Waziri kumsaidia mpaka akawasilisha hotuba yake nzuri hapa. *(Makofi)*

Sasa moja kwa moja niende katika ukusara wa 17 kuhusu Shirika la Utangazaji. Mhe. Spika, dhamira nzuri sana ya serikali na hatuna budi sote kuipongeza

kutoka katika idara kwenye kwenye shirika hiki ni kitu muhimu tena bora zaidi na tumeona jinsi gani wenzetu wanavyoendelea. Kwa hivyo, ninawapongeza sana na pia watu walioteuliwa hapa nafikiri Mhe. Rais ameona hapa, kwa sababu mimi ninawaamini sana. *(Makofi)*

Kwa mfano, Mhe. Spika hivi karibuni tumeona *television* yetu tunakwenda *live* katika Baraza letu hili la Wawakilishi. Kwa kweli huu ni ukuzaji wa demokrasia, wananchi majimboni mwetu wanatuona jinsi gani tunavyoweza kuchangia pamoja na kuwatetea. Kwa hivyo, hili ni jambo zuri sana na niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, panapokuwa na mafanikio basi lazima pawe na changamoto katika hili shirika letu. Mhe. Spika, kuendesha kitu kama hiki *live* si kitu cha mas-hara, kwa sababu uzoefu unaniambia kama kule Bungeni *TBC* inalipwa zaidi ya shilingi milioni 9/= kwa mwezi, kwa nini wawalipe kwa sababu kipindi hiki hakina wadhamini.

Sasa moja kwa moja TVZ tunapaswa na mimi ningeshauri basi Baraza nalo lichangie, ili lipunguke na makali haya ya umeme. Kwa mfano, hivi karibuni tumesikia Redio Zanzibar wamekatiwa umeme, hivyo tupunguze na kadhia kama hii, ili tuweze kuwalipa.

Vile vile kuhusu vifaa vya utangazaji hawana na walivyonavyo ni vibovu *camera* zenyewe ndio mtihani mtupu *cassette* hatuna, sasa lazima vijana wetu tuweze kuwafikiria wanakaa masaa mengi hapa bila ya kufanya kitu chochote.

Mhe. Spika, sasa nije ukurasa wa 21 kuhusu Idara ya Habari Maelezo. Kwa kweli serikali idari hii ndio jicho lake kubwa hata kwenye ibara ya 18 katika Katiba yetu ya Zanzibar imo na wala sitoweza kunukuu kwa sababu ya kujali muda wako Mhe. Spika. Kwa kweli idara hii ni muhimu sana, lakini ukweli inakabiliwa na changamoto nyingi sana.

Kwa mfano, idara haina vitendeakazi, vipaza sauti vibovu, tukizingatia hivi sasa tunao watendaji Wakuu Watatu katika Serikali yetu, sasa hawa tunaweza kuwalaumu ikifika siku ya wakati, kwa sababu wanaweza kutuwekea vipaza sauti vikalia kama mbuzi pale kumbe sio wao na vile ni vipaza sauti vibovu. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri akija atueleze lini atatununulia vipaza sauti vile au wamejipanga vipi?

Mhe. Spika, hata ile Maktaba yetu pale ni mbovu ya kuhifadhia picha za viongozi wetu, yaani mpaka hivi sasa wanadiriki picha za Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwenda kukopa kule nje, katika kupita kamati yangu iliangalia hawana kabisa Picha za Viongozi Wakuu, sasa wanakwenda kukopa na

wanashindwa kulipa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utuambie utawawezesha vipi katika Idara ya Habari Maelezo, ili tuepukane kabisa na changamoto hizi.

Kwa kweli hata katika suala la usafiri wanakosa hawa, yaani wanakabiliwa na changamoto nyingi sana. Mhe. Spika, naiomba serikali kwa dhati kabisa iweze kuiongezea bajeti yao, kwa sababu bajeti ni ndogo na wala hawatoweza kufanya chochote na huu ndio uso wa serikali. Kwa mfano, ukienda kwenye Chumba cha Habari pia kuna mtihani mtupu, kama vile kuna *computer* mmoja ndio inayotumika na hiki sio kitu kizuri. Kwa hiyo, tunaomba wizara ijitahidi, ili kuweza kuboresha kazi hii.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nakwenda kwenye ukusara wa 24 kuhusu Shirika la Magazeti. Mhe. Spika, jitihada za serikali zinaonesha wazi, mwanzo kabisa tulikuwa tukitumia magazeti meupe ambayo tulikuwa wasi wasi kabisa kwamba macho yetu yanaweza kufa mara moja.

Lakini kipindi hiki kizuri magazeti yale yana rangi tena yanavutia, yaani unaweza kuyasoma kwa muda wote bila hata kuchoka. Kwa hivyo, nampongeza sana Mkurugenzi kwa jitihada zake alizozifanya mpaka kufikia pale. Hivyo, namuambia aendee na ashike uzi huo, ili tuendelee zaidi.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye ukurasa wa 29 kuhusu Tume ya Utangazaji. Pamoja na nia nzuri ya serikali Mhe. Spika tunapaswa tuviboreshe vyombo vyetu hivi vya utangazaji, ikiwemo Sauti ya Tanzania Zanzibar. Kwa mfano, kule mitaani wanasema biashara yoyote inayotangazwa na Sauti ya Tanzania Zanzibar ndio inayotoka. Kwa hivyo, tujitahidi sana ili kuviendeleza.

Vile vile kuna vyombo binafsi ambavyo ni vingi. Kwa mfano, kuna *Coconut FM, Zenji FM* pamoja na vyengine vyote ni vizuri, kwa sababu pale wanatutangazia michezo kama vile ile *Coconut FM* na mwenyewe anajiita Mkurugenzi wa Fitina, kwa kweli yule kijana ni hodari na tunaweza kupata kipaji kizuri siku za mbele pale kwa jinsi anavyotutangazia ile michezo ya nje na ndani.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa niende kwenye Chuo cha Uandishi wa Habari. Kwa kweli naipongeza sana wizara kwa uamuzi uliochukua hivi sasa wa kuanza kusomesha *Diploma*, *Certificate* pamoja na Darasa la Kichina pale chuoni. Kwa mfano, zamani tumezoea kusikia wataalamu wanatoka Chuo Kikuu na Zanzibar tunapata wawili.

Kwa kweli hivi sasa tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa sababu Zanzibar yetu ni njema tunaweza kupata waandishi wengi kwa mara moja. Hivyo, hii ni dhana nzuri ya serikali na tunaipongeza idara pamoja na wizara kwa kuweza

kuchukua hatua madhubuti ya kutusomeshea waandishi na watangazaji wetu kwa pamoja.

Mhe. Spika, nataka kushauri tu, kwamba vyuo hivi lazima viwe na sauti moja, yaani viweze kuwa na sauti moja ya kuweza kuunda chombo chao cha pamoja, kwa ajili ya kuwa na sauti ya kuweza kuwasemea pahala popote pale. Kwa hivyo, huu ni bora zaidi katika vyombo vyetu hivi.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 35 kuhusu Kamisheni ya Utalii. Kwa kweli hivi sasa tumeondoka katika utalii kuondoa Sera hii yetu kubwa na tumeingia katika Mapinduzi ya Kilimo. Mhe. Spika, nataka kuishauri serikali pamoja na kuingia kwenye Mapinduzi ya Kilimo, basi bado tuweze kuendelea na utalii, kwa sababu visiwa vingi kama hiki chetu vimepata mafanikio mengi kupitia utalii. Hivyo, nadhani kama Mhe. Waziri ataweka sera madhubuti basi tunaweza tukatoka na huu utalii na kutuweka katika hali nzuri zaidi kuliko kuuacha wazi.

Mhe. Spika, takwimu zinanionesha kuwa asilimia 40 ya ajira zinapatikana kwenye Sekta ya Utalii ambazo ni rasmi, asilimia 45 ni ajira zisizorasmi kama vile watu wa masikiti wanavyouza bidhaa zao. Kwa hivyo, hii inatuonesha wazi kwamba bado Utalii ni Uti wetu wa Mgongo na wala tusiuache kabisa tukaingia kwenye Mapinduzi ya Kilimo. Kutokana na hali hiyo, ni vyema kuendelea nao na utatusaidia.

Mhe. Spika, pia nizungumzie kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Utalii kwenye ukurasa wa 39. Mhe. Spika, ni dhahiri sasa tunaona wazi kuwa tunapata wataalamu wengi ingawa Waheshimiwa Wajumbe wengi wamechangia wanasema sio ajira nyingi zinazopatika. Kwa kweli mimi ninasema ajira nyingi tunapata, kwa sababu tumetembelea mahoteli mbali mbali hivi sasa na vijana wetu wengi wanafanyakazi za hoteli, sasa panapokuwa na raha na matatizo yanatokea.

Lakini tujitahidi ili tuweze kuweka sera zetu imara na Mhe. Waziri utusaidie, ili tuweke sera zetu kuwa madhubuti mpaka tuweze kumubu hili suala la matatizo liweze kupungua, kwa sababu haliweze kuondoka kabisa, lakini linaweza kupungua kiasi cha kuweza kutia moyo.

Sasa nije Hoteli ya Bwawani. Mhe. Spika, hoteli hii ilikuwa na matatizo mengi, ni kweli kabisa na tunakiri. Lakini hivi sasa hoteli hii iko katika hali nzuri, yaani asilimia 80 ya wafanyakazi wa pale wamepata mikataba. Kwa kweli tunampongeza sana Mhe. Waziri kwa hatua zake zote alizochukua yeye pamoja na watendaji wake wakuu. Kwa hivyo, mimi namuambia hii asilimia 20 iliyobaki baada ya miezi miwili basi matumaini yetu itakuwa imekwisha.

Mhe. Spika, pale Hoteli ya Bwawani kuna *Laundry* na mikataba yake hatujaijua. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho hapa, atueleze kuhusu mikataba hiyo imekwenda vipi na serikali inaweza kufaidika vipi?

Mhe. Spika, hivi karibuni hoteli ya Bwawani ilinunua vespa mbili, vespa zile zilisajiliwa kwa namba za Private, sasa atwambie Mhe. Waziri hizi ni za watu binafsi au hizi ni za hoteli yenyewe kwa kuimarisha usafiri wa wafanyakazi wake.

Mhe. Spika, nije kwenye ukurasa wa 64 Baraza la Michezo. Mhe. Spika, baraza la Michezo ni zuri zaidi na sisi tunalipongeza kila mara tunaoposimama hapa, mimi nije tena kwenye Uwanja wa Mao tse Tung wenzangu wengi walijaribu kuzungumzia juu ya suala hili lakini uwanja ule ukweli ni mbaya, mbovu juzi tulicheza mechi pale na mimi mwenyewe nilikuwa namba nne wa Baraza lako hili. Lakini kuna namba sita wangu mmoja Mhe. Abdalla alipata majeraha kwa ule uwanja mgumu sio uwanja mzuri, sasa tunaomba Wizara iweke sera maalum za kuwasaidia ZFA ili kuweza kuujenga kwa haraka ule uwanja wetu.

Mhe. Spika, serikali ya Jamhuri ya Muungano ilipoona chama cha Mpira TFF hakiendi vizuri kiliamua kukipangua wao wenyewe na kuunda chama kipya, sasa tunaiomba Wizara basi kama itaona ZFA haiwezi kuendesha michezo vizuri iweze kuipangua na kuwa na timu bora, hatuwezi kuwa na timu bora ya kufaya *junior Academy* mimi ninaamini Zanzibar tuna vipaji vizuri sana na kama tutafanya *junior Academy* basi sisi tunaweza kuwa na timu bora ya taifa, hakuna nyumba inayoaanza tu moja kwa moja lazima atuanze na *foundation.*

Sasa Mhe. Waziri ningekuomba ufanye *junior academy* ili tupate wachezaji wazuri wenye sifa tele, naamini ukifanya hivyo tunaweza kufikia pale malengo yetu tulipoyataka, lakini sio kwa kufanya *academy* ya wachezaji tu vile vile tunahitaji kusomesha na makocha wetu makocha wetu waliopo sasa hivi nimecheza mpira na mimi nitafundisha, lakini tunataka wapewe mafunzo ya kutosha ili waweze kumudu kwenye ushindani huu wa kimataifa.

Tunampongeza sana Mhe. Waziri kwamba juzi alitutangazia wanamichezo wetu wa karati wamerudi na wamerudi na ushindi hivyo ndio tunavyoona kama vipaji vimekuja kwetu kabisa.

Mhe. Spika, mimi nije kwa wafanyakazi waandishi pamoja na wafanyakazi wa wizara hii, waandishi wengi wamekuwa na matatizo mazito wanaweza kukaa hapa kutwa nzima posho hawapati hata yale maji ya kunywa wanashindwa kupewa, sasa namuomba Mhe. Waziri basi wakikaa hapa wawafikirie hawa

watendaji wake ili waweze kufikia katika hali nzuri kabisa, mimi sina budi kumpongeza Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya wizara hii na watendaji wake wote wakubwa, ukweli wizara wamerithi na walirithi wizara yenye matatizo kidogo. Lakini sasa kwa asilimia hamsini matatizo yale yameanza kupungua .

Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi kwa niaba yangu na wananchi wa Mpendae naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak:** Ahsante sana Mhe. Spika, nami kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na uzima kwa jioni hii ya leo na kufika katika Baraza lako tukufu kutekeleza majukumu yetu tuliyotumwa na wananchi. Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nami niteue mchango wangu mchache katika Wizara hii ya Habari Utamaduni na Michezo.

Mhe. Spika, basi na mimi nisiwe mwingi wa fadhila nimpongeze basi Mhe. Waziri kwa pongezi zote na nimpongeze pamoja na watendaji wa vyombo vya habari, kwa sababu ile kiu yetu tuliyokuwa nayo miaka iliyopita takriban baraza la saba tulikuwa tuna kelele na kiu kubwa kwamba mjadala wa bajeti uonyeshwe katika vyombo vya habari, leo matumaini yetu kiu ile imepungua au imekatika. Kwa hivyo pongezi hizo naomba Mhe. Waziri azichukue pia ziwafikie watendaji wake.

Mhe. Spika, mimi nianze katika idara ya makumbusho na nitazungumza katika magofu Mhe. Spika, Mhe. Waziri kumekuwa na uvamizi mkubwa wa maeneo ya magofu magofu yetu yanavamia, basi ningelimuomba Mhe. Waziri afanye utaratibu wa kupatiwa hati miliki ili kuondosha usumbufu huu wa kuvamiwa, kuna gofu la Bungi ambalo maarufu gofu la Bihole, gofu hili linasemekana kwamba kuna uvamizi ambao umetokea. Ningemuomba Mhe. Waziri basi afanye ziara ya kwenda kuliangalia hili gofu na pia magofu yote yaliyokuwa hayajapatiwa hati miliki yaweze kupatiwa ili huu usumbufu wa kuvamiwa vamiwa na wananchi usitokee Mhe. Spika.

Mhe. Spika, niende katika sehemu ambayo tunaizungumza kila siku na tunaendelea katika mijadala ambayo hatujui hatima yake itakuwaje, lakini tumo katika mijadala nakumbuka siku zote tuna kilio cha utamaduni kutoweka hichi ni kilio chetu Wazanzibar na hatujui hatima yake itakuwa nini. Nadhani nisingelitaka kuchangia sehemu hii lakini imenibidi nichangie imechangiwa vya kutosha Mhe. Ismail Jussa asubuhi kachangia vizuri, Mhe. Panya kachangia vya kutosha kwa hivyo na mimi haitokuwa vyema kwamba na mimi muumini mkubwa wa masuala ya kuenzi utamaduni wetu. Kwa hivyo itakuwa si vyema nami kama sikutoa mchango wangu Mhe. Spika, utamaduni wetu tukitaka tusitake unapotea kwa nguvu na unatuweka vya kutosha, tutafute basi

sababu gani zinazofanya kupotea kwa utamaduni wetu na kutoweka kwa nguvu.

Mhe. Spika, kinachosababisha vitu vyote viko wazi na hatuwezi kuviepuka Mhe. Spika, kwa hali iliyopo ya utandawazi uchangia kwa sehemu yake, haki za binaadam zinachangia sehemu yake, sifikirii leo mtu anakwenda uchi kumkuta katiwa mikwaju utaambiwa unavunja haki za binaadam, kwa hivyo haya ni mambo ambayo Mhe. Spika, yanachangia vya kutosha. Kwa hivyo sijui Mhe. Waziri atakuwa na miujiza gani yeye ya kupita hata tuone kwamba huu utamaduni wetu unarejea au utamaduni wetu unabakia kama asilimia dhama hautoweki, sijui Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri ambae mwanamke.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipata safari hivi karibuni alikwenda Iran lakini alivyorudi tu hapa Mhe. Spika, mimi wa mwanzo nilimdaka hebu tueleze umepata nini, kwa alivyokuwa muumini mkubwa wa utamaduni alitueleza utamaduni wa Iran alioukuta kule jinsi ya wenzetu wanavyothamini utamaduni wao, jinsi wanavyojali utamaduni wao. Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa kweli alitueleza kitu ambacho alikikuta kule wala hawakujali kwamba wameingia wageni tayari wabadili utamaduni wao hawakuona walikaa na utamaduni wao ule ule.

Mhe. Spika, anasema kitu kikubwa ni kwamba mwanamme yoyote hampi mkono mwanamke, basi ananieleza vile ambacho kitu hicho na mimi nasema ukweli kinaniuma sana, hupata masuala mengi huulizwa najua ni utamaduni wetu wa Zanzibari kweli si rahisi tu mtoto wa kike kuwa anakumbatia kumbatia wanaume tu hivi hivi, kwa hivyo mimi nadhani suala la utamaduni nnavyohisi tutakuwa tunalizunguza kubakia kwenye kumbu kumbu kwenye Hansard, kubakikia kwenye vitabu lakini kuondoshwa kwake je wakati tumekabiliwa na mambo haya kweli hii tutaweza kubaki na utamaduni wetu ubakie au turejeshe ule utamaduni wetu leo wa asili.

Mhe. Spika, leo utakuta kuna vitu vya ajabu vinauzwa si utamaduni wetu kukuta vitu vya ghaibu nadhani nikizungumza hivyo tunafahamu vitu vya ghaibu kutandazwa hadharani kuuzwa sio utamaduni wetu, vitu ambavyo vinauzwa wakati wa wazee wetu vilikuwa vinauzwa kwa siri sisi watoto hata kina mama Asha wakati huo watoto walikuwa hawajui vitu hivyo, mpaka ukifika wakati wao ndio wanavijua. *(Makofi)*

Lakini leo unavikuta vinatandazwa hadharani jua kali hapo ule sio utamaduni wetu Mhe. Spika, hata kidogo ndio maana tunafika wakati tunawakuta wanafunzi wa skuli, hivi sasa wanafunzi wa skuli kuna mama mmoja siku moja niko harusini anahadithia mtoto kainama hivi kava kishati na kisketi basi anamuona na vitu vya ajabu, mtoto mwari wa skuli nini kilichotupelekea hivyo

kwa sababu vinauzwa hadharani. Basi sijui Mhe.Waziri hali hii itarekebishika vipi tuone kwamba vitu vya ghaibu visivyostahiki kutandazwa hadharani visiwekwe hadharani.

Mhe. Spika, nije katika sehemu ya michezo kuna vifaa vya michezo ambavyo vinauzwa ghali sijui Mhe. Waziri ana mpango gani kurejesha duka ambalo lilikuwa likiuzwa vifaa vya michezo, nakumbuka duka hili lilikuwa lipo Amani kwa sababu leo kuwaachia wafanya biashara wanauza wanavyotaka wenyewe na michezo hivi sasa ni kitu ambacho kipo kinaimarika kila usiku ukicha, vifaa hivi vimekuwa ghali sijui Mhe. Waziri au Serikali ina mpango gani wa kurejesha lile duka ambalo lilokuwa la serikali lililokuwa likiuza vifaa hivi ili waweze kuuziwa wananchi vifaa hivi vya michezo vilivyo hafifu, wanamichezo wetu waache kuvaa vile viatu vya raba vinavyoitwa raba ya Abeid Mziba.

Mhe. Spika, jengine tunakuja katika viwanja vya michezo, viwanja va michezo hususan vilioko katika vijiji vyetu navyo havina hati miliki, kwa kweli ni usumbufu leo kesho na keshokutwa nina imani kutakuwa hakuna viwanja vya michezo kila mmoja atachukua haki yake, kwa hivyo navyo hivi sijui una mpango gani Mheshimiwa, viwanja hivi tukitizama Bungi pale pana kiwanja cha michezo, lakini ukenda kuuliza pale hawana hati miliki, Binguni kuna kiwanja cha michezo na mwengine. Sijui Mhe. Waziri ana mpango gani kila wilaya kujenga kiwanja ambacho kimezungurushwa uzio ili kuwa kiwanja madhubuti cha michezo.

Mhe. Spkika, jengine mwaka 2006/2007 mimi nilikuwa mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, mwaka 2007/2008 nilikuwa mjumbe wa kamati ya Ustawi wa Jamii, 2009/2010 mjumbe wa kamati ya ustawi wa jamii. Mhe. Spika, wakati nilipokuwa kwenye kamati hiyo tulikuwa tukifanya ziara zetu Pemba, Unguja na tulipokwenda Pemba tulikuta matatizo ya viwanja vya kufurahishia watoto, nilitarajia kwamba kwenye bajeti yake hii atakuja kutueleza jinsi ya kuboreshwa viwanja hivi. Tatizo moja nililolikuta ni kwamba na kamati ikatoa maelezo yake kwamba viwanja vya kufurahishia watoto viimarishwe, kile kiwanja cha Pemba kiko hali mbaya na tukasema kwamba kiimarishwe kwa kuwa ionekane kuwa kuna Pemba mpya, sababu watoto wetu leo tunasema tuko mwezi wa Shaaban, Ramadhani na siku za kufurahi watoto ni mfunguo mosi na mfunguo tatu, sijui watoto wetu furaha hizi zitaishia wapi.

Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri aje atueleze je, viwanja hivi bado yale maoni ya kamati zilizopita yalichukuliwa ili kuimarishwa viwanja hivi, au hivi viwanja ndio basi au vimeshaimarishwa pia tupate taarifa hiyo, tuone basi ili watoto wetu tujue ishaalla Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai na uzima mfunguo mosi wanapo pa kwenda kukonga nyoyo zao.

Mhe. Spika, nadhani bajeti hii tokea asubuhi inachangiwa na mengi yameshachangiwa yale ambayo yamechangiwa sitaki kuyarejea, lakini tu na mimi nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sikuwatetea ndugu zetu hawa ambao wamesimama tokea asubuhi. Kule kusimama kwao Mhe. Spika, mimi niwapongeze hodari sana wanasimama mwanzo wa asubuhi mpaka saa 7.00, saa 11 mpaka saa mbili kasorobo tuwaonee huruma kusimama kule kuna vitu vinapungua katika maungo yao *(Makofi).*

Namuomba Mhe. Waziri, hakuna kazi isiyochokesha naomba tuwajali ndugu zetu hawa, tuwajali tuwatizame na tuwaonee huruma mimi nadhani kwa huruma tuliyonayo kwa ndugu zetu hawa, mimi ningekuwa na maarifa mamoja kama Wizara imeshindwa kuwalipa hawa basi nadhani wakatwambia sisi wawakilishi tukawalipa, kwa ile huruma tunayowaonea, kutwa wamesimama labda mtu angojee muazini atoke akatekeleze ibara ikesha anarudi kasimama vile vile kazi kubwa Mhe. Spika, kwa hivyio tuwaoneeni huruma, tuwatizameni tuwapeni kinachostahiki kupewa nadhani kelele hizi baraza la saba wajumbe wengi walikuwa wakipiga kele juu ya ndugu zetu hawa.

Kuna hadithi inasema hutokuwa muumini kama hukumpendelea ndugu yako kwa yale unayoyapenda wewe, kwa sababu sisi hatutokubali na sisi kukaa hapa bure na wale basi tuwapendelee yale tunayoyapenda sisi, kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba kwa hili panga pangua punguza huku na kule Mhe. Hija Hassan Hija katoa ushauri tuukubali ushauri ule na mimi naunga mkono kwa lile ili tuwatizame ndugu zetu hawa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nami naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja nakushukuru Mhe. Spika, *(Makofi)*

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwanza nianze kwa kusema kwamba nimshukuru yeye Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Mhe. Waziri umerithi lakini umerithi rasilimali nzuri wizara hii ni wizara ambayo imekusanya vyombo vya habari na tumesema kwamba vyombo vya habari vinaimarisha na kutoa burudani na pia vinatujulisha mambo mengi tu yanayotokea.

Mhe. Spika, nijirabu sana kupitia wizara hii ndio wizara ambayo nilianza kazi ingawaje ilikuwa kwa vipande vipande, nilianza kazi nikiwa mila utamaduni ambayo ilikuwa na mambo ambayo ilikuwa na wizara hizi za utamaduni ambayo imekusanya mila sanaam,na Idara ya Michezo, Kadiri nilivyokuwa nikiendelea mbele ikawa hii wizara inabadilka badilika lakini bado ilikuwa nipo pale, imebadilika baada ya muda mfupi ikawa Wizara ya Habari

Utamaduni, na Televisheni ambayo ilikuwa inachukua pamoja na redio na televisheni na magazeti haya. Kadiri ilivyokuwa inakwenda mpaka ikaingia na uchapaji na mambo mengine lakini kwekweli hii wizara ni nzito na ngumu. Lakini hata hivyo Mhe. Waziri nimwambie kwamba ana vianzio vingi tu vya mapato.

Nikianzia kwenye habari kwa kweli vyombo vyetu vinajitahidi lakini Mhe. Spika, niseme kwamba bado vyombo hivi vinataka kuingia kwenye ushindani, sasa hivi televisheni kwa kweli inaonyesha vipindi lakini bado twendeni na ushindani kwa vile vyombo vingine vilivyoanzishwa katibuni tu kama TV zimeanza vizuri na wameongeza muda na kuwa masaa 24. Kwa hivyo na sisi tuendeni huko sasa hivi tujenge ushindani wa vyombo vya habari, mimi nasema serikali ielekeze nguvu zake zote kwanye vyombo hivi na tunajua kwamba tatizo ni pesa mambo yote haya yanataka pesa, tuvitizame vyombo hivi ili viweze kusaidia kwa sana serikali iwape pesa za kufanya mambo hayo.

Kuna mambo mengine yanawezekana kuyafanya mara moja kwa kuonyesha ule utendaji wetu wa kazi uliokuwa mzuri, kwa bahati tunapata mambo mazuri mazuri kutoka kwenye misaada mbali mbali, lakini sisi wenyewe baadae tunashindwa kuyaendeleza tumejengewa jengo la Sauri ya Tanzania Zanzibar pale kwa muda mfupi tu, baada ya kukabidhiwa tunaliona jengo lile sasa hivi linapoteza ile haiba yake. Huku barabarani sisi tunasema ni nyuma na kule mbele naona limekaa kinyume nyume kusema kweli.

Sasa ukipita huku nyuma gugu lilioko pale linasikitisha sasa haya yote tunasema na utendaji nao tujitahidi, ukilitizama lile jengo sijui kama tokea tulipokabidhiwa sijui kama limetiwa rangi au vipi, ukipita imeshaanza kuchipua mipapai kule nyuma naliona. Kwa hivyo hii namna gani inavyoonyesha kwamba tuwe na kubuni mambo au mambo ambayo tunayaona, tukishakabidhiwa basi sisi wenyewe tuwe waangalifu wa haya masuala wale wakija tena pale kutusaidia wakiona mambo yale sijui itakuwaje.

Mhe. Spika, tuende vile vile na magazeti, kwa kweli gazeti nalisifu sana. Sasa hivi tunalisikia gazeti kwenye vyombo vya habari vya wenzetu linatangaziwa, lakini hata hivyo linataka kuboreshwa kiasi fulani kwa kulipia angalau rangi, bahati nzuri naambiwa limeshaanza kutiwa rangi. Kuna hii *Adobe photoshop* ambayo inatengeneza *news paper* na kalenda, ambayo hata Chuo cha Utumishi wanatoa mafunzo hayo.

Kwa hivyo nafikiri Mhe. Waziri aweze kuchukua fursa ya kuwapeleka hawa wachapishaji wa magazeti ili wakasome hapo, wala hawatosoma nje kwa sababu kama lengo ni kuuza magazeti kama wenzetu, kwa sababu magazeti ya wenzetu yanavutia vizuri.

Mhe. Spika, suala jengine ni utamaduni kama walivyokwishasema wenzangu kwamba utamaduni ni moja ya kigezo cha mtu katika nchi yake. Kwa kweli tumeanza kupoteza silka, mila zetu na utamaduni wetu. Mhe. Spika, tumeanza kuiga mambo ya nje zaidi ambayo siyo yetu.

Mhe. Spika, zamani mwanamke kulikuwa na mambo yalikuwa huyaoni, kama mwanamke kupita ukala njiani kwa kweli sio vizuri. Kwa hivyo, na mimi niseme kwamba haya ni matatizo ambayo sisi tunajipotezea haiba na ule uzuri wetu wa Mzanzibari.

Mhe. Spika, nikija na suala la utalii kwa kweli tunasema ni uti wa mgongo wetu na kuna mambo mengi ambayo hapa yanatoa mchango mkubwa kwa pato letu la serikali. Kwa hivyo, kuna mambo kama tumekubali kwamba ni uti wa mgongo wetu, basi ni lazima tushughulike na tuone huu utalii tutauendeleza kutokana na hali ya nchi yetu. Mhe. Spika, utalii sasa hivi tumeona mji wetu kwanza unatia aibu kiasi fulani, mji unakuwa mchafu, mle kwenye maeneo ambayo ya utalii ya kwenda kutizama mambo ya utalii sehemu hizo zimekuwa ni chafu sana.

Mhe. Spika, kama tunataka utalii uendelee na uwe ni chanzo cha mapato katika taifa letu, basi ni lazima tulione suala hili na tulitilie mkazo ili mambo haya madogo madogo yaondoke.

Mhe. Spika, kwa kweli michezo ni muhimu na michezo ni ajira pia michezo ni afya. Nasikitika sana Mhe. Spika, kwamba safari hii nimesikia huu mpira uliochezwa juzi Bara wa *CECAFA* ilikuwa ni zamu yetu kwa sababu kila mwaka tunakuwa na mabadilishano, mwaka huu inakwenda huku nafikiri ni nchi zote zile ambazo zimo katika *CECAFA*. Lakini safari hii ilikuwa ni kwetu sisi.

Mhe. Spika, mimi nauliza kwa nini haukuchezwa hapa? Naambia tatizo ni pesa. Mhe. Spika, kwa kweli serikali iyatizame mambo haya kwani ni mambo muhimu na yanatia pesa katika nchi yetu. Nakumbuka mimi kama nilivyokwambia Mhe. Spika, kwamba wizara hii mimi nilikuwa nayo kwa muda mrefu na nimefanya kazi, nilikuwa najua mambo yote ambayo yalikuwa yakikaribia katika *CECAFA* namna gani mikakati inachukuliwa kutokana na viongozi ambao waliokuwepo pale na wengine wapo hapa hapa ndugu Bakari Mshindo ni mtu ambaye wizara hii anaijua.

Mhe. Spika, leo yupo pale nafikiri mheshimiwa anaweza akakaa nae ili apate kujua ni mikakati gani ambayo walikuwa wakiichukua na kufanikisha mambo haya. Kwa kweli inasikitisha sana kusema kwamba sasa hivi baada ya michezo

kukua inaporomoka. Mhe. Spika, niseme kwamba kweli michezo ni afya, michezo ni ajira na michezo ni kila kitu.

Mhe. Spika, nimemwambia Mhe. Waziri kwamba hapa ana wizara ambayo ina mapato mengi na pia kuna maeneo mengi. Vile vile kuna maeneo mengi za magofu kama vile kwa Bi Hole, kuna gofu kule Fukuchani na kuna eneo moja kuna shimo ambalo naambia ni la kwenye karne ya 17, kulitokea upepo mkali likakatika gogo lipo pale na mpaka leo maji yak masafi nafikiri kupitia kwa Mkurugenzi aliyekuwepo hapa wa mambo ya kale anaweza siku moja labda akatualika tukenda tukaona mambo mbali mbali ambayo yaliyotokea huko.

Mhe. Spika, hili suala la mambo ya kale haya ya *theology* kuna wataalamu wazuri ambao tunao, lakini sasa hivi kutokana na hali hii ya kwamba hamna fedha, hamna maslahi mazuri, wengi wameshakimbia, wengine wako Bara wanafanyakazi kutokana na hali ya kutokuwa na fedha. Mhe. Spika, serikali itizame watu kama hawa tunakuwa na watu wazuri lakini baada ya muda tunakosa kwani wanakuwa wanakimbia wanakwenda sehemu mbali mbali kutokana na maslahi yao. Mhe. Spika, niseme kwamba wizara hii sio masikini, wizara hii ni tajiri.

Mhe. Spika, vile vile niende kwenye ukurasa wa 65 kuna kituo hiki cha Eacrotanal ambacho hiki na mimi enzi hizo nilipokuwa Mila na Utamaduni pia kituo hiki kilikuwa chini ya wizara hiyo ya mila na utamaduni. Mhe. Spika, sijui kwa nini ikafikia *stage* kwamba sasa hivi kimekufa na sasa hivi kinataka kufufuliwa. Mhe. Spika, ni kwamba ndio kama yale niliyosema mwanzo kuwa tunaanzishiwa mambo lakini sisi wenyewe kuyaendeleza yanakuwa magumu.

Kwa kweli hiki kituo kama alivyosema Mhe. Waziri kulikuwa na hizi kama za Burundi, Commoro, Ethiopia, Madagasca, Mouritius, Msumbuji na Somalia. Sijui kwa nini ikawa leo kimefikia hadi yakuwa kimekufa, nashangaa Mhe. Spika, kwa sababu hawa ni wanachama wote sisi tungekuwa ni endelevu, baada ya kukiachia kikafa ingekuwa kila baada ya muda tunawasiliana nao hawa watu. Mhe. Spika, tungekuwa tunawasiliana nao na halafu tunagawana madaraka, kwa sababu hawa nakumbuka kuna kipindi alikuwepo hapa huyu mtu wa Madagasca ndiye aliyekuwa *director* wa hii idara. Kwa hivyo, sisi kama tukijiachia huwa tunaachiwa mambo kama halafu tunayaachia kwa hilo Mhe. Spika, maisha itakuwa tuko nyuma nyuma na hatutokuwa tunaendelea mbele kwa matatizo kama haya.

Mhe. Spika, ni lazima tuwe watendaji wazuri na tuwe na mikakati mizuri, kila siku tukisema kwamba tuwe hivi hivi mambo haya kwa kweli yanarudisha nyuma hatutokomaa hata siku moja. Mhe. Spika, kila siku tutakuwa wachanga na sijui sasa hivi tutasema nini, tulikuwa tukisema serikali bado ni changa,

lakini sasa hivi sijui tutasemaji. Mhe. Spika, kwa miaka hii tuliokuwa nayo mimi nikisema kwamba nina miaka 52 ndio nitasema ni mchanga, sijui tena lini nitapea.

Mhe. Spika, jengine kuhusu Hoteli ya Bwawani kwa kweli ndio kama yale yale niliyosema ile hoteli ni nzuri, lakini hata kuitia rangi ndio tunashindwa. Mhe. Spika, kwa nini hatuyaendelezi haya majengo tukayafanya yakawa mazuri na yakavutia. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naona bado tungali tuna matatizo na sijui ni matatizo gani. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kutokana na hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa kweli ni nzuri na amejitahidi kwa uwezo wake, lakini tunahitaji kuwa serikali itizame umuhimu wa hii wizara. Mhe. Spika, hii wizara ina mambo mengi ya muhimu ambayo ni pato ya taifa letu.

Mhe. Spika, kwa hayo naomba kuunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana.

**Mhe. Mussa Khamis Silima:** Ahsante Mhe. Spika, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii na mimi kusema machache ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Moja kwa moja Mhe. Spika, kwa kujali wakati niende moja kwa moja kwa kuchangia sehemu ya Baraza la Michezo.

Mhe. Spika, nadhani sote ni mashuhuda wa hivi karibuni tu kulikuwa kuna mashindano yalikuwa yafanyike Bara mpira wa basket ball, kwa bahati mbaya mchezo ule haukufanyika sababu zilizoulizwa ni kwamba Chama cha Mpira wa *Basket Ball* hapa Zanzibar kilikuwa hakijafanya uteuzi kwa hiyo hakikuweza kushirikisha timu zake. Hiyo imenipelekea kusema ni kwamba Baraza la Michezo ina maana haikukamilisha taratibu zake kuhakikisha kwamba tunakuwa na uongozi ambao unaweza kuvifanya vyama vyao kushiriki katika mashindano yote yale yanayotokea. Kwa hivyo, niseme tu kwamba kidogo nimehisi kwamba kuna mapungufu kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri aone nalo Baraza la Michezo aweze kulishajihisha ili kifanye uchaguzi wa uongozi wake na hatimae waweze kushindana pale mashindano yanapotokea. Mhe. Spika, pia ashajihishe vyama vyengine ili visije vikakumbwa na kadhia kama hiyo.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye Uwanja wa Amani, ni kwamba wengi wamesema wachangiaji waliopita kama hivi karibuni uwanja ule ulifanyiwa matengenezo makubwa sana, tunaipongeza serikali kwa hilo. Lakini kilichojitokeza baada ya matengenezo yale uwanja ule hauwezi ukatumika vizuri hivi sasa, hata juzi katika mashindano ambayo tulitaka tuletewe hapa ya *challenge* imeshindikana kutokana na kwamba picha ile ya uwanja ni mbaya, na hiyo kwa sababu ni kwamba ule udongo ambao umewekwa pale baada ya yale matengenezo sio

mzuri. Mhe. Spika, matokeo yake majani yalioteshwa pale hayakuota vizuri na kubwa zaidi lilochangia ni kwamba kumekosekana maji pale uwanjani ndio maana hata majani yaliyopandwa hayawezi yakaota kutokana na kwamba yanakosa maji.

Mhe. Spika, kwa hiyo inaonekana pamoja na kwamba tumeutengeneza ule uwanja lakini sasa dhamira ya uwanja ule ni kuchezwa mpira, hivyo kama mpira hauchezwi maana yake ni kwamba hauna maana au hayana maana yale ambayo yamefanywa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri ahakikishe kwamba maji katika uwanja ule yanapatikana wakati wowote ili yaweze kutumika kwa shughuli za pale uwanjani, na ikiwa moja wapo ni hili la kuchezwa mpira pamoja na matumizi mengine.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba umefika muda wa kwenda na wakati huu mpango wa kupanda majani haya ya kawaida ni basi sasa kwani viwanja vyote sasa hivi havina tena mambo yale ya majani kama hayo. Hivi sasa chakufanya ni kuweka zulia kama wenzetu wanavyofanya katika viwanja vyao hasa hivi vikubwa ambavyo wanavitumia kwa michezo hii ya kimataifa. Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri ahakikishe anauona uwanja wa amani kwa jicho la huruma ili aweze kuuwekea majani hayo, hilo litasaidia kutokana na ile hali ambayo ipo sasa hivi pale ya uwanja ule kushindwa kutumika kwa kuchezewa michezo hiyo mikubwa mikubwa.

Mhe. Spika, vile vile pale uwanja wa amani kuna hoteli, hoteli ile ilijengwa kwa madhumuni ya nia njema tu, alijenga Marehemu Abeid Karume hoteli ile ili iweze kuwasaidia wana michezo wanapokuja pale kuja kucheza mpira waweze kutumia hoteli ile kuweza kukaa pale na kushiriki mashindano au michezo ambayo wamealikwa. Lakini hoteli ile Mhe. Spika, mimi nilidhani baada ya matengenezo ya uwanja kitakachofuatia ni utekelezaji wa ile hoteli, kwa bahati mbaya hoteli mpaka hivi sasa ninavyosema bado iko katika sura yake ile ile na katika hali yake ile ile.

Mhe. Spika, kwa kumbukumbu zangu ni kwamba wale waliotengeneza uwanja ule walikodisha ile hoteli pale ile kampuni ambayo ilitengeneza ule uwanja walipewa ile hoteli kwa kukodishwa na mwisho wa kumaliza matengenezo ya uwanja zile fedha ambazo zitakuwa wamekodi wale ndio ilikuwa zitumike kwa matengenezo ya ile hoteli. Kwa hivyo, sijui hali imekwenda vipi matokeo yake hoteli imebakia vile vile, sijui hizo fedha kama zipo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri labda aje kutufafanulia hilo tuone kama wamebadilisha maamuzi au ni vipi.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende kwenye Shirika la Utalii. Mhe. Spika, shirika hili lina nyumba nyingi sana ambazo zilirithi huko nyuma ikawa

zinatumika kwa masuala ya kuwaweka wageni au kukodisha kwa shughuli mbali mbali za wageni. Lakini baadhi ya nyumba hizo nyingi zimechoka mno, matengenezo yake baadhi mpaka sasa hazina matengenezo kwa mfano kama ile ya Chwaka ambayo imetajwa ina matatizo ni aibu hata kumpeleka mgeni pale na hata huyo mtu anayetaka kukodi hawezi akaitumia kutokana na hiyo hali ilivyo. Nadhani nalo hilo nimuombe Mhe. Waziri zile nyumba za Shirika la Utalii zilizokuwepo maeneo mbali mbali kama Bwejuu, Chwaka na kwengineko basi zingefanyiwa matengenezo ili ziweze kutumika kwa shughuli hizo za utalii.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye suala la Shirika la Magazeti ya Serikali. Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada na bidii aliyoifanya pamoja na watendaji wake kwa kulifanya gazeti la Zanzibar Leo kama vile ambavyo limeelezwa humu katika kitabu kama litakuwa la rangi ili liweze kuvutia wasomaji na kadhalika. Kwa hivyo, nampongeza kwa hilo.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba hivi sasa hapa kwetu kuna utitiri wa magazeti, magazeti mengi yale ya udaku, sijui yanafunza nini magazeti yale mengine kwa maadili ya hapa kwetu na silka zetu. Nadhani kuna taasisi ambayo inahusika na kuzifanyia sensa hayo magazeti, hivyo nadhani taasisi ile ingeweza kupembua yale magazeti ambayo yaliyokuwa hayatufai hapa yenye kuonesha picha ambazo hazistahiki kuwepo kwenye magazeti au sio nzuri kuziona watoto wetu na hata sisi wakubwa. Kwa hivyo, magazeti yale tungeepukana nayo tukachagua yale magazeti ambayo yanatuelimisha, yanatupa habari za maana lakini sio magazeti ya ovyo ovyo tukayaruhusu yakawepo hapa kwetu na wala hayatuletei mafunzo ya aina yoyote.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye Chuo cha Uandishi wa Habari. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 32-33 Mhe. Waziri ameeleza tu pale kwamba ameanzisha chuo cha uandishi wa habari. Mhe. Spika, ni habari njema na kwa kweli nimpongeze kwa hilo kwani ameeleza mambo mengi yanayohusiana na hicho chuo na utaratibu mzima. Mwisho akamalizia kusema kwamba sasa hivi pale wameanzisha mitaala katika chuo hicho cha lugha ya Kichina. Ni sahihi na ni moja katika lugha ambazo zinatumika sasa duniani, lakini pia isiwe imeishia hiyo ya Kichina kuna lugha nyengine maarufu zaidi hivi sasa kuliko hata hiyo ya Kichina. Kwa mfano, kama Kifaransa na Kijerumani nadhani nazo hizo ingekuwepo mitaala kama hiyo nayo ikawa wale wanafunzi wanapata mafunzo watakaoingia katika chuo kile kuweza kujifunza katika lugha hizo. Mhe. Spika, ni vyema pia kuwe na lugha za nchi nyengine ili ziwe zinafundishwa pale isiishie na hiyo ya Kichina.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye Idara ya Utamaduni. Mhe. Spika, Mji Mkongwe kumejaa utitiri wa maduka yale ya vinyago, sijui kama vinyago ndio

utamaduni wa Zanzibari, nadhani kuna tamaduni nyingi za Zanzibar ni vizuri katika maduka yale tukaonesha zile tamaduni za kwetu hasa, isiwe vinyago sio tamaduni zetu. Lakini kila maduka unayopita Mji Mkongwe mengi yao yana vinyago, hiyo sio tamaduni yetu hapa tungetafuta zile tamaduni za kwetu ili tukaziweka maduka yetu hayo ili wageni wakija waone tamaduni zetu ni hizi sio vinyago tu.

Mhe. Spika, vile vile niende kwa wale wanaotembeza wageni, ningemuomba Mhe. Waziri kwenye suala hilo hilo la utalii hususan wale wanaotoka Bara kwa kweli hawatoi historia halisi ya nchi yetu, wanaeleza mambo tu kijujuu kwa sababu wao hawayajui. Kwa hivyo, ni vizuri tungepata wale watembezaji wageni wenye asili ya hapa kwetu ambao wanayajua mambo ya hapa kwetu wakaweza kuyaeleza vizuri kwa wale wageni na wageni wakaondoka hapa na taaluma njema. Lakini wenzetu wale wa Bara mengi ya hapa kwetu hawayajui, lakini wao ndio wako mbele kabisa katika shughuli hii ya kutembeza wageni. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akashajihisha watu au akatoa taaluma kupitia wizara yake kwa watu wanaohusika na masuala haya wakawa wengi ni wale wanaotoka hapa kwetu wenye kuijua Zanzibar na kuweza kuijua historia yote ya Zanzibar.

Mhe. Spika, vile vile niende kwenye makadirio ya matumizi ya mwaka 2010/2011. Mhe. Spika, kwenye eneo lile la ukusanyaji wa mapato nimeona kwamba makadirio yamakusanyo kwa mwaka huo ni shilingi 1,126,800,000, lakini hali halisi ya makusanyo yaliyokusanywa ni shilingi 1,735,117,000 kuna tofauti kama ya milioni 119 au karibu milioni 20. Mhe. Spika, hapo kuna picha gani? Nilichokihisi mimi ni kwamba kuna matatizo ya uvujaji wa mapato kwa hiyo ningemuomba Mhe. Waziri katika jadweli yake ile ya Nam. 2 yenye kuonesha hali hiyo ya ukusanyaji wa mapato hapo kidogo angetupa ufafanuzi tukaona kuna matatizo gani hata yale makadirio ikawa hayakufika kwa baadhi ya taasisi hata nusu. Lakini kuna taasisi kwa mfano hapo katika kiambatanisho Nam.2 ukurasa wa 77, kwa mfano Sauti ya Tanzania Zanzibar makadirio yalikuwa ni milioni 72, lakini kilichokusanywa ni milioni 56. Hapo kidogo inatia moyo na kuona kwamba jitihada imefanyika labda pengine matatizo mengine madogo madogo tu yametokea.

Kwa mfano, nyengine kama ile Idara ya Televisheni makadirio ni shilingi milioni 73 kilichokusanywa ni milioni 24. Ukija kwenye Idara ya Habari Maelezo hiyo ndio yenye kutia moyo peke yake makadirio yalikuwa ni milioni 23 lakini kilichokusanywa ni karibu ni mara mbili ya kile ambacho kilikadiriwa kuna milioni 43. Kwa hivyo, kitu ambacho kinatia moyo hicho hapo. Pia pengine Idara ya Utamaduni makadirio yalikuwa ni milioni 7 kilichokusanywa ni milioni 1 kwa kweli hapo hiyo inavunja moyo inabidi ujiulize kuna nini au kumetokea nini mpaka ikasababisha kuwa katika hali hiyo.

Mhe. Spika, idara nyengine pale iliyokuwepo ni Idara ya Makumbusho nayo hiyo kidogo inatia moyo sana makadirio yalikuwa ni milioni 145, lakini kilichokusanywa ni milioni 107, halikadhalika Kamisheni ya Utalii. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri katika makusanyo ya mapato katika hizi taasisi zetu nayo hayo pia ayatupie macho kwa sababu inaonekana kwamba labda kuna ujanja fulani ndio unaochangia kwa baadhi ya taasisi kufanya vizuri na baadhi ya taasisi kutofanya vizuri.

Mhe. Spika, kwa kujali muda mimi niseme hayo machache kwa sababu mengi wenzangu waliotangulia kuchangia wameyasema, sioni sababu ya kuyarejea tena hivyo nasema mimi niishie hapo. Mwisho kabisa niseme kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi jioni hii ya leo kuchangia machache katika hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kutokana na jitihada yake anayoifanya, waswahili wanasema, huwezi ukakamilisha yote lazima utakuwa na mambo mengine yatakuwa na kasoro lakini pale ambapo mtu anastahiki sifa basi mpe sifa yake. Mhe. Spika, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri kutokana na vyombo vyake vya habari TVZ sasa hivi alhamdulillah Wazanzibari wote sasa hivi wako kwenye televisheni wanawaangalia wawakilishi wao wanavyowawakilisha.

Kwa hivyo, wananchi wote wana furaha kubwa kuona kwamba Baraza letu la Wawakilishi la Zanzibar sasa hivi ni sawa sawa na Bunge kwa sababu tulikuwa tunaona uchoyo wa Bunge kuwa wanaoneshwa *live*, lakini sisi ikawa hatuonekani tunapochangia kuhusu maendeleo ya nchi yetu. Pia niwashukuru sana waandishi wetu wa habari wanaochukua TV humu ndani kwa jitihada yao pamoja na kazi ngumu waliyonayo. Kwa hivyo, na mimi niungane na Mhe. Mtumwa namuomba Mhe. Waziri aone kwamba jitihada yao iungwe mkono ili wasije wakavunjika moyo.

Mhe. Spika, baada ya hapo waswahili wanasema sadaka huanza nyumbani, kwa hiyo na mimi nisije nikasahau kwanza nianzie na kule nyumbani. Naishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuona kama kuna haja ya wananchi wa Micheweni kupewa ile Redio Jamii. Na kwa kweli redio ile inafanya kazi vyua kutosha na wananchi wana muamko wa kuitumia ile Redio Jamii.

Sasa niiombe tu serikali ione kwammba kile kituo sasa kina haja ya kukuzwa na kukuzwa kwenyewe ni kwamba wale waaandishi au watangazaji walioko kule sasa wanastahiki kupewa taaluma. Kwa sababu wameshafanya kazi muda mkubwa kwa uzoefu. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aone kwamba sasa wale vijana kuna haja ya kusomeshwa ili watoe zile habari kwa kuwa na taaluma nayo hasa wasende kwa kubahatisha. Nashukuru sana kwamba kituo kile kinafanya kazi kinyume na vile kilivyotarajiwa, maana ni ziada zaidu kuliko vile kilivyotarajiwa.

Mhe. Spika, baada ya kushukuru na kutoa shukurani za nyumbani sasa niende kwenye Bodi ya Sanaa. Mhe. Spika, kama walivyozungumza wenzangu kwamba utamaduni na mila zetu zinapotea. Kwa sababu sasa hivi kuna watu ambao wana mabaa wanapiga madisko mpaka saa nane za usiku, usiku mzima ni magoma tu. Sasa nauliza hii Bodi ya Sanaa hivi ndivyo inavyotoa vibali kwamba watu wapige ngoma mpaka asubuhi, kwa sababu ngoma zile kuna watu wanafurahi na kuna wengine zinawakera. Sasa hii Bodi ya Sanaa iko wapi? Au haioni, au ndio mila yetu ya Zanzibar. Kwa hivyo naomba watimize wajibu wao, wanapotoa vibali au leseni basi watoe leseni kwa mujibu wa sheria na waweke mipaka yao.

Kwa sababu Mhe. Spika, siku zote unapotoa ruhusa ya kitu ikawa ile ruhusa haina mpaka basi lazima yule aliyepewa ruhusa atazidi mipaka tu, lazima awekewe mipaka. Demokrasia ikizidi mpaka basi inakuwa ni hatari sasa haiwi tena demokrasia inakuwa ni hatari. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kama kuna haja ya hawa watu wanapotoa leseni basi wapewe kwa kuwekewa mipaka, lazima wizara iingie ndani kwa kuweka mipaka.

Mhe. Spika, suala jengine nikiwa niko kwenye mila na utamaduni wetu kipindi kilichopita cha bajeti Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo alikuwa ni Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Lakini alitueleza kwamba sasa hivi tunataka kufanya utaratibu wa kupita wilaya zote, majimbo yote kuangalia utamaduni wetu yaani ngoma zile za asili na kuziweka kwenye orodha ili kurudisha utamaduni wetu wa zamani. Lakini kwa bahati mbaya au nzuri miaka mitano imekwisha hatukuona chochote kile, kwa hivyo tulipewa kwenye karatasi tu. Sasa namuomba Mhe. Waziri aone kwamba kuna haja ya kurejesha miala na utamaduni wetu wa asilimi na ngoma zetu za asili. Kuna michezo mingi sana ya zamani ambayo inafurahisha lakini sasa hivi imeachwa moja kwa moja, sasa hivi ngoma zilizoshika nguvu ni kizazi kipya, jamani sisi kizazi kipya ndio utamaduni wetu? Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri aone kuwa kuna haja ya kurudisha utamaduni na ngoma zetu za asili na tuzione katika televisheni zetu.

Mimi naona kule Bara wenzetu kuna vipindi wanasema ni kipindi cha Ngoma Zetu, utakuta kila mkoa na ngoma ya asili ya ule mkoa inaoneshwa kwenye

televisheni. Kuna siku maalum vipindi hivyo vinakuwa *live* unaona kama ni utamaduni wetu wanaonesha ngoma zao za asili. Kwa hivyo na sisi tunataka tuone kwamba kuna ngoma ambazo zilikuwa kila michezo ambayo ilikuweko kama ni mchezo wa ng'ombe, kama mchezo gani tuone kwenye televisheni kwamba leo wako katika wilaya fulani au mkoa fulani na tunaona utamaduni wa ile wilaya au jimbo lenyewe. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri aona kwamba kuna haja ya kurudisha na kuuonesha utamaduni wetu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze na namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi au anielimishe. Kuna *TCRA* ambayo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Kwa ninavyoelewa mimi ni kwamba Mamlaka hii ni moja katika taasisi za Muungano, sasa hawa wanakuwa wao ndio wanaogawa mawimbi kwenye TV, Redio na kila kitu, kwa sababu ni *regulate* wa Tanzania nzima na hawa kuna fedha zinazoingia kwa ajili ya kazi zao, nilitaka kujua tu anambie Mhe. Waziri atapokuja simama anieleze kuna uhusiano gani wa hii taasisi na hii Wizara yetu ya Habari ya Zanzibar. Kwa sababu hawa wanakusanya mapato je, *TRA* inapokusanya fedha zinabakia hapa hapa Zanzibar kwa *TRA* iliyopo Zanzibar.

Hii *TCRA* inapokusanya mapato tunapata kiasi gani Zanzibar kutokana na mapato ya kazi yake hiyo. Sasa Wizara ya Habari tunafaidika vipi Zanzibar.
Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kuwa kuna uhusiano gani na tunapata kiasi gani sisi kutokana na mapato yanayoingia kutoka *TCRA*.

Mhe. Spika, suala jengine Zanzibar kuna *ZFA* na Bara kuna TFF, sasa TFF ninavyojua mimi hii ni Shirika la Michezo au Chama cha Michezo cha Tanzania. Sasa chama hiki kinapokuwa na michezo aidha kunapokuwa na michezo ya kimataifa timu zinapokuja zikawa zinacheza inakusanya mabilioni ya shilingi, lakini fedha hizi zinazokusanywa kwa ninavyojua mimi kuna fedha zinaingia kwenye timu zile zinazocheza, kuna fedha zinazoingia kwa kiwanja na kuna fedha ambazo zinabakia katika chama cha michezo kile *TFF*. Kwa hivyo nataka kujua kwamba hizi pesa zinapokwishakusanywa mabilioni ya shilingi haya je, sisi Zanzibar tunapata nini, *ZFA* inapata kitu gani kutokana na fedha hizo kwa sababu *ZFA* ni Chama cha Mpira cha Zanzibar.

Lakini Mhe. Spika, *TFF* ni ya Tanzania nzima na ndio maana tunaunda timu ya taifa kwa ajili ya Tanzania nzima. Sasa je, sisi tunafadika vipi na hizi fedha zinazokusanywa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hili atakapokuja atupe ufafanuzi ili tujue kwamba tunafaidika vipi na hiki chama cha michezo cha Tanzania.

Mhe. Spika, suala jengine namuomba Mhe. Waziri atwambie kuhusu Uwanja wa Gombani Pemba, uwanja huu tuliambiwa tangu kipindi kilichopita kwamba

nyasi zishafika na sasa zinataka kutengenezwa lakini mpaka leo nyasi zile naona sijui ziling'oka au zilivuja njiani, mpaka leo hii hatujui habari zake. Halafu atwambie hizi nyasi hasa zilipokuja ziligharimu kiasi gani, tulipata wafadhili gani na serikali yetu ilichangia kiasi gani kuptia Baraza letu la Michezo au kutoka katika wizara yetu hii. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atapokuja atueleze hili suala ili na sisi tupate ufafanuzi kulijua.

Mhe. Spika, naomba kwa leo hii niishie hapo na mimi naunga mkono hoja lakini namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe ufafanuzi kutokana na hayo niliyoyazungumza. Naunga mkono hoja.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia leo kufika hapa tukiwa wazima wenye afya na kuweza kulitumikia taifa letu. Napenda kukushukuru wewe Mhe. Spika, kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia mawili matatu.

Kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Naibu wake na watendaji wake wakuu kwa kutayarisha hotuba nzuri ambayo ina mwelekeo makini na nachukua fursa hii kuwaombea Mwenyezi Mungu awajaalie waweze kutekeleza yale ambayo wameyapanga.

Mhe. Spika, mimi nitaanza moja kwa moja kwanza kwa kuwapongeza Waandishi wa Habari wote wa Zanzibar. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waandishi wa Habari kwa vile walivyoweza kutusaidia katika uchaguzi wetu mkuu wa Zanzibar, amani na utulivu, umoja na upendo na mshikamano umesababishwa na wao, walikuwa wakifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba wananchi wanapata taarifa zote vizuri na wananchi wa Zanzibar wanaweza kutumia haki yao ya kupiga kura. Tunawashukuru sana kwa kweli Waandishi wa Habari.

Kwa hivyo, kwa sababu tunajua kwamba waandishi wetu wanafanya kazi kubwa nawaombea kwa waziri waandishi wetu tuhakikishe kwamba maslahi yao tunayaboresha. Maslahi yanazidi kuwa mazuri, maposho yao wanalipwa vizuri na mambo mengine na haki zao kama wafanyakazi basi wapewe mambo mazuri.

Mhe. Spika, mimi ningeanza moja kwa moja ukurasa wa 17 kwa kumpa pongezi kubwa sana Rais wa Zanzibar kwa kuanzisha Shirika la Utangazaji. Kwa kweli ilikuwa kuna haja kubwa ya kuanzisha shirika hili hasa kwa kuona kwamba Idara hii ya Utangazaji ilikuwa inalegalega. Kwa hivyo, kuunda shirika hili ni kuokoa Idara ya Utangazaji na Habari.

Mimi vile vile niwapongeze sana wafanyakazi wote wa Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa kuweka maadili yetu, kuna redio nyingi ambazo zimejitokeza lakini kwa kweli Sauti ya Tanzania Zanzibar imefanya kazi kubwa katika kuweka maadili yetu. Sauti nyengine zinafanya kazi lakini Sauti ya Tanzania Zanzibar imekuwa inahakikisha kazi yake kubwa ni kuelimisha na kutoa taarifa lakini kuhakikisha kwamba maadili yetu ya Kizanzibari bado yanaendelea kuwa mazuri.

Vile vile nachukua fursa hii kuwapongeza wafanyakazi wa Televisheni Zanzibar, ingawa nasikitika sana kwamba sasa Televisheni Zanzibar sio ile iliyokuwa miaka ya nyumba mingi sana ambayo ilikuwa kwa lengo la kuelimisha, kutoa taarifa na kuburudisha. Ukweli ni kuwa Televisheni yetu ya Zanzibar ilikuwa ni katika televisheni za mwanzo kabisa katika Afrika ya Mashariki. Lakini kwa kweli sasa hivi imekuwa televisheni ya mwisho kabisa katika Afrika Mashariki. Inasikitisha Mhe. Waziri, inasikitisha kwa sababu Wazanzibari wanajivunia televisheni waliokuwanayo, lakini katika majivuno hayo televisheni ile haiwawakilishi wao.

Sasa hivi Televisheni Zanzibar imekuwa ina vipindi vya nje vingi ambavyo vinaustaarabu wake, kwa sababu ukichukua vipindi vya nje vingi tunaona ule ustaarabu wa wenzetu ambao sisi kwa mila na desturi zetu yale mambo hayatufai. Mhe. Waziri naomba uhakikishe kwamba vipindi ambavyo havitufai basi visitiwe katika Televisheni yetu ya Zanzibar. Hilo moja.

Lakini katika miaka ya nyuma Televisheni Zanzibar ilikuwa ikitengeneza vipindi vingi sana kuanzia vya watoto mpaka watu wazima, sasa hivi hakuna. Tulikuwa na vipindi vya shangazi na mjomba wakitengeneza vitu mbali mbali vya kuwachangamsha watoto sasa hivi hamna.

Mimi mara nyingi sana huwa ninajaribu kutaka kuiangalia Televisheni Zanzibar lakini inanivunja moyo, sio mimi peke yangu naamini kwamba Wazanzibari wengi sana sasa hivi hawaiangalii Televisheni ya Zanzibar kwa sababu hizo.

Televisheni ya Zanzibar zamani tulikuwa hata na mapishi mnafundishwa ya kiasili ya Zanzibar, kusuka mkeka unafundishwa kwenye televisheni ya asili ya Zanzibar, kukunja kanga unafundishwa na televisheni, yako wapo yale mambo, watoto wetu inabidi wajifunze watajifunza wapi. Hii ni njia moja ya kujifunza na ndio lengo kubwa la Televisheni ya Zanzibar. Sasa Mhe. Waziri naomba urudishe hadhi ya televisheni yetu, inahitaji mkakati mzuri na ninaamini uwezo upo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kwa hilo tunakuomba tukija tena mwakani hili tusilizungumze tuzungumzie mengine.

Mhe. Spika, napongeza vile vile Gazeti la Zanzibar Leo ambalo kwa kweli nalo kwa sasa hivi limepiga hatua nzuri sana. Gazeti limekuwa zuri linavutia, la rangi, lakini vile vile limekuwa na taarifa nzuri zenye ukweli ndani yake. Ndio maana nikasema kwamba nawapongeza sana waandishi wa habari, kwamba wanazungumza vitu vingi ambavyo sasa vinatuletea matumaini.

Mhe. Waziri sasa hivi tatizo ni moja kwamba gazeti lile linachapishwa Bara na thamani ya mashine za kuchapishwa ni shilingi 800 milioni. Mimi nafikiria kwamba ukifanya hesabu na kwenda kupeleka Bara kuchapishwa nakurudishwa hapa Zanziba kwa mwaka pengine itazidi hata hiyo thamani ya ununuaji wa hizo mashine. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri tufanye juu chini tuhakikishe Gazeti letu la Zanzibar Leo tunalichapisha Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa naingia katika Sekta ya Utalii. Sekta ya Utalii ndio uti wetu wa mgongo wa uchumi wetu wa Zanzibar. Sasa hivi asilimia kubwa ya mapato yetu inategemea utalii lakini bado hatuutendei haki utalii, nasema hivyo kwa maana kwa sababu tuko katika mashindano ya utalii. Zanzibar tuna sifa zetu lakini na wenzetu nje wana sifa kama sisi au wengine zaidi ya sisi kutokana na miundombinu ambayo wameiweka ili kuhakikisha kwamba Sekta ya Utalii itakuwa bora. Sasa sisi tumeanza utalii tukasahau kwamba kuna mambo ambayo lazima tuyaunganishe ili tuhakikishe kuwa utalii unatuletea tija.

Moja ni sera. Kama tunataka utalii utuletee tija basi tuhakikishe kwamba tuna sera nzuri ambayo itahakikisha kwamba utalii wetu unawasaidia wananchi wetu wa Zanzibar. Mimi Mhe. Waziri nakuomba tuipitie tena sera yetu kwa manufaa ya uchumi wa Zanzibar na kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar. Hilo moja. Lakini katika utekelezaji tuhakikishe yale ambayo tunayapanga tuyatekeleze. Wale wawekezaji wanaokuja wakija hapa wanaambizana huko waliko wapi pa kwenda ili waweze kuchuma lakini wachume kirahisi, wanakuja hapa wanavunja sheria tunawatizama kwa nini? Kwa nini tuwatizame wawekezaji ambao wanavunja sheria tuwachukulie hatua.

Mhe. Spika, hii ni nchi yetu sisi wao wamekuja kutoka kwao wamekuja hapa lazima wafuate masharti kwa sababu na sisi tukienda sehemu nyengine kama hufuati masharti haiwezekani na itatuathiri sisi, kwa sababu sisi tunabakia wao wanaondoka. Kwa hivyo, Mhe. Waziri sera tuipitie upya, tuitizame na sheria zetu ndogo ndogo tuzipitie tuhakikishe kwamba utalii unanufaisha uchumi wa Zanzibar na unawanufaisha Wazanzibari.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia kuhusu Kamisheni ya Utalii, nimefanya kazi mimi Kamisheni ya Utalii, tuko katika ushindani lakini kuna suala zima la kujitangaza Zanzibar. Wenzetu Bara wanatumia pesa nyingi sana kujitangaza

na kujitangaza maana yake umo kwenye ushinda wa biashara na utumie fedha bila ya fedha kutumia huwezi kujitangaza kibiashara. Sasa hawa moja katika lengo kuu la kuanzisha taasisi hii ni kuitangaza Zanzibar ndani ya nje, uwezo huo wao ni mdogo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri uwezo wa kujitangaza Zanzibar ni mdogo mno, sasa imekuwa ni tabia na desturi wanakwenda katika nchi fulani tu, sehemu nyengine hawafiki kwa sababu uwezo ni mdogo. Lakini mapato tunayoyakusanya ni mengi kutoka kwenye utalii, sasa kama tunakusanya mapato tu-*invest* hapa, tukate fungu la pesa kuwekeza huku ili tupate watalii wengi zaidi matokeo yake tunapata watalii vishuka wengi. Mhe. Waziri nakuomba taasisi hii uitizame kwa jicho la huruma, wapeni pesa hawa watu wafanye kazi waende wakaitangaze Zanzibar nje matokeo yake tutakuja kuyaona. Wanahitaji kutengeneza vipeperushi, kutengeneza vitu vyengine, haya yote ni mambo ya kujitangaza kiutalii, lazima utengeneze vipeperushi, magazeti, kalenda kila kitu cha kujitangazia, lakini sasa tukisema kila siku tunashindwa kufanya vitu hivyo basi mimi naamini kwamba utalii tutashindwa na ni afadhali tusiseme kwamba utalii ndio uti wa mgongo wa taifa letu. Kwa sababu wenzetu na wao wanajikaza wanafanya vile vile na zaidi ya vile na ndio maana tunaona wenzetu wanatajirika sana katika utalii.

Mhe. Spika, mimi nataka kugusia kidogo kuhusu Shirika la Utalii. Kwa kipindi kirefu sana ile nyumba ya Kihistoria ya *Living Stone* imekuwa tukiisema kwamba ni nyumba ya kihistoria kwa hivyo tunatafuta wafadhili waijenge ili na sisi tuweze kuendeleza utalii nchini kwetu. Kweli ile ni nyumba ya kihistoria na kwa kweli inataka matengenezo. Lakini ni kipindi kirefu mno tumeshasubiri sana hakuna. Sasa Mhe. Waziri naomba anieleze hivi, kwamba kama hatujapata mpaka kufikia labda mwaka fulani tutafanya nini na ile nyumba inaharibika kila siku. Ikiwa kama tutasubiri wafadhili ili tufanyiwe biashara basi mimi nafikiri wafadhili kama hawaji ile nyumba itakwendazake chini hasara itakuwa kubwa zaidi. Mhe. Waziri naomba hili ulitizame na upange mikakati mizuri sana ya kuhakikisha kwamba hata sisi wenyewe basi tuweze kufikiria mbinu ya sisi wenyewe kulikarabati hili jingo.

Mhe. Waziri naomba nizungumzie suala la Idara ya Uchapaji. Idara hii tunaifahamu sote kwamba ni idara ambayo takriban kila wizara inaitegemea idara hii. Lakini idara hii tumekuwa sisi wenyewe tunaididimiza na kuididimiza kwenyewe mbali ya madeni ambayo tunadaiwa, lakini vile vile hata hao wafanyakazi hatuwapi huduma zinazofaa. Wafanyakazi wa idara hii kwa kweli wanafanya kazi sana lakini hata maposho yao hawapewi kikamilifu wanarundikiwa maposho, wakiuliza inakuwa tabu na yote inasababishwa na kuwa madeni hayalipwi. Kwa sababu yangekuwa yanalipwa madeni mimi naamini kabisa wafanyakazi wangepewa maposho yao lakini kwa sababu

hawalipwi. Sasa mimi naomba hilo tulifikirie na basi waanze kulipwa kidogo kidogo waonewe huruma ili na wao waweze kujiendeleza.

La pili afya ni muhimu, afya zao ni muhimu sana. Kuna mchangiaji mmoja amesema hapa kwamba walikuwa wanajua kuwa wanapewa *ratio* fulani ya maziwa kwa siku lakini sasa ile *ratio* imefanywa robo yake ndio wanayopewa na siku nyengine hawapati kabisa. Mimi naona ipo haja ya kuwasaidia hawa ili tuhakikishe kwama tunawa *retain* nao kwa sababu baada ya muda watakujakutukimbia au kuacha kazi kutokana na maradhi mbali mbali na hasara itakuwa ni ya taifa.

Mhe. Spika, mimi wakati nikiwa mdogo Zanzibar ilikuwa naifahamu kwamba ni moja katika kisiwa ambacho kinatoa wanariadha wengi sana, lakini sasa hivi wanariadha hatuwasikii, zamani tulikuwanao wengi na tukiwajua, lakini sijui wapi tumekwenda kombo. Sasa hivi tumekuwa tunafanya michezo mingine tunaisahau riadha. Mimi ningetoa rai Mh. Waziri kwa sababu tunajua wanariadha wengi wanaaza chini, sasa wizara kuchukua jukumu kubwa la masuala ya michezo kwa kweli saa nyengine inakuwa sio sawa. Kwa sababu michezo inaanzwa katika mitaa, kwa hivyo, hebu tuwezeshe Serikali za Mitaa watutafutie wanamichezo huko wahamasishwe vijana kufanya michezo, sio wizara ifanye kazi peke yake, lakini lazima kuwe na mkakati wa kuhamasisha vijana kama itakuwa ni kwa kupitia Wizara ya Elimu au kwa kupitia Serikali za Mitaa, Wilayani, Mkoa tuhakikishe kwamba vijana kule ndiko tunakowatoa na wao tunasaidiana tunakwenda nao sambamba katika kuinua michezo ya riadha.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ninalotaka kulizungumzia ni uwanja wa Mao Tse Tung. Mhe. Spika, uwanja ule mimi nilikuwa nikipita na kuuona ulikuwa ni uwanja mzuri sana. Mhe. Spika, juzi wakati tumekwenda na mimi nilikuwa mgeni rasmi wa mechi ya mpira wa miguu baina ya Baraza la Wawakilishi na benki zetu za Zanzibar, tulisikitika sana kuona hali ya uwanja wetu. Mhe. Spika, ule uwanja ni wa kihistoria tunao kipindi kirefu namuomba Mhe. Waziri aufanyie ukarabati uwanja ule, ili tuhakikishe kwamba tunautumia ukiwa katika hadhi yake iliyokuwa zamani.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache nachukua tena fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake kwa kipindi ambacho wamekaa katika wizara hii na kufanya mambo yaliyo muhimu, pia kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi kwa niaba ya wanawake wote wa Unguja na Pemba naunga mkono hotuba hii mia juu ya mia.

**Mhe. Spika:** Kwanza niseme kuwa muda wetu unatukwaza sana na bado tuna wajumbe wengi wanaotaka kuchangia. Kwa dakika kama 45 zilizobaki hizi pengine tukifupisha tunaweza kumudu kuwaita Waheshimiwa Wajumbe wanne. Sasa niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wale ambao tutapata nafasi tupunguze sana muda ili angalau hawa wanne tuwapate ili kesho Mhe. Waziri baada ya kusaidiwa na baadhi ya Mawaziri aweze kufanya majumuisho.

Kwa hiyo, nimwite Mhe. Saleh Nassor Juma jitahidi utumie dakika 10 na baadae Mhe. Mohammed Haji Khalid kwa dakika hizo hizo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia fursa hii kuchangia machache katika hoja iliyopo mbele yetu. Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha siku ya leo tukiwa hai. Pia nadhani nitakuwa mchache wa shukrani kama sikukushukuru wewe uliyenipa nafasi hii na mimi kutia nyalio kidogo kwa sababu si msemaji sana wa mambo haya. Mimi ni mwalimu zaidi kuliko mtu wa teknolojia ya habari siwezi kusema sana katika mambo ya habari. Kwa hivyo, nadhani dakika 10 zinaweza zikanitosha.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais kwa kutuchagulia kijana wetu huyu Mhe. Abdillah Jihad Hassan, ni kijana bado ana uwezo na kweli kapata *gender* msaidizi ambaye naamini kila siku atakuwa anatujibia maswali yetu hapa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa niende kwenye hoja na nianzie kwenye Shirika la Magazeti ya Serikali. Mhe. Spika, hili ni shirika muhimu sana na linalohitaji kutunzwa, kuenziwa, pamoja na kuwezeshwa katika uendeshaji wake. Mhe. Spika, shirika hili naweza nikasema kwamba kupitia magazeti na kupitia makala za waandishi wa magazeti yale ni kioo ambacho jamii hukitumia na hatimae kujirekebisha. Kwa hivyo, shirika hili linatakiwa liendeshe shughuli zake kwa umakini na inatakiwa iwe na wigo mkubwa katika kutoa taaluma.

Mhe. Spika, hapa leo tuna gazeti moja tu la Serikali linalojulikana kama Zanzibar Leo ambalo linachapishwa Dar es Salaam. Inaonekana wenzetu hawa hawako *creative*, sitaki nizungumze neno hilo lakini nadhani si wabunifu sana. Kwa sababu gazeti hili moja tangu mwaka 1964 hadi leo hii Zanzibar tunazungumzia gazeti moja ni aibu. Mhe. Spika, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alituachia gazeti moja hapa lililokuwa likijulikana kama Kweli Ikidhihiri Uongo Hujitenga tulikuwa nalo tangu enzi hizo. Mwaka 1964 hadi leo hii limeondoka lile Kweli Ikidhihiri Uongo Hujitenga likaja Zanzibar Leo. Jamani nchi hii ina gazeti moja tu haipendezi, wenzetu mnatakiwa muwe wabunifu katika kuhakikisha kwamba *transparency* katika nchi inapatikana na inapatikana pale ambapo vyombo vya habari vinakuwepo.

Mhe. Spika, inasikitisha sana, hii Idara ya Habari Maelezo inatumia vigezo gani katika kuhamasisha watu kuanzisha magazeti. Hapa lilikuwepo gazeti la Dira watu wengi walikuwa wakilipenda, watu walikuwa wakitoka Tanga, Mombasa, Pemba na kuja kununua gazeti la Dira, lakini yule mzee wakamfungulia mashtaka mpaka akafa.

Sasa Mhe. Spika, sijui ni misingi gani inayotumika mpaka yakafunguliwa haya magazeti, kuna kigazeti cha Zanzibar Leo hicho hicho kinatayarishwa Dar es Salaam. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wawe *creative* waruhusu magazeti na kazi ya kusema watu ndio ilivyo, isiwe leo ameshaandikwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kesho akalifunga gazeti ndio maana yake unaambiwa ujirekebishe. Mimi nadhani yule mzee ameshakufa lakini pengine wengine wapo wanataka kuanzisha gazeti basi waruhusiwe ili *transparency* katika nchi ipatikane.

Mhe. Spika, sasa nije katika TVZ. Mhe. Spika, kwa kweli TVZ ni TV ya mwanzo tena ya rangi kwa hapa Afrika Mashariki. Mhe. Spika, niwapongeze viongozi wetu wa awamu ya mwanzo kwa kutuletea kitu kama hichi. Kilichotakiwa ni kuiendeleza TVZ. Mhe. Spika, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alipokuwa hai TV ile tulikuwa tukiisikia mpaka mvunguni Vitongoji. Wale mahaini wa kesi ya Mzee Karume tulikuwa tukiisikiliza kwenye mivungu yetu. Leo inasikitisha, Mhe. Spika, mimi nilitaka uniruhusu nilie japo dakika mbili kwamba *asset* tumeachiwa na wazee wetu leo wanazibeza hawa vijana. Kama kanuni zinaruhusu Mhe. Spika, naomba unipe dakika mbili nilie.

Mhe. Spika, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume yeye alikuwa akisema "Tumesoma hatukufahamu, tumejifunza tumejua." Aliweza kuiendesha TVZ tukawa tunaiona mvunguni Pemba, leo kuna watu *intellectual*, watu wa teknolojia ya habari lakini TV hatuisikii mwaka wa ngapi kule Pemba. Mimi nadhani hawana uwezo wa kusimamia chombo kama hichi.

Mhe. Spika, leo nataka jambo moja Mhe. Waziri anambie ni lini Wapemba wataona TVZ. Pia ikifika siku hawakuona TVZ ajiuzulu yeye na Naibu Waziri wake itakuwa hawana uwezo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ajue kwamba kuangalia TV Wapemba ni haki yao ya msingi kwa sababu ni walipa kodi wa nchi hii. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ajue kwamba ana-*violate* Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 13 (4). Mhe. Spika, naomba kwa heshima na taadhima uniruhusu ninukuu kidogo.

Ibara ya 13 (4):

> "Ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi."

Sasa Mhe. Spika, kutoona TVZ wakati ni walipa kodi na wanalipia sawa sawa na walioko Unguja, Wapemba wakawa hawaoni wanaona Waunguja ni kuwabagua.

Sasa kwa mnasaba huo basi, naomba Mhe. Waziri atakapotoa majumuisho yake atwambie ni lini Wapemba wataona TVZ na siku ikifika kama hawakuona yeye na Naibu Waziri wake wajiuzulu mara moja.

Mhe. Spika, nizungumzie uwanja wa Mao Tse Tung ambao ni urithi vile vile. Mhe. Spika, ule uwanja umeibua vipaji sana, kina Nassor Mashoto na wengineo wameanzia pale. Lakini leo kila kukicha wanatafutwa wawekezaji waje wafungue sekta ya utalii, mbona hamuwaiti wakaja wakakishughulikia kile kiwanja cha asili kikawa ni urithi wa nchi yetu tunauendeleza jamani.

Mhe. Spika, juzi wakati Mhe. Naibu Waziri anajibu swali la Mhe. Mwakilishi alisema kwamba viwanja vya Mnazi Mmoja wanaoshughulikia ni Baraza la Manispaa. Sisi tunajua wenye dhima ya kushughulikia michezo ni Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Vile viwanja kama mnakumbuka katika miaka ya 60 ilikuwa ukipita pale siku za sikukuu panafurahisha sana. Enzi za Marehemu Mzee Abeid Amani Karume tulikuwa tunakwenda wenyewe kwenye sikukuu tunafurahi na Athuman Kifupi siku zile raha mustarehe, lakini leo wameshakigeuza jalala, pale pameshakuwa bahari.

Mhe. Spika, mimi nadhani Baraza la Manispaa kile kiwanja wakirudishe kwa Wizara ili kiweze kuendelezwa. Pale ilikuwa hao kina Karume Mussa wale waliokuwa wachezaji wazuri wa nchi hii wameanzia pale, leo kiwanja kinafuga mbu aibu. Akija mgeni pale anakwenda Ikulu akifika lazima aangalie mifugo ya mbu kwanza, ni aibu kubwa sana kwa nchi.

Mhe. Spika, katika kuendeleza michezo wenzetu wamefungua vyuo. Leo nataka anambie Mhe. Waziri vyuo vya utalii amefungua lakini vitengo vile vya kufundisha na kuinua vipaji ana vingapi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie kuhusu Viwanja vya Kufurahishia Watoto vilivyoko Kariakoo Unguja na kile cha Tibirinzi Pemba. Mhe. Spika, viwanja vile watoto wetu walikuwa wanastarehe sana, mapembea ya farasi, treni na nyenginezo, sikukuu ilikuwa kunang'ara lakini leo ni magofu, ni mafichio ya

wala unga na walevi, havifai kabisa. Sasa sijui tatizo liko wapi na hawa ni wataalam. Kama Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kaweza, Mzee Aboud Jumbe kaweza, nyinyi mnashindwa kwa nini watu wenye taaluma. Inasikitisha Mhe. Spika, sasa hivi watoto wetu wanacheza chini ya miembe, mabarabarani humo mara wanagongwa na gari siku za sikukuu wakati viwanja vipo pale.

Mhe. Spika, la kusikitisha zaidi hata kwenye bajeti yake Mhe. Waziri mara hii hakukitaja sijui anaogopa nini. Lazima tujue kwamba watoto ni walipa kodi watarajiwa, lazima tuwalee katika mazingira mazuri, tuwashughulikie, tuwastareheshe. Leo watoto siku za sikukuu wanacheza barabarani wakigongwa na gari, wanacheza kwenye miembe wakiangukiwa na miembe si tatizo hilo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atwambie ni lini atavifufua viwanja vile. Kama tatizo ni hazina atwambie sisi kesho kutwa bajeti yake Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inakuja hapa.

Mhe. Spika, jengine niende kwenye sekta ya utalii. Kwa sababu umeninyima kulia Mhe. Spika, hapa ndio nilikuwa nataka nilie zaidi, nipate kama dakika tano mimi nalia tu. Mhe. Spika, sekta ya utalii katika nchi hii imeondosha utamaduni wetu wote, inaonekana kwamba serikali imeingiza sekta hii kutuondoshea utamaduni wetu wa asili, kutuondoshea heshima na silka za Wazanzibari tulizowekewa na wazee wetu waasisi wa nchi hii.

Mhe. Spika, wale wazee wenzangu wanakumbuka kwamba mtalii alikuwa akiteremka pale Ngerengere kulikuwa na kiwanja jeshini pale siku hizo hakujawa na *Sheikh Abeid Karume Airpoirt*, kulikuwa na matenge pale anafungwa tenge anatembea. Leo hii tumeingiza sekta hii bila ya kuwawekea masharti watalii inadhalilisha.

Mhe. Spika, juzi mchana nilikuwa nasafiri na binti yangu lakini ilinibidi nipate kigugumizi nifumbe macho, mambo tuliyooneshwa uwanja wa ndege ni ya fedheha mno, mpaka leo hii mimi nimeshakoma kufuatana na mwanangu kwa aibu iliyonipata. Sasa inaonekana hawa wamepokea utalii katika mazingira ya hofu au kuwaridhisha watu. Mhe. Spika, hakuna watu waliokuwa *flexible* kama wazungu, mzungu anafuata kadri ya unavyotaka. Kama tungewawekea masharti hawa kwamba ukija nchini vaa hivi wangevaa, pale Saudi Arabia wazungu wanavaa *hagal* wanatembea katika miji, kwa nini sisi tushindwe.

Mhe. Spika, inaonekana serikali ina hofu na kwa mujibu wa Kim Il Sung alisema kwamba kuna utumwa wa aina mbili, kuna utumwa wa bwana na mtwana *(slave and lord)* na utumwa wa hofu *(slave of fear).* Sasa kwa mujibu wa Kim Il Sung anakwambia *"The most worst slavery in the world is slavery of fear."* Katika utumwa mbaya sana ulimwenguni ni huu wa hofu. Wanahofu nini kuwaambia wazungu wasituendee uchi hapa. Mhe.Spika, nadhani sekta hii

ya utalii inahitaji *renovation* ya hali ya juu, lazima tuitafakari upya, kinyume na hivyo bora iondoke isituletee balaa sisi hapa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nadhani sasa nikuombe maelekezo ya kiti, nakaa kitako ikiwa utaniruhusu naomba maelekezo ya kiti.

**Mhe. Spika:** Mhe. Saleh Nassor Juma nilikupa dakika kumi ukachukua 12. Nikuombe basi ufunge hoja yako sasa.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana nitaunga mkono hoja hii baada ya kuelezwa ni lini TVZ itasikika Pemba, ni lini serikali itaanza kufanya mpango wa kushughulikia uwanja wa Mao Tse Tung.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Spika, nakushukuru nami kupata muda huu mdogo ambao haunitoshi hasa kulingana na *art* yangu ya usemaji, lakini nitajaribu kusema machache ambayo nitaweza kuyasema katika kuchangia Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake kwa kuandaa hotuba hii yenye mambo mengi muhimu.

Mhe. Spika, nije moja kwa moja katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi nichukue pointi moja tu inayosema Kutoa Nafasi za Masomo na Mafunzo kwa Wafanyakazi wake. Mhe. Spika, ni jambo muhimu kuwapatia wafanyakazi wetu masomo na mafunzo. Kwa sababu vyombo hivi vya habari siku hizi tunakwenda katika ushindani. Kwa hiyo, kwa kuwa chombo hichi ndio sauti ya serikali lazima tuwe na watendaji ambao wamepata taaluma ya kutosha. Sasa azma ya wizara hii kuwapatia nafasi za mafunzo watendaji wake naiunga mkono pindipo kama wataitekeleza kweli. Ningewaomba waitekeleze isibakie katika maandishi tu katika kitabu hichi.

Mhe. Spika, nije Afisi Kuu Pemba napo nichukue pointi moja tu inayosema Kuvijengea Uwezo Vyombo vya Habari ili vitekeleze majukumu yake kwa ufanisi. Mhe. Spika, kuvijengea uwezo ni pamoja na kuvipatia vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi na kuwapatia wafanyakazi wake huduma bora katika kufanya kazi.

Mhe. Spika, jengine ni kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kila mmoja afanye kazi kulingana na kada yake. Mhe. Spika, kuna tabia mara nyengine watu wanapelekwa nje kusomea fani fulani lakini anaporudi pengine kasomea upigaji picha anafanywa mtangazaji itakuwa ile taaluma aliyosomea sio anayoitumikia. Kwa hivyo, ni vyema mafunzo unayopata ndio uyatumikie.

Mhe. Spika, nimalizie na TVZ Pemba. Mhe. Spika, mimi sitounga mkono bajeti ya Mhe. Waziri kama hatutopata tarehe hasa ni lini Wapemba wataiona TV yao.

Mhe. Spika, nizungumzie Baraza la Kiswahili hapa niseme kwamba Kiswahili kilikuwa chetu lakini tumekiuza, niseme kuwa Kiswahili kimetekwa nyara. Sisi ndio Waswahili na Kiswahili fasaha na fanisi kilikuwa kinasemwa Unguja Mjini, leo Unguja Mjini ndio penye Kiswahili cha ajabu ajabu. Mhe. Spika, utamaduni ni pamoja na lugha yetu, mtu ukimuuliza umekuja kwa chombo gani, anakwambia nimekuja na meli, sio sawa, kuja na meli ama umeichukua au mmefuatana. Mtu utamsikia nimekuja na ndege, ama umeichukua au mmefuatana, lakini nimekuja kwa ndege.

Mhe. Spika, Kiswahili tumewaachi watu wamekipotoa sasa tunalazimika kwenda na huu upotevu wa Kiswahili. Mtu baada ya kuuliza habari za asubuhi, anakwambia mambo poa, si Kiswahili. Mhe. Spika, Kiswahili kimetekwa nyara na pengine hatuna uwezo tena wa kukirudisha. Kwa hivyo, ningeliomba Baraza la Kiswahili la Zanzibar lijiandae kukifanya Kiswahili kirudi katika hadhi yake. Wengine wote huko nyuma walikuwa wanasoma Kiswahili Zanzibar kwa sababu ndio penye Kiswahili lakini tumekiachia. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili alijue na alishughulikie.

Mhe. Spika, nije katika utamaduni, utamaduni ni pamoja na lugha, michezo, mavazi na mengineyo. Mhe. Spika, mimi nina mjukuu wangu ni mwanafunzi lakini tumefika pahala tunazungumza akanambia kile kimashine kidogo cha kuchongea penseli jina mimi hapa siwezi kulitaja. Akanambia babu nataka pesa nikanunue hicho kitu mimi sikitaji. Mimi nikajiuliza ndio nini. Kile kimashine cha kuchongea penseli jina lake ni la ajabu kwa Zanzibar na sisi tunakikubali. Mhe. Spika, kama walimu wapo hapa wanakijua kinavyoitwa. Mhe. Spika, hapa ndipo Kiswahili kilipofikishwa na sisi Waswahili wa asili tupo tunatoa macho tu.

Mhe. Spika, nirudi kwenye huu utamaduni. Mhe. Spika, kwa kweli tuna kazi kubwa na si rahisi tena pamoja na yote tunayozungumza kuurudisha utamaduni wetu na malezi yetu ya asili hii hali imeshakuwa ngumu mno. Kwa sababu huu utandawazi uliopo wa mawasiliano ya redio, televisheni na mambo mengine yote hatuna uwezo wa kuwadhibiti tena. Mhe. Spika, TV ni chombo kizuri kinaelimisha mambo mbali mbali mazuri, inatoa elimu ya dini, inatoa elimu ya dunia lakini kinapotosha mambo chungu nzima na hatuna uwezo wa kuweza kuvifanya virudi katika ile hali ambayo tunataka sasa hivi viende.

Mhe. Spika, kwa kweli tumefika pahala sisi tunakaa na watoto wetu wa kike, wa kiume, baba na mama, tunatazama mchezo kwenye TV watu wanakumbatiana, wanabusiana, wanafanya kila kitu, tumefika pahala hatuoni aibu tena. Kule kupoteza maadili Wazanzibari sasa imekuwa ndio maadili yetu, sasa kurudi katika maadili itabidi tufanye kazi ya ziada wala si kazi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Ni kazi ya kila mlezi, kila mzazi, kila mtu, kila wizara, kila idara na jamii kwa jumla. Vyenginevyo leo watu wanakwenda nusu uchi, iko siku watakwenda uchi moja kwa moja. Tunasema haki za binadamu kila mtu anafanya atakavyo. Watakwenda watu tufikirie kuwa ni wendawazimu na kweli ni wazimu, lakini na yeye ndio haki yake alivyoamua afanye hivyo. Kwa hivyo, tuna kazi kubwa katika nchi hii. Nchi tumeiwachia mpaka leo imekuwa maisha ya jangwani, hapana ni maisha ya msituni. Haiwezekani Mhe. Spika, leo Zanzibar yenye watu ambao asilimia 99 ni Waislamu lakini vitendo vyetu 99 ni kinyume na Uislamu, yaani ni kinyume na imani yetu ni moja tu ambayo ndio tuna ile imani yetu halisi.

Mhe. Spika, mimi ukinipa dakika 10 hukunidhulumu, lakini kwa hii haki yangu ya kusema nitashindwa kusema yale niliyokusudia. Mhe. Spika, hii nchi siku hizi, hawa wanawake zaidi wamekuwa wasomi wakubwa wa dini yao. Zaidi walimu kule makazini kwao. Juzi nilisema lakini Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali hakunijibu. Niliuliza walimu wavae namna gani ili iwe ndio vazi hasa likubalike. Kwa sababu wao lile vazi ambalo wao wanaona ni la heshima basi kuna walimu ambao wanarudishwa makazini eti kwa sababu wamevaa mashungi. Lakini kwa kuwa vazi liko katika mambo ya utamaduni, ningeitaka wizara hii ni lipi vazi hasa linalokubalika na liwe la heshima kwa wanawake la kwenda kazini, likubalike na liwe la heshima la kwenda kazini. Sio kuvaa suruali refu na shati kwa mwanamke.

Mhe. Spika, wizara hii ina mambo mengi makubwa na magumu. Mhe. Spika, utalii ni moja katika *source* ya uchumi wetu. Mhe. Spika, mimi mengi nimeyashuhudia, kwa wakati huo mgeni anapoingia *Airport* pale akiteremka, apewe kitenge avae, au vyenginevyo abakie katika ndege. Wala ilikuwa hawalalamiki wala hawapigi kelele ya kusema kuwa wanavunjiwa haki za kibinadamu. Leo imekuja hii haki ya binadamu duniani kuja kutuondolea utaratibu wetu, silka zetu, mila zetu, desturi zetu na mengineyo.

Mhe. Spika, watu wanapiga ngoma ya msewe, hivyo wanavyocheza sivyo msewe unavyochezwa, watu wanaigiza kibati hawajui, mtu aliyekuwa sio Mzanzibari vipi aujuwe mzewe na msewe ni ngoma za Wazanzibari. Lakini utakuja msewe hapo ucheze utaambiwa huu ni utamaduni wa Mzanzibari, lakini anayecheza sio Mzanzibari.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, malizia.

**Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Spika, ningeomba nimalizie na hawa watumishi

**Mhe. Spika:** Kwa kufunga hoja yako na maelezo yako.

**Mohammed Haji Khalid:** Naam. Haya. Naomba nimalizie kwa kumuomba Mhe. Waziri ajibu maswali yakidhi TVZ Pemba ili niweze kuunga mkono hoja yake hii, ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum: (Mhe. Haji Faki Shaali):** Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa muda huu mfupi ili nichangie machache sana katika hotuba hii.

Mhe. Spika, mchango wangu wa kwanza nataka nije katika hoja ya baadhi ya wachangiaji wenzangu kwamba katika hotuba hii Mhe. Waziri hakuonesha fedha ambazo zimetumiwa nyuma. Moja kwa moja katika kuomba tu fedha

**Mhe. Spika:** Waheshimwa Wajumbe, tusikilize maelezo ya Waheshimiwa Mawaziri, ambayo ni sehemu ya majumuisho.

**Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum: (Mhe. Haji Faki Shaali):** Mhe. Spika, kidogo nataka niwakumbushe wenzangu kwamba Mhe. Waziri ameeleza matumizi ya fedha za nyuma, lakini ni katika utaratibu ule wa nyuma ambao tuliupendekeza katika mwaka uliopita.

Mhe. Spika, nakumbuka mwaka jana tulikuwa tukiwalaumu sana mawaziri kwamba wanakuja na hotuba ndefu ambazo zinachokesha. Wewe ukatoa muongozo wako kwamba wajitahidi mawaziri ili hotuba ziwe tupi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, wizara hii wameitikia wito wa kufanya hotuba iliyokuwa fupi na inayoeleweka.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu Mhe. Waziri amejaribukueleza matumizi yaliyotumika nyuma, lakini kaeleza kitakwimu na kaeleza katika majadweli, ukiangalia jadweli nambari 1(a), katika ukurasa wa 7475. Pale matumizi yaliyotumiwa kwa mwaka wa fedha huu uliomaliza, kwa idara zote na taasisi zote yamelezwa, makisio yalikuwa shilingi gapi, zilizotolewa ngapi na asilimia ngapi zimepatikana. Kwa hivyo, nadhani Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, nina imani walikuwa bahati mbaya hawajaangalia kule nyuma wakaona yale matumizi ya nyuma yalivyowekwa kitakwimu.

Vile vile hata katika fedha za maendeleo kuna jadweli pale nambari moja 1(b). Mhe. Spika, katika ukurasa 76, pia waziri ameeleza fedha ambazo ziliombwa,

fedha zilizopatikana na asilimia ya fedha iliyotolewa. Kwa hivyo, nadhani yale mashaka ambayo walikuwa nayo wajumbe wenzangu kama wachangiaji watatu, nafikiri wakiangalia ukurasa huu mashaka yao yataweza kuondoka. Hilo lilikuwa la kwanza.

Mhe. Spika, pia kulikuwa na wasi wasi wa baadhi ya wajumbe waliotangulia kwamba Shirika la Utangazaji limeanzishwa lakini halijaanzishwa kisheria. Hoja yao kweli ina msingi sana, lakini ukiyasoma haya maelezo na ukija katika yale maelezo yenyewe basi utagundua kitu kimoja kilichopo, kwamba lile shirika hasa halijaanzishwa rasmi ni kama *orientation.* Kwa sababu ukiyaangalia yale malengo katika ukurasa wa 17, ukiyaangalia yale malengo yenyewe ya shirika ni karibu malengo yale yale ya televisheni na Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar, ambayo utekelezaji wake bado hauhitaji kuwepo sheria, bado ni taratibu za kawaida tu za kiserikali. Lakini kama ingekuwa wamekwenda ndani katika yale malengo na ikawa wanafanya mambo ambayo yanahitaji sheria, nadhani hapo ndio wengeweza kubeba lawama kwamba wameanzisha shirika kinyume na sheria.

Kwa hivyo, nadhani Waheshimiwa Wajumbe watakubaliana na mimi kwamba tumpe muda Mhe. Waziri, ataleta mswada katika Baraza hili kwa ajili ya shirika hili na tutaushangia na kuupitisha, ili aweze kuanzisha shirika rasmi na hapo shirika litaweza kufanya mambo makubwa zaidi ambayo yatahitaji nguvu za kisheria. Ukiyaangalia haya malengo yaliopo Mhe. Spika, ni mambo ya kawaida tu ya kiserikali wala hayahitaji kamwe kuwepo nguvu za kisheria. Hilo nilitaka wajumbe wenzangu ambao kwa bahati mbaya nadhani hawakuyaangalia yale malengo ya hili shirika. Vile vile hawakuangalia bajeti, kwa sababu hata bajeti zao, bado bajeti ya STZ, bado televisheni Zanzibar wana bajeti yao. Sasa kama ingekuwa shirika wasingekuwa na bajeti zao wala wasingekuwa na wakurugenzi, basi nadhani muundo ungebadilika ingekuwa kuna mtendaji mmoja mkubwa, pengine kungekuwa kuna mameneja wa taasisi hizi, kusingekuwa tena hata na muundo huu kama ulivyotajwa. Lakini kwa huu muundo ulivyooneshwa, fedha zilivyoombwa bado inaonekana kwamba hili halijakuwa ni shirika rasmi, isipokuwa wako njiani kuandaa Shirika rasmi la Utangazaji. Nadhani ukisoma *objective* iko wazi na inajionesha hali kama hiyo

Vile vile Mhe. Spika, nataka nimshukuru sana Mhe. Mgeni. Mhe. Mgeni kanifilisi mazungumzo yangu, ambapo kazungumza kuhusu kutangaza utalii kuwa kunahitaji pesa. Mimi nakubaliana na Mhe. Mgeni kwamba kutangaza utalii kunahitaji pesa. Kwa hivyo, hata ile hoja ya kwamba pesa ya safari kwamba ni nyingi kwenda nje milioni 48, mimi naona ni *peanut*. Kwa sababu siku hizi Mhe. Spika, hata mawaziri wanashirika katika kutangaza utalii.

Kwa mfano Mhe. Spika, Najib Balala Waziri wa Utalii wa Kenya anakwenda nje mwenyewe na watu wake wa utalii kutangaza utalii. Sasa kama waziri hana pesa za kwenda nje akafuatana na maofisa wake kwenda kutangaza utalii. Tunamuambia kwamba akatangaze utalii, sasa atakwenda kutangaza vipi ikiwa kafanyiwa bajeti ya milioni 2 ambapo hata safari moja haitoshi.

Kwa hivyo, ndio nikasema kwamba Mhe. Mgeni katusaidia sana kwa sababu yeye anatoka katika sekta ya utalii, kuonesha kwamba hizi fedha zilizotengwa kwa *promotion* ni ndogo. Kwa hivyo, nadhani hata wale wenzangu waliokuwa wakifikiria kwamba labda pesa hizi milioni 48 kutangaza utalii ni ndogo sana, kwa sababu ukichukua waziri, katibu mkuu na watendaji wengine ambao watashirikiana na Kamisheni ya Utalii kwenda kutangaza utalii hawawezi kuifanya hiyo kazi. Kwa hivyo, hata ule wasi wasi kwamba hivi fedha kuwa ni nyingi, baada ya hoja ya Mhe. Mgeni tutaona kwamba hizi fedha Mhe. Spika, ni ndogo sana.

Mhe. Spika, suala la mwisho ambalo nataka nilizungumze, tuangalie bajeti ya serikali kwa jumla. Mhe. Spika, katika bajeti ya serikali aliyoitoa Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ilionesha kwamba katika fedha za maendeleo tutatumia karibu bilioni 377,253,255, hayo ndio matumizi ya fedha zetu za maendeleo. Lakini Mhe. Spika, katika fedha hizo ambazo nimezitaja bilioni 377,000,000,000 ni bilioni 37,945,000,000 ndio itakuwa fedha zetu sisi wenyewe za ndani. Bilioni 339,308,000,000, hii itakuwa ni misaada na ruzuku kutoka nje.

Sasa Mhe. Spika, ikiwa mawaziri hawakusafiri hasa mawaziri wa sekta kama hizi, wakenda kuzitafuta hizi bilioni 339,000,000,000, kama watakaa ndani tu hapa basi hizo fedha zitakuwa hazipatikani. Kwa hivyo, ni lazima tukubali Mhe. Spika, kutumia milioni 48 ili tuweze kupata bilioni 339,000,000,000, lakini tukisema kwamba mawaziri wasitoke nje. Hasa waziri huyu. Mhe. Spika, waziri huyu tumuangalie vizuri. Kwanza waziri huyu atahitaji atoke nje kwa shughuli za utalii, waziri huyu huyu atahitaji atoke nje kwa mambo ya habari na waziri huyu huyu atahitaji atoke nje kwa mambo ya utamaduni. Sasa Mhe. Spika, waziri kama huyu kama wizara yake haitowekewa fedha za kutosha za kusafiri atashindwa kufanya kazi na malengo yake ni kwamba afanyekazi ili aisaidie nchi yake na taifa lake.

Kwa hivyo, nadhani ile hofu Mhe. Spika, ya kwamba labda hizi pesa ni nyingi nafikiri itakuwa imeeleweka kuwa ni pesa ndogo sana. Kwa sababu huyu waziri ni lazima atashiriki vikao vingi sana vya kimataifa. Mara nyingi Mhe.Spika, tutakuwa tunalalamika. Mimi ni shahidi Mhe. Spika, mara nyingi tunalalamika kwamba mawaziri wetu hawashiriki katika vikao vya kimataifa, na mara nyingi tulikuwa tukilaumu hata katika vikao vya Jumuiya ya Afrika ya

Mashariki, tulikuwa tunalalamika kwamba watendaji na wataalamu hawaendi. Ni kweli ilishatokezea nyuma kwamba watu walikuwa hawendi kutokana na uchache wa fedha, lakini tuliokuwa tukilaumu ni sisi ma-*backbenchers* na mimi wakati ule nilikuwa ni *backbenchers* Mhe. Spika.

Kwa hivyo, sisi tusipokwenda wenzetu watakwenda, watakachopata itabidi tutataka tugawane, na sisi Zanzibar tumesema tujenge utamaduni wa kwenda kujiombea wenyewe, nadhani ndio maamuzi yetu hayo tuliyokubaliana humu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ni lazima tukubali kwamba Mhe. Waziri huyu na wenzake ni lazima watoke nje ya nchi, watafute pesa na washiriki katika vikao. Kwa maana hiyo pesa iliyotengwa nadhani bado ni ndogo sana. Nakushukuru Mhe. Spika, ahsante.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, nilipenda sana walioomba wote wapate nafasi ya kuchangia ili kumsaidia sana Mhe. Waziri katika bajeti hii ya wizara yake. Lakini muda wetu umekuwa finyu kidogo na kwa hivyo niwaombe radhi sana waheshimiwa wafuatao kwamba wamekosa kabisa nafasi ya kuchangia kwa leo na kesho asubuhi pia haitowezekana.

Waheshimiwa hao ni Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Amina Iddi Mabrouk ambaye hayupo na Mhe. Hassan Hamad Omar. Waheshimiwa wajumbe hao nawaomba radhi kwamba hawatoweza kupata nafasi na wanaweza kupeleka kwa maandishi kwa Mhe. Waziri ili waweze kumsaidia.

Waheshimiwa Wajumbe, kesho asubuhi tukijaaliwa tunategemea kumsikiliza Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Naibu Waziri, ambapo baada ya hapo tumuombe Mhe. Waziri atufanyie majumuisho na tumpe hizo fedha mkikubali ili akafanyekazi ya kutengeneza mambo mengi aliyoahidi katika bajeti yake hii.

Baada ya hapo Waheshimiwa Wajumbe, sasa naahirisha kikao hiki mpaka kesho tarehe 21/07/2011 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 1:45 Usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 21/072011 saa 3:00 asubuhi)*